

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 8 Novemba, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tatu na leo ni Kikao cha Tatu. Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. *(Makofi)*

Namwita Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, uliza swali lako.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la kukosa soko la mahindi hasa kwa mikoa ile inayolima mahindi kwa wingi. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wananchi hawa ambao mpaka sasa hivi wamekata tamaa kabisa ya kulima mahindi? *(Makofi)*

Swali langu la pili, naomba kujua...

**SPIKA:** Swali moja tu.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Aah, ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakulima wa mahindi.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucia, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upo ukweli kwamba wakulima wetu wa zao hili la mahindi, zao ambalo linalimwa sehemu kubwa sana nchini kama zao la chakula na pia kama zao la biashara, tumekuwa na upungufu wa masoko yake. Awali unatambua kwamba tumeshajadili sana hapa ndani ya Bunge tutumie mfumo gani wa kuuza zao hili ambapo pia huku ndani inaonekana tunajitosheleza kwa chakula, lakini pia nyakati kadhaa kumekuwa na maeneo ambayo yamekosa chakula na kwa hiyo, tunatumia zao hilo hilo kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Kilimo alitoa maelekezo na tamko kwamba tunaruhusu wakulima kuuza na kutafuta masoko ya nje, lakini tunaruhusu pia nchi jirani ambazo zina upungufu wa chakula kuja nchini kununua chakula. Jambo muhimu ambalo tunataka kwenye eneo hili na tunalisimamia, pamoja na kutoa ruhusa hiyo, nchi lazima itambue tunatoa mahindi kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameweka utaratibu kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya walioko kwenye maeneo ambako mahindi haya yanatoka ili yule ambaye amepata soko nje au kama kuna mkulima amepata mnunuzi kutoka nje, basi kuwe na utaratibu wa kutoa taarifa au kuripoti kwa Mkuu wa Wilaya mwenyeji, tuwe na takwimu ya kiasi gani cha chakula kimetoka nje. Kama kimeuzwa, tuwe na taarifa za bei za upande huo ili tujiridhishe

kwenye taarifa zetu kwamba zao hili kwa mwaka huu wa kilimo tumeingiza dola kiasi fulani cha fedha ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, muhimu zaidi ni kwamba kibali cha kuza nje kipo na kibali cha kuruhusu mataifa ya nje kuja ndani kipo. Wizara inaendelea kufuatilia pia mahitaji ya chakula cha ndani ili tusije tukatoa chakula chote Taifa likabaki halina chakula tukaanza kuhangaika baada ya kuwa tumetoa chakula nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maeneo yote yanayolima mahindi, kwanza, Serikali kupitia Kitengo chetu cha *NFRA* kilitoa fedha siyo nyingi, lakini tulienda kununua katika maeneo mbalimbali na bado wakulima wana mahindi mengi. Kwa ruhusa hii, sasa mataifa ya nje na sisi tunaweza kwenda kuza nje na utaratibu huo unaendelea kusimamiwa na Wizara ya Kilimo kupitia Kitengo chake cha *NFRA*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mlowe, swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi tena niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo hili lililojitokeza la ukosefu wa soko la mahindi na kusababisha wananchi wauze kwa bei ya chini sana na kukosa pesa za kuweza kununulia pembejeo, je, Serikali sasa iko tayari kushusha bei ya pembejeo kwa wananchi hawa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tena nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lucia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la gharama ndogo au upatikanaji kwa bei ndogo ya pembejeo limefanyiwa kazi vizuri sana na Wizara. Nasema hili kwa sababu awali mbolea

tulikuwa tunaagiza *randomly*, kila mmoja anaagiza na kuleta nchini na kwa hiyo kila mmoja alikuwa anaweza kuuza kwa bei ya juu sana, lakini Wizara imekuja na mkakati mzuri wa kuagiza kwa pamoja. Tumetafuta mzabuni mmoja awe analeta mbolea yote nchini, yeye awe ndiyo anasambaza kwa wenzake kwa udhibiti wa bei ambao umewekwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunapata mbolea karibu asilimia 40 ya bei ya awali ambayo ni ndogo ukilinganisha na zamani. Bado tuna mjadala wa namna bora ya kufikisha pembejeo kwa mkulima, ikiwemo na mbolea kule kijijini ili aipate kwa urahisi lakini kwa bei ile ile ambayo sisi Serikali tunasema ni muhimu mfuko wa mbolea wa aina hii upatikane kwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wizara imeendelea kuratibu kupatikana kwa mbolea kwa bei nafuu lakini kwa wakati ambapo pia wao wameshaamua na sasa wanasimamia kupeleka mbolea kwenye maeneo kulingana na msimu angalau mwezi mmoja, miwili kabla ya msimu haujaanza. Kwa hiyo, tunaendelea kuratibu vizuri kumwezesha mkulima aweze kupata pembejeo ikiwemo mbolea kwa bei rahisi, kwa wakati na pia katika mazingira ambayo siyo magumu sana kwa sababu wafanyabiashara wako tayari na wameanza kuleta pembejeo pia.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii kwa kumbukumbu zangu kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Kilimo, tumeshaleta pembejeo kwa maana mbolea zaidi tani 260 ambazo zinakaribia asilimia 60 ya mahitaji ya nchi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na wakulima wote wa mahindi na wakulima wa mazao karibu yote nchini, Wizara inaendelea kuratibu vizuri upatikanaji wa pembejeo wa kila zao ili wakulima waweze kufanya kazi yao ya kilimo katika mazingira rahisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla ya swali langu, naomba nitoe pongezi kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa jinsi inavyoshughulikia mambo mbalimbali na hasa hivi karibuni lile janga la kuzama kwa MV...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, maswali kwa Waziri Mkuu ni moja kwa moja swali ili tuweze kuokoa muda.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali langu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi au niseme watumishi kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya likizo zao. Sijui Serikali imejipangaje kutatua tatizo hili la muda mrefu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anazungumzia matatizo makubwa ya malimbikizo ya watumishi na ulipaji wake. Ni kweli kwamba Serikali imejikita katika kuratibu maslahi ya watumishi wetu ikiwemo kupanda madaraja, masuala ya mishahara na pia hata malimbikizo ikiwa ni sehemu ya madeni ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ilitenga fedha kwa ajili ya kulipa malimbikizo haya ambayo yanatokana na kupanda kwa madaraja, lakini pia madeni mengine ya utumishi kwenye sekta hiyo kama alivyosema ya likizo na kumbukumbu zangu zinaonesha na juzi nilikuwa Lushoto nilizungumza na wafanyakazi, niliwapa takwimu kwamba kuanzia mwezi wa Julai mpaka Septemba, 2018

Serikali ilishalipa madeni mbalimbali yakiwemo malimbikizo ya watumishi ya shilingi bilioni 184.9. Hiyo ikiwa ni awamu ya tatu ya malipo mbalimbali yaliyoanza toka mwaka 2017. Kwa hiyo, lazima hapo sasa watumishi waone kwamba Serikali inaendelea kulipa malimbikizo mbalimbali ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia suala la likizo ni sehemu ya malipo ambayo TAMISEMI inaratibu vizuri kwa kupokea taarifa ya idadi ya watumishi kwa Idara kutoka kila Halmashauri nchini kwa wanaokwenda likizo miezi mitatu/minne kabla. Serikali kutokana na fedha ambayo imetenga, inapeleka fedha kwenye Halmashauri hiyo, kwa hiyo, ni juu ya Afisa Utumishi na Mkuu wa Idara kuratibu watumishi wangapi wanakwenda likizo.

Mheshimiwa Spika, Idara nyingine hazina shida, shida tunayo sana katika sekta ya elimu na sekta ya afya ambazo zina watumishi wengi. Kwa hiyo, Wakuu wa Idara na Maafisa Utumishi wetu ndani ya Halmashauri na Wizara wamepewa maelekezo maalum ya kuratibu likizo zao vizuri ili kila mmoja aweze kulipwa nauli ya kwenda kwake.

Mheshimiwa Spika, kwenye likizo uratibu huo unaendelea. Mkakati wa Serikali ni kwamba kama likizo inaanza tarehe 1, basi tunataka tarehe 30 mtumishi apate hundi yake na malipo ya nauli kwenda nyumbani kwake ili tarehe 1 aanze likizo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali imejipanga vizuri, kwanza, tumedhibiti kuzalisha madeni, lakini pili, yale machache yaliyopo, yote tunayalipa. Kwa utaratibu huu, yale ya mwanzo yote ndiyo hayo ambayo nimesema tumelipa shilingi bilioni 184.9 ili kuweza kukamilisha kulipa madeni yote ya watumishi. Zoezi hili linakuja baada ya kuwa tumekamilisha utafiti au uthamini kwa maana ya uhakiki wa madeni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayo takwimu ya madeni na tunaendelea kuwalipa. Watumishi nchini

waendeleo kuiamini Serikalini yao, waendeleo kuamini utaratibu tunaotumia ili kutuwezesha Serikali kulipa madeni kwa wale wote wenye stahiki zao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwakasaka, swali la kwanza baada ya maswali ya Waziri Mkuu linahusu mambo haya ya watumishi, kama utakuwa na swali la nyongeza nitakupa nafasi wakati huo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Maftah Abdallah Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali imeweka utaratibu wa kutangaza bei elekezi za mazao ya kilimo. kwa mfano katika zao la korosho mwaka huu kulitangazwa bei elekezi na Serikali ikatoa maelekezo kwamba wanunuzi waweze kununua zao la korosho, lakini walivyoenda kununua kwenye minada ile bei ilikuwa ni ya chini sana hali iliyopelekea wakulima kugomea kuuza zao la korosho kwenye minada ile. Baadae Serikali kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akatoa kauli kwamba Serikali inaweza kununua...

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Maftaha, ngoja kwanza Sheikh yaani hotuba acheni, ni swali.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Sawa Mheshimiwa Spika, nilikuwa najenga hoja.

**SPIKA:** Acha kujenga hoja, wewe uliza swali.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kutoa maelekezo kwamba inaweza kununua zao la korosho, nataka kujua kauli hii ya Serikali imetekelezwa kwa kiasi gani mpaka leo, kwamba ni tani ngapi za korosho zimeweza kununuliwa na Serikali? Ahsante.

**SPIKA:** Katika maswali yenu Waheshimiwa Wabunge tunaambiana kila wakati, ukimuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu tani ngapi au kiasi gani kimenunuliwa wakati mpaka jana tulikuwa naye hapa Bungeni, swali la takwimu, tunategemea majibu kweli? Kwa yale mengine Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali kuhusu kilimo cha korosho.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maftaha, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, najua anataka kujua mwenendo wa zao la korosho na mfumo wa mauzo ambao sasa unaendelea kupitia minada yetu, mfumo ambao Serikali imeweka dhamira ya dhati kwenye mazao haya, korosho ikiwemo kuyauza na kuwawezesha wakulima kupata tija kutokana na kilimo hiki ambacho wanakilima. Tuliweka utaratibu wa minada ambao unawezesha wafanyabiashara kuja kununua kwa namna ya ushindani na hiyo ndiyo iliyowezesha zao hili la korosho miaka mitatu, minne iliyopita kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu kumekuwa na dosari hiyo kama alivyoeleza kwamba minada yetu haikuwa mizuri kutokana na mabadiliko ya bei kwenye soko la dunia. Hata hivyo, wataalamu wetu walioko kwenye vitengo walishauri na walitoa maelekezo kwamba bei ambayo inanunuliwa kwa sasa ni ya chini sana ambapo inatakiwa bei ya chini kuwa shilingi 3,000. Ndiyo sababu Mheshimiwa Rais baada ya mazungumzo na wadau ambao ni shilingi 3,000.

Mheshimiwa Spika, siwezi kujibu tani ngapi, lakini minada imeshaendeshwa katika kila Chama Kikuu cha Ushirika na bado inaendelea ingawa idadi ya wanunuzi, viwango wanavyotenda ni vidogo sana ukilinganisha na idadi ya korosho iliyoko kwenye maghala. Nini Serikali tunafanya? Serikali tunazungumza na mataifa makubwa moja kwa moja ambako pia tunaendelea kuzungumza na tunaanza kuona nia ya wanunuzi wakubwa kuja kuchukua korosho. Leo hii kutakuwa na kikao na baadhi ya wanunuzi



kati ya Wizara na Waziri yuko hapa, akishatoka hapa saa 5.00 asubuhi atakuwa nao kuendelea kujua nani anaweza kununua korosho kiasi gani? Kwa hiyo, baada ya kupata mauzo yale na takwimu zikija, tunaweza kukujibu sasa ni tani ngapi tumeuza.

Mheshimiwa Spika, nitoe salamu na ujumbe kwa wakulima wetu na Waheshimiwa Wabunge ambao wanatoka kwenye maeneo hayo ya korosho kwamba waendeleo kuwa wavumilivu, watulivu, kwani korosho tunaitafutia masoko na Serikali tunajitahidi kuhakikisha kwamba zao hili linanunuliwa. Kama ambavyo tumefanya kwenye zao la kahawa ambako pia kulikuwa na kusuasua sana na wakulima walikaa muda mrefu mpaka tulipoweka utaratibu mzuri, sasa kahawa yote imeondoka.

Kwa hiyo, mazao haya yote ambayo tunayalima na tunayatafutia masoko, tunazo changamoto hizo ambazo ni za kidunia, tunaendelea kukabiliana nazo na tunaratibu vizuri na Wizara yetu inaendelea kufanya hivyo vizuri. Tuwahakikishie katika kipindi kifupi kijacho, kama ambavyo tumetatua tatizo la kahawa na tumbaku, pia kwenye korosho tutafanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wako hapa najua wana *forum* nzuri ya kuwasiliana na wakulima, tumeagiza Wakuu wa Mikoa waendeleo kuwatuliza wakulima na tunashukuru angalau wametulia, nasi Serikali tunaendesha taratibu zetu kwa haraka ili zao hili tulitoe haraka sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, swali langu la msingi nililotaka kuuliza limeshaulizwa na Mheshimiwa Mlowe, ambalo

lilikuwa linahusiana na suala la kupanda kwa bei za pembejeo za kilimo lakini zaidi ya asilimia 90 ya mbolea tunaagiza nje, Serikali imeweka mazingira gani mazuri ya kuwahamasisha wawekezaji ili kuweza kufungua viwanda vingi vya mbolea ndani ya nchi yetu ili bei iweze kupungua? (Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu mzuri wa uwekezaji wa sekta zote kwa kujenga viwanda, lakini pia pale ambako tunahitaji uzalishaji wa bidhaa mbalimbali na masoko yake kwa wawekezaji wenyewe, tumetengeneza mazingira mazuri. Kwa eneo la ujenzi wa viwanda vya mbolea, ni kweli tuna idadi ndogo sana ya viwanda, lakini Serikali tumeendelea kutoa wito kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vinavyozalisha mbolea hapa nchini ili tupate mbolea nyingi ya kutosha hapa hapa nchini. Kwa sasa tuna viwanda vichache sana kikiwemo kile cha Minjingu ambacho kinazalisha lakini bado hakijafikia uzalishaji kulingana na mahitaji ya nchi. Kwa hiyo, tunalazimika sasa kutafuta namna nzuri ya kuleta mbolea nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, bado tuna nafasi ya ujenzi wa viwanda viwili. Kimoja kitajengwa Kilwa na kampuni moja kutoka Ujerumani lakini kampuni nyingine kutoka Ujerumani inajenga kiwanda Mtwara. Hivi vipo tayari na sasa hivi wanaendelea na makubaliano ya mifumo ya kifedha na malipo ili waweze kuwekeza. Kwa hiyo, tutakuwa na viwanda vitatu vikubwa ambavyo vitakuwa vinazalisha mbolea.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba viwanda hivi viwili vikianza kazi pamoja na Minjingu uzalishaji utakuwa mzuri na kiwango cha mahitaji kutoka nje kitapungua. Kwa hiyo, tutaendelea kupunguza kiwango cha mahitaji kutoka nje ili tujitegemee ndani wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mazingira mazuri ya uwekezaji ni kwamba tumewapa ardhi, lakini pia tumetoa motisha kadhaa kwa wawekezaji wetu na tunawapa ushirikiano katika ujenzi wa viwanda hivi kutokana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maana ya mikoa mahali walipo na kupitia Wizara ya Kilimo nao pia wanaendelea kufanya mawasiliano ya kuweza kuimarisha ujenzi wa viwanda hivyo.

Kwa hiyo, mazingira hayo tunaamini tutaweza kupata viwanda na wengine ambao wana nia ya kuja kujenga viwanda nchini, tunawakaribisha waje kujenga viwanda vya mbolea ili nchi iweze kuwa na mbolea ya kutosha. Ahsante. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa wana taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ilikuwa asiwepo leo asubuhi, ndiyo maana hawakuweza kujiandikisha. Lakini kwa vile, tuna dakika kidogo, basi natoa nafasi kwa mtu mwenye *pressing question*. Nilikuona Mheshimiwa uliza swali lako.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Zanzibar.

**SPIKA:** Hapana, hapana, hapana. Nani tena kule nyuma? Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama tunavyojua Tanzania sasa hivi tunakwenda kwa kasi zaidi katika ujenzi wa viwanda. Jambo kama hilo vilevile kwa upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limechukuliwa kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni mwekezaji wetu wa ndani, Mheshimiwa Bakhresa katika ule mlolongo wa kujenga viwanda, alijenga kiwanda Zanzibar na ameajiri vijana wetu wengi. Katika *process ya production, all of a sudden* katikati

*regulations* zikawa zimebadilika kwa *importation* ya maziwa ambayo anazalisha Zanzibar anayaleta Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu anatoa gauli ya Serikali kutokana na changamoto hiyo iliyotokea na ambayo itadumaza sana uchumi hususan kwa upande wa Zanzibar? (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa kuwa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yanapaswa kuwa ya kisera, hebu liweke kisera badala ya kuwa ni *event* ya mfanyabiashara binafsi. Unachotaka hasa hapo ni sera ipi Mheshimiwa Saada?

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nachotaka ni *implementation* nzuri sana kwa pande mbili zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye sera yetu ya ujenzi wa viwanda kuelekea katika uchumi wa kati. Kumekuwa kuna changamoto hususan uimara wa uzalishaji unaotokana na viwanda ambavyo vipo Zanzibar vinavyoleta *products* zake Tanzania Bara. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saada Mkuya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanzania Visiwani (Zanzibar) ikiwemo tunahamasisha ujenzi wa viwanda kwa maeneo kulingana na uzalishaji na fursa zilizopo kwenye maeneo hayo. Viwanda hivi vipo vya kilimo, maliasili na madini. Kwa hiyo, wawekezaji wapo huru kuchagua ujenzi wa viwanda kulingana na mahitaji yake lakini na fursa ambayo ipo kwenye pembe za nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa viwanda vilivyopo Zanzibar na Bara ni vyetu sote na viwanda vya Zanzibar vina usimamizi na Waziri wa Viwanda na Biashara aliyeko Zanzibar anasimamia sera na namna ya ujenzi wa viwanda kule Zanzibar. Tunapokuja kwenye masoko na kuondoa

changamoto za kati ya Bara na Zanzibar, hili lilipotokea kwenye zao la sukari na uzalishaji wa maziwa, tumelazimika kuwataka Mawaziri wetu wote wawili; wa Mifugo wa Bara na Zanzibar, Waziri wa Kilimo wa Bara na Zanzibar na vilevile Waziri wa Viwanda wa Bara na Zanzibar wakae watengeneze utaratibu mzuri ambao utawezesha kuondoa changamoto zinazokwamisha kuendeshwa kwa biashara zetu kwa bidhaa zinazozalishwa hapa ndani. Vilevile wafanye mapitio ya sheria tulizonazo ambazo pia wakati mwingine siku za nyuma zimekuwa zikitukwaza ili tuondoe mazingira hayo ili Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili tumeliacha mikononi mwa Mawaziri na wanaendelea na mijadala yao. Watakapomaliza mjadala huo tutajua maeneo yaliyokuwa na changamoto yametatuliwa kwa kiasi gani? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe swali la mwisho.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumeshuhudia Balozi wa *EU* akiwa ameitwa nyumbani kwenda kufanya majadiliano na nchi yake kutokana na mahusiano kati ya nchi yake pamoja na Tanzania. *(Makofi)*

Sasa swali langu, ni nini msimamo wa Serikali kuhusiana na mahusiano yetu na jumuiya za Kimataifa?

**SPIKA:** Napata taabu kuliruhusu hili swali kwa sababu kwa maelezo yako ni kwamba alitwa huko kwao, sasa kama alitwa kwao, unataka Waziri Mkuu ajibu nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru. Huo ndiyo mwisho wa kipindi cha maswali, unaweza sasa kupumzika. Ahsante sana, muda wa maswali umekwisha. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.  
(Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa muda huu uliotupatia. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya Kawaida, tunaanza na Ofisi ya Rais, (Utumishi na Utawala Bora), swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, tafadhali.

Na. 29

#### **Watumishi wa Umma Kutopandishwa Madaraja**

**MHE. JORAM I. HONGOLI** aliuliza:-

Watumishi wa umma walioajiriwa mwaka 2012 hawajapandishwa madaraja mpaka leo hii.

Je, ni lini watumishi hao watapandishwa madaraja?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMM NA UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Hongoli, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa mwaka 2012/2013 jumla ya watumishi wa umma 37,388 walijajiwa. Kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi, watumishi hao walitakiwa kuwa kwenye kipindi cha majaribio kwa muda wa mwaka mmoja hadi kufikia mwaka 2013/2014 na walitakiwa kutumikia cheo kimoja kwa kipindi cha angalau miaka mitatu baada ya kuthibitishwa kazini.

Mheshimiwa Spika, watumishi hao walistahili kupandishwa madaraja kuanzia mwaka 2016/2017 iwapo wangekidhi sifa muhimu za kimuundo kama utendaji mzuri wa kazi, kukidhi matakwa ya muundo husika wa maendeleo ya utumishi, kuwepo kwa nafasi wazi pamoja na uwepo wa bajeti iliyoidhinishwa. Hata hivyo, watumishi hao pamoja na watumishi wengine hawakuweza kupandishwa kutokana na Serikali kutekeleza zoezi la uhakiki wa watumishi hewa na vyeti vya elimu ya sekondari na ualimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa zoezi hili la uhakiki wa watumishi hewa na uhakiki wa vyeti, Serikali imepandisha madaraja watumishi wakiwemo walioajiriwa mwaka 2012/2013 kwa awamu kama ifuatavyo:-

(a) Awamu ya kwanza ilihusisha upandishaji vyeo watumishi 28,049 waliokuwa wameidhinishwa vyeo vyao kabla ya kutekeleza zoezi la uhakiki wa watumishi hewa na uhakiki wa vyeti kuanzia mwezi Juni, 2016.

(b) Awamu ya pili ilianza mwezi Novemba, 2017 na ilihusisha watumishi 59,967 ambao taarifa zao za kiutumishi zilikuwa kwenye Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*HCMIS*) kabla ya zuio tajwa.

(c) Awamu ya tatu ilianza mwezi Aprili, 2018 na ilihusisha watumishi 25,504 ambao barua zao zilikuwa hazijaingizwa kwenye mfumo tajwa.

Mheshimiwa Spika, bakaa ya watumishi walioajiriwa mwaka 2012/2013 na wengine ambao walistahili kupanda kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 imeendelea kukasimiwa

bajeti ya mishahara ili waweze kupandishwa vyeo katika mwaka huu wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, waajiri wanaelekezwa kukasimu bajeti ya kupandisha madaraja ya watumishi kwa kuzingatia ikama iliyoidhinishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali ameridhika? Endelea kama una swali.

**MHE. JORAMI I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini bado naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa sababu kwa utaratibu wa kupandisha madaraja kwa awamu, kuna baadhi ya watumishi ambao watakuwa wameanza kazi pamoja itafika muda watakuwa na *gap* la mwaka mmoja au miaka miwili hivi. Nataka nijue kauli ya Serikali ni namna gani mta-*harmonize* kuhakikisha kwamba mwisho wa siku hawa watumishi wanamaliza wakiwa na uwiano sawa wa madaraja, kwa sababu wana sifa sawa na wote walistahiki kupandishwa kwa wakati huo ule mwaka 2016/2017?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na malalamiko na manung'uniko kwa baadhi ya watumishi kwamba Kitengo cha Idara ya TAMISEMI kinacho-*approve* upandishwaji wa madaraja kimekuwa kikichelewa sana. Nataka nipate kauli ya Serikali ni namna gani au kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba kitengo kile kinafanya kazi kwa wakati ili tuondoe haya manung'uniko na watumishi waweze kufanya kazi wakiwa na morali nzuri kabisa kwa sababu kunapokuwa na malalamiko ya kucheleweshwa kwa muda mrefu, baadhi ya watumishi utendaji wao kazi unapungua kwa kunung'unika na kusikitika kwamba wanacheleweshwa kupandishwa madaraja yao. Nataka nijue mkakati wa Serikali. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Swali hili ni muhimu sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Karibu ulijibu, kwa sababu walioajiriwa mwaka 2012



walitakiwa wapande 2015, mwaka 2018 walitakiwa wapande mara ya pili, huyo mtumishi hajapanda, wenzake wengine walipanda kule mwaka 2015. Miaka inavyoenda sasa hawa watakuja kukutana wapi? Hii ni kero kubwa katika Majimbo yote kwa upande wa watumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hongoli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna wakati ambapo imetokea wale walioajiriwa pamoja ambao walistahili kupanda kwa pamoja wamekuwa hawapandi kwa pamoja kwa sababu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Spika, ili mtumishi aweze kupanda, kuna masuala ya kiutumishi ambayo lazima ayatimize. Wakati mwingine inakuwa *case to case*, lakini katika hali ya kawaida kama sifa zote zinalingana na amejaza fomu kwa mujibu wa taratibu kama inavyotakiwa, hakika Serikali haimuachi awaye yeyote kwa sababu wanapopandishwa hawapandishwi kwa upendeleo. Kama kuna *cases* za watumishi ambao wanadhani kwamba walistahili kupandishwa, hawakupandishwa kwa sababu ambazo hawazielewi ni vizuri labda tukali-*address* tatizo kwa sababu ni *case by case*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, anasema kumekuwa na ucheleweshaji kwa maana ya *approvals* kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ni kweli kuna malalamiko ambayo yamekuwa yakipokelewa na hata juzi nilikuwa nafanya mawasiliano nao, kuna malalamiko ambayo tumepokea, kuna watumishi ambao walistahili kupandishwa lakini hawakupandishwa. Pia kuna kazi ambazo Maafisa Utumishi wa Halmashauri zetu hawatimizi wajibu kwa wakati. Kwa hiyo, nawataka Maafisa Utumishi, ni wajibu wao

kuhakikisha kwamba zile taarifa sahihi ambazo zinatakiwa, ziletwe Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili watumishi waweze kupata haki zao wazifanye kwa wakati na bila kubabaisha.

**SPIKA:** Swali hili bado halijatendewa haki. Mheshimiwa Naibu Waziri sisi tutakachoomba Alhamis kama leo, tupate takwimu za watumishi walioajiriwa mwaka 2012 ambao mpaka 2018 hawajapandishwa vyeo wa TAMISEMI tu peke yake, tutalirudisha tena swali hili Alhamisi ijayo. Kwa sababu kuna watu fulani wazembe wanaoshughulika na mambo haya, tukiona takwimu tutaona tatizo ni kubwa kiasi gani, tutalipangia Alhamisi ijayo. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya.

Na. 30

### **Uhitaji wa Gereza katika Wilaya ya Rorya**

**MHE. LAMECK O. AIRO** aliuliza:-

Eneo la Rorya lina ukubwa wa kilometa za mraba 9,345, eneo la ziwa likiwa asilimia 78, nchi kavu ni asilimia 22 na shughuli kubwa zinazofanyika katika eneo hili ni uvuvi, kilimo, ufugaji na biashara. Idadi ya watu katika eneo hilo ni takribani 400,000 (sensa mwaka 2012) hadi sasa Wilaya inategemea kutumia Gereza la Wilaya ya Tarime ambalo linahudumia wahalifu wote wa Rorya na Tarime hasa ikizingatiwa kuwa shughuli zinazofanywa kwenye maeneo haya zinahusisha pia majirani zetu kutoka Uganda, Kenya na kadhalika, hivyo uhalifu kutokea kwa wingi ni jambo lisiloweza kuzuilika.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Gereza Wilaya ya Rorya?

**SPIKA:** Majibu ya swali, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Injinia Masauni, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rorya ni miongoni mwa Wilaya 52 nchini ambazo hazina magereza. Ni azma ya Serikali kujenga Magereza katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Rorya. Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa magereza ambapo ujenzi wake umeshaanza, kwani kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kukamilisha miradi ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lakairo.

**MHE. LAMECK O. AIRO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Wilaya ya Rorya na Tarime nafikiri Serikali iliona umuhimu kuweka Polisi Kanda Maalum. Wilaya ya Rorya ina *OCD* watatu; wa Kinesi, Utegi na Shirati.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuweka kipaumbele cha kuwa na gereza sehemu hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tarehe 4 kuamkia tarehe 5, Kijiji cha Nyamasanda waliibiwa ng'ombe na walifuatilia mpaka kwenye Wilaya jirani ya Tarime. Pale palitokea purukushani, watu wakaanza kurushiana mishale na mtu mmoja akakatwa mapanga na mpaka sasa yupo Hospitali ya Poaki. Kwenye eneo hilo ilikuwepo gari ya polisi kwenye Kituo cha Tatwe ambalo ilikuwa ikihudumia maeneo ya Kituo cha Polisi Kogaja na Panyakoo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lakairo umeanza *story*.

**MHE. LAMECK O. AIRO:** Mheshimiwa Spika, *sorry*. Hiyo gari ilichukuliwa na Mkuu wa Polisi Kanda Maalum ikaenda kufanya *operation* kule Nyamongo. Je, hii gari itarudishwa lini ili kufanya doria kwenye maeneo hayo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Lakairo, swali lako la msingi linasema, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Gereza Wilaya ya Rorya? Sasa habari ya magari na swali lako la msingi havina uhusiano kabisa.

Mheshimiwa Naibu Waziri kwa lile swali la kwanza kwamba Kanda Maalum kuna ma-*OCD* watatu halafu gereza limebanana na unajua kabisa kule kwa kweli kunahitajika gereza, unasemaje Mheshimiwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba kuna haja ya kuongeza gereza katika Jimbo la Rorya ama Mkoa wa Mara kwa ujumla. Kama ambavyo nimemwambia katika jibu langu la msingi ni kwamba tutaweza kufanya hivyo pale ambapo tutakuwa tayari kifedha na kibajeti. Kwa sasa hivi tuna changamoto ya zaidi ya maeneo 52 ikiwemo eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge anatoka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na umuhimu huo, lakini pale ambapo tutakuwa tumefanikiwa kupata fedha, basi tutazingatia maombi yake.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali linaulizwa na Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, tafadhali.

Na. 31

**Upungufu wa Madaktari Bingwa Hospitali ya Rufaa  
Kitete - Tabora**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete, ina upungufu wa Madaktari Bingwa na Wauguzi. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam hao katika hospitali hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, anakuja Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, karibu tena kwa mara nyingine.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kabla sijatoa majibu ya swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kusimama mahali hapa kwa mara nyingine tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote kwa ujumla na pia kwa namna ya kipekee Madaktari wa Kituo cha Afya Magugu, Hospitali ya *Mount Meru*, Hospitali ya Selian na Hospitali za Muhimbili kwa hunihudumia na hatimaye leo naweza kusimama hapa tena. Nawashukuru sana kwa dua zenu na maombi mbalimbali mliyonyanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora (Kitete) ina Daktari Bingwa mmoja ambaye ni Daktari Bingwa wa Watoto (*Pediatrician*). Aidha, wapo madaktari bingwa wengine watatu ambao wamemaliza masomo yao, mmoja akiwa ni Daktari Bingwa wa Watoto na wengine wawili ni Madaktari Bingwa wa Mifupa (*Orthopaedic Surgeons*). Madaktari hao watatu wanafanya kazi kama madaktari wa kawaida wakati taratibu za kiutumishi za

kuwabadilisha vyeo (*re-categorization*) zikiendelea baada ya kuhitimu mafunzo yao katika fani ya ubingwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wauguzi, wapo jumla ya Wauguzi 135; kati yao Maafisa Wauguzi ni wawili, Maafisa Wauguzi Wasaidizi 67 na Wauguzi 66. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya Wauguzi 28 wameajiriwa na Serikali kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora. Kati ya hao, Maafisa Wauguzi ni watatu, Maafisa Wauguzi Wasaidizi ni 13 na Wauguzi 12. Serikali itaendelea kuboresha rasilimali watu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Kitete kadri vibali vya ajira vitakavyokuwa vinapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Daktari Bingwa mmoja katika mahitaji ya Madaktari Bingwa 26 mpaka 35, haifiki hata robo. Mwaka 2017 niliuliza swali kama hili na nikajibiwa kwamba mpaka mwezi Novemba, 2018 tunaweza tukawa tumeongezewa madaktari saba na mpaka sasa hakuna. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba Tabora, hasa Hospitali yetu ya Kitete ipatiwe upendeleo wa makusudi ili Madaktari Bingwa waweze kuwepo kwenye hospitali ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa katika majibu ya Mheshimiwa Waziri ameongelea suala la vibali akisema kwamba vitakapopatikana, sijui kwa nini hawawi *specific* na muda kwa sababu hili neno kwamba "vibali vitakapopatikana" na hapa tunaongelea maisha na afya ya wanadamu, vibali hivyo vinachukua muda gani? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):**

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Afya ilikuwa ni kuongeza madaktari saba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora yaani Hospitali ya Kitete na katika vibali vilivyotoka hivi karibuni Hospitali ya Mkoa wa Tabora ilipata jumla ya watumishi wapya 50 ambao walijiriwa na katika hao, watumishi 40 tayari wamesharipoti. Katika hao watumishi 40 ambao wameshakuripoti, madaktari ni watano, hawa ni madaktari wa ngazi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika vibali vile kulikuwa kuna Madaktari Bingwa hao saba ambao anawazungumzia ambapo tayari wawili wamesharipoti na sasa tunasubiria mgao mpya ili tuweze kupeleka hao madaktari wengine kukamilisha idadi ya madaktari wanaohitajika. Hospitali ile ina upungufu wa Daktari Bingwa wa Upasuaji *(General Surgeon)* na Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Magonjwa ya Akina Mama *(Obstetricians)* na hao ndiyo ambao watapelekwa katika awamu hii ya pili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vibali, hili ni suala ambalo linaendana na mzunguko mzima wa bajeti ambapo Serikali inaajiri kadri ambavyo uwezo wake wa kibajeti unavyoruhusu. Kwa hiyo, kusema tutatoa muda muafaka, maana yake muda muafaka huwa ni kila bajeti inapopitishwa na Bunge letu tukufu, basi ndiyo mwanzo sasa wa mchakato wa kuongeza watumishi unakuwa umefikiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunashukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu.

Mheshimiwa Mwakasaka, Mheshimiwa Waziri alisema kwenye majibu yake ya msingi, kuna baadhi ya Madaktari Bingwa ambao tayari wapo ila hawajawa *re-categorized*. Sasa hili ndiyo kama lile la Utumishi la TAMISEMI, yaani mtu ni Daktari Bingwa, yupo anafanya kazi, *re-categorization* haifanyiki, si unamvunja moyo? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hii hii na swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

Na. 32

## Ongezeko la Ugonjwa wa Kisukari

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa kisukari nchini, aidha, baadhi ya watoto wanazaliwa wakiwa na ugonjwa huo.

Je, Serikali ipo tayari kufanya uchunguzi na kueleza chanzo cha ugonjwa huo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hili, bado tuko na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, tafadhali Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kisukari ni mojawapo kati ya magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza. Tafiti nyingi za kubaini chanzo cha ugonjwa huu zimeshafanyika ambapo ilibainika kuwa ugonjwa huu husababishwa na sababu kuu tatu. Mosi, mwili kushindwa kutumia sawasawa kichochezi cha *insulin* mwilini. Hii hutokana na kongosho kushindwa kutengeneza kabisa *insulin* au kongosho kufanya kazi chini ya kiwango. Pili, mfumo wa kinga (*autoimmune system*) kuharibu kwa bahati mbaya seli kwenye kongosho zinazotengeneza *insulin*, hivyo kulifanya kongosho lisifanye kazi yake. Tatu, *hormone* zinazozalishwa na mwili wakati wa ujauzito (*insulin blocking hormones*) zinaweza kuzuia *insulin* kutoka ila kisukari hiki huweza kupotea baada ya mama kujifungua.



Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wananchi kujikinga na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kuzingatia mtindo bora wa maisha na ulaji unaofaa kwa kufanya mazoezi ili kupunguza uzito uliozidi na unene uliokithiri. Aidha, wananchi wanaaswa kuwa na tabia ya kupima afya mara kwa mara na kuwahi kwenda kwenye vituo vya afya kwa ajili ya matibabu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rukia nilikuona.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa mara nyingi mtu anapojijua ana ugonjwa huu wa kisukari tayari inakuwa ilishamuathiri, kama vile baadhi yao kupoteza nuru ya macho au kupofuka, wanaume kupoteza nguvu za kiume, jambo ambalo linawaathiri sana kisaikolojia.

Je, Serikali sasa iko tayari kuweka vipimo vya ugonjwa huu wa kisukari katika hospitali zetu kuanzia ngazi ya kata, wilaya na kadhalika ili watu waweze kujijua mapema? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna baadhi ya maradhi tayari yamepatiwa kinga, je, Serikali sasa iko tayari kutafuta kinga ya maradhi haya kama tulivyopatiwa kinga ya homa ya ini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rukia, wewe unajuaje kama wanaume wanaathirika? *(Kicheko/Makofi)*

Majibu ya maswali hayo Waziri Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza linahusu uwepo wa vipimo mpaka ngazi ya kata. Serikali iko tayari na inafanya

hivyo. Vipimo vya kupima kisukari vinapatikana mpaka kwenye ngazi ya kata, nikimaanisha kwenye ngazi ya Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kinga, kama ambavyo tunapatiwa kinga ya ugonjwa wa homa ya ini, Serikali imeendelea kuongeza idadi ya kinga ambazo zinapatikana hapa nchini na ushahidi ni hii kinga ya homa ya ini ambayo siku za nyuma ilikuwa ikitolewa kwa wataalam ambao wanatoa huduma kwenye sekta ya afya ama makundi ambayo yapo kwenye *risk* kubwa ya kupata ugonjwa wa homa ya ini, lakini sasa tunaanza kuitoa kinga ya *Hepatitis B* (homa ya ini) kwa wananchi wote na tunaanza taratibu. Ndiyo maana tumetoa wito Waheshimiwa Wabunge wawe mstari wa mbele kuanza kupata kinga hii. Siku za nyuma tulikuwa tunapata sisi madaktari tukiwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, pia chanjo nyingine tumeanza kuzileta kwa mfano *HPV* tunaanza kuwapa watoto, ni chanjo mpya, hazikuwepo huko nyuma, chanjo ya magonjwa ya kuharisha, chanjo ya magonjwa ya kifua kwa watoto wadogo hazikuwepo miaka tunazaliwa sisi, mpaka juzi hapa miaka ya 2000 lakini leo tumeanza kuwapa watoto wetu. Tumeongeza sana wigo wa kutoa chanjo hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware, nilikuona swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la magonjwa yasiyoambukiza, kisukari na saratani...

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa.

**WABUNGE FULANI:** Hasikiki.

**SPIKA:** Hasikiki eeh?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Tumia *microphone* nyingine.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

Nilianza kwa kusema kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza, mfano saratani au kisukari na matibabu yake yamekuwa ya ghali sana na siyo ya moja kwa moja. Napenda kujua nini msimamo wa Serikali katika kuboresha huduma kwa walioathirika na magonjwa haya kwenye matibabu hususan katika gharama? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo, gharama za magonjwa yasiyoambukiza.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Spika, gharama za magonjwa yasiyoambukiza (*non-communicable diseases*) ni kubwa sana kwa uhakika. Ili tupambane na gharama hizi kama Taifa, Serikali imeanzisha mkakati wa kuhamasisha watu kuishi maisha yenye afya zaidi kwa kuangalia afya zao kwa maana ya kuangalia chakula wanachokula, kufanya mazoezi na kupima afya zao mara kwa mara kwa sababu Serikali inaamini kwamba kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Spika, hivyo ili tuepukane na gharama ya kutibu, ni bora tukaingia gharama ya kuhamasisha watu wabadilishe mtindo wa maisha yao (*lifestyle*) ili waweze kuishi kiafya zaidi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan alizindua mradi unaotekelezwa na Wizara ya Afya wa kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye mazoezi na kuishi maisha ya kiafya zaidi na kuondokana na mtindo wa *sedentary lifestyle* (maisha ya kuishi kwa kujiachia) zaidi. Lengo lilikuwa ni hilo, kuhamasisha zaidi kinga kuliko tiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama sasa kama itajitokeza mmoja wetu bahati mbaya akapata ugonjwa usioambukiza, maana yake tuna mkakati ndani ya Serikali wa kuhamasisha sasa watu wote wawe na Bima ya Afya ili ule mzigo wa gharama usiwe mkubwa sana kwake peke yake, uweze kubebwa na jamii yote kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq kwa Wizara hii hii ya Afya.

Na. 33

### **Kuwaasili Watoto Waliotelekezwa**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Wako watoto wengi wametelekezwa na wazazi wao na kuachwa wakizagaa mitaani.

Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kuihamasisha jamii kuwaasili watoto hao ili nao wafaidike na malezi ya jamii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Waziri wa Maliasili na Utalii, tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matunzo, malezi na ulinzi wa mtoto ni haki ya mtoto kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, kifungu cha 8 na cha 9 cha sheria hiyo kinatoa majukumu kwa mzazi ama mlezi na mtu yeyote mwenye jukumu la kumlea mtoto kuhakikisha anawatunza

na kuwalea watoto wake ipasavyo, ikiwemo kuwapatia huduma za msingi kama chakula, malazi, mavazi, elimu na kuwalinda dhidi ya vitendo vya unyanyasaji, ukatili, unyonyaji na utelekezaji. Aidha, kifungu cha 14 cha Sheria ya Mtoto kinatoa adhabu kwa mzazi ama mlezi yeyote atakayekiuka kifungu hiki kutozwa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Utafiti wa Watoto Wanaoishi na Kufanya Kazi Mitaani ya mwaka 2018 jumla ya watoto 6,393 wakiume wakiwa 4,865 na wakike wakiwa 1,528 walitambuliwa katika Mikoa sita ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya, Iringa, Dodoma, Arusha na Mwanza. Aidha, hadi kufikia Juni, 2018 jumla ya watoto 1,745 wamepatiwa huduma mbalimbali kama vile kuunganishwa na familia zao, kurudishwa shuleni, kupatiwa stadi za maisha, kuanzisha vikundi vya ujasiriamali na kuwatafutia malezi mbadala ya kifamilia. Lengo la Serikali ni kuhakikisha watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani wanaunganishwa na familia ili wapate huduma zote za msingi ikiwemo haki ya kulelewa na kutunzwa katika familia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuasili watoto kupitia vyombo mbalimbali vya habari na kupitia Maadhimisho ya Kitaifa ya Siku ya Mtoto na Programu ya Ulinzi na Usalama. Juhudi hizi kwa ujumla wake zimewezeshwa jumla ya watoto 66, wakike wakiwa 29 na wakiume wakiwa 37 kupata huduma ya uasili kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2015/2016 mpaka 2017/2018. Serikali inashauri wananchi wenye nia ya kuasili mtoto au watoto wawasiliane na Maafisa Ustawi wa Jamii walio karibu nao ili kupewa utaratibu wa namna bora zaidi ya kuasili watoto hao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq nimekuona.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyoyatoa.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, pamoja na kuwa Serikali inaelekeza wananchi wanaotaka kuasili watoto waende katika Ofisi za Ustawi wa Jamii, lakini bado wananchi wengi hawana taarifa ya kuasili watoto. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwa na programu maalum ya kuiarifu jamii kuhusiana na kuasili watoto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwabaini watoto waliopo mtaani ambao wana umri wa kwenda shule ili waweze kupata haki ya kwenda shule, ikizingatiwa kwamba sasa hivi Serikali imetoa elimu bure? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO):** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, majibu yake yanapatikana kwenye jibu letu la msingi ambapo nimesema kuna programu maalum ya kutumia vyombo vya habari, lakini pia kutumia Maafisa Ustawi wa Jamii ya kuelimisha umma kuhusu utaratibu mzima wa kuasili watoto ili mtu ambaye ana nia ya kufanya hivyo aweze kuelewa kwamba utaratibu unaopaswa kufuatwa ni upi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu utaratibu tulionao ndani ya Serikali wa kuwakusanya watoto hawa na kuwarejesha mashuleni ili waweze kupata elimu ikizingitiwa kwamba sasa hivi Awamu ya Tano tunatoe elimu bure, programu hiyo ipo. Kwenye jibu la msingi nimesema kuna idadi kubwa ya watoto ambao tumeweza kuwarejesha aidha kwenye familia zao na pia kuhakikisha wanarejea shuleni.

Mheshimiwa Spika, programu hiyo huwa inaanza kwanza kwa kujenga mahusiano na watoto walioko mitaani ama wanaoishi katika mazingira magumu, kuzungumza nao na kuwachukua na kuwapeleka kwenye vituo mbalimbali vya Serikali ama vya watu binafsi ambavyo tunavitambua

ambapo wanapata malezi. Pale watakaa katika kipindi cha matazamio cha muda usiozidi miezi miwili au mitatu na mara nyingi ni ndani ya mwezi mmoja ambapo wataalam wa saikolojia watakuwa wakiongea na hawa watoto na kujenga nao mahusiano ya karibu mpaka pale ambapo wataonekana kuelewa na kuwa tayari kurudi kuwa *re-unified* na familia zao.

Mheshimiwa Spika, mchakato huo ukikamilika, Serikali hutoa fungu na kuwakabidhi Maafisa Ustawi wa Jamii na kusafiri na wale watoto mpaka kwenye maeneo ambayo ndugu zao wapo ama familia zao zipo na watoto wale hukabidhiwa kwa familia zao ama kwa ndugu zao baada ya mazungumzo ya kina kufanyika baina ya Afisa wa Ustawi wa Jamii wa Serikali na hao ndugu. Hivyo, utaratibu huo umekuwa ukiendelea kutumika na ndiyo ambao umesaidia sana kupunguza idadi ya watoto walioko mitaani, vinginevyo tungekuwa nao wengi sana. Utaratibu huo unafanya kazi vizuri sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Josephine Thabitha Chagula.

Na. 34

### **Ahadi ya Ujenzi Barabara ya Kahama-Busisi Kivukoni**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kahama kupitia Nyang'holongo, Bukwimba, Karumwa, Nyijundu, Busolwa, Ngoma hadi Busisi Kivukoni kwa kiwango cha lami.

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
**(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Thabitha Chagula, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kahama kupitia Nyang'holongo, Bukwimba, Nyijundu, Busolwa, Ngoma hadi Busisi Kivukoni ni barabara ya mkoa inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) katika Mkoa wa Mwanza, Geita na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu za Wizara yangu zinaonesha kuwa Mheshimiwa Rais aliahidi ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara inayoanzia Geita (Nyankumbu) hadi Kahama kupitia vijiji vya Nyang'hwale, Nyijundu, Karumwa, Bukwimba hadi Nyang'holongo kwa Mkoa wa Geita na kuendelea hadi Kahama Mkoani Shinyanga yenye urefu wa kilometa 149.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imeanza kuijenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo kwa awamu ambapo kilometa nne zimekamiliwa kujenga kuanzia Nyankumbu hadi Mkolani. Ujenzi wa kiwango cha lami utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kutokana na umuhimu wa barabara hiyo, *TANROADS* imeendelea kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi bilioni 1,771.751 zimetengwa kupitia Mkoa ya Geita na Shinyanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Chagula.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kuridhisha na ya kututia



moyo wananchi wa Mkoa wa Geita, lakini nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana na ni kiunganishi kati ya Mkoa wa Shinyanga na Geita, lakini pia itafungua uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Geita na Shinyanga wakati wa kuuza mazao yetu. Je, ni lini sasa ujenzi huu utakamilika? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo moja kutoka kwa Mheshimiwa Chagula. Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza zile pongezi alizozitoa nazipokea, lakini namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia maendeleo mbalimbali katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, ni lini? Niseme tu kwamba ule usanifu wa awali umeanza. Baada ya kukamilika usanifu na kupata michoro tutajua gharama za ujenzi wa barabara hii na pia muda ambao utatumika na baada ya kupata fedha tutaweza kujua kwamba ni lini barabara hii itakamilika. Niwashukuru wananchi na Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano waliotupa maeneo yote tuliyotembelea, tumeweza kupata michango mingi kuona kwamba wana utayari wa kupisha maeneo ili tuweze kujenga babaraba hii.

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Desderius Mipata.

Na. 35

### **Ahadi ya Barabara ya Chala Kutopita Katikati ya Mji**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Mwaka 2015 akiwa katika Kampeni, Mheshimiwa Rais aliwaahidi wananchi wa Mji Mdogo wa Chala kuwa barabara ya lami iliyokuwa inajengwa ingepita nje ya Mji huo na hakuna nyumba ambayo ingevunjwa, lakini katika

ujenzi barabara hiyo ilipita katikati ya Mji ilipokuwa inapita barabara ya vumbi na hivi karibuni Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Rukwa ametoa *notice* ya kuvunja nyumba za wananchi zilizowekwa alama ya 'X'.

(a) Je, kwa nini Serikali inatoa kauli mbili tofauti kwa wananchi?

(b) Je, Meneja wa *TANROADS* kutotekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais inatafsiri gani kwa wananchi wa Chala ambao Mheshimiwa Rais aliahidi nyumba zao kutovunjwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wananchi wa Nkasi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifautavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sumbawanga - Mpanda inayopita katika Mji mdogo wa Chala ni barabara iliyokuwepo tangu enzi za Ukoloni ilipotungwa Sheria ya Barabara (*The Highway Ordinance*) ya mwaka 1932. Sheria ya Barabara ilifanyiwa marekebisho tena mwaka 1967 ambapo hifadhi ya barabara ilikuwa mita 22.5 kila upande. Aidha, mwaka 2007 ilitungwa Sheria ya Barabara Na.13 ambapo upana wa barabara uliongezeka kutoka mita 22.5 na kuwa mita 30 kutoka katikati ya barabara kila upande kwa barabara kuu na za mikoa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 Mheshimiwa Rais alitoa agizo kuwa hakuna mwananchi wa Chala atakayebomolewa nyumba yake bila kulipwa fidia kwa mujibu wa sheria. Katika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais na matakwa ya sheria, Wakala wa Barabara Tanzania

(TANROADS) imeweka alama ya 'X' nyekundu kwa nyumba zilizo ndani ya mita 22.5 na alama 'X' ya kijani kwa nyumba zilizo kati ya mita 22.5 na mita 30 kutoka katikati ya kila upande kwa ajili ya kuweka kumbukumbu. Hata hivyo, nyumba zilizo katika Mji Mdogo wa Chala hazitabomolewa kwa sasa kufuatia kukamilika kwa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Sumbawanga - Kanazi mpaka maeneo hayo yatakapohitajika kwa ajili ya upanuzi wa barabara katika miaka ijayo. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na vilevile nashukuru sana kwa majibu mazuri sana ya Serikali ambayo kwa vyovyote vile watakuwa wameridhika sana wananchi wa Mji wa Chala. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika ujenzi wa barabara hii ya kutoka Sumbawanga kwenda Kanazi, wajenzi walichimba mashimo mbalimbali katika Vijiji vya Kasu na Kipande ambayo hata baada ya kukamilisha ujenzi bado hayajafukiwa na hata waliposhauriwa hatujaona kama yamefukiwa.

Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba wajenzi hawa wanayafukia mashimo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kufuatia mvua nyingi zilizonyesha Mkoani Rukwa na Tanzania kwa ujumla, zimeathiri miundombinu ya barabara nyingi nchini, lakini barabara mbili za Jimbo la Nkasi Kusini zimeathirika sana na haziwezi kupitika wakati wa mvua kama mvua zitaanza hivi karibuni. Barabara hizo ni Milundikwa - Kisura - *Malongwe Junctions* yenye kilometa 15 na barabara ya Kitosi - Wampembe yenye kilometa 67 hasa maeneo ya milimani. Naomba Serikali ifanye juhudi ya kuhakikisha kwamba maeneo haya yanashughulikiwa mapema iwezekanavyo. Je, Serikali iko tayari kuitikia wito wangu wa kwenda kutekeleza mara moja inavyowezekana?

**SPIKA:** Ahsante sana. Tatizo la maswali yako yote mawili hayaendani na swali la msingi na hili nalisitiza sana Waheshimiwa Wabunge. Swali lako ni barabara isipite katikati ya Mji Mdogo wa Chala, ipite nje ya Mji Mdogo, kitu ambacho barabara inapopita nje Mji Mdogo ina *re-organize*, ina-*disturb*, *center* ya Mji inabidi tena ihamie barabara iliko. Kwa sababu ndiyo mapendekezo yenu, Mheshimiwa Rais aliwakubalia na Mheshimiwa Waziri amewakubalia, sasa hayo mengine hayako hapa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, swali la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande.

Na. 36

### **Uhaba wa Mkubwa wa Maji-Mkoa wa Lindi**

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE** aliuliza:-

Wananchi wa Mkoa wa Lindi wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa muda mrefu hadi kusababisha baadhi ya wananchi hasa wa vijijini kutumia maji ya mito na mabwawa pamoja na mifugo.

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi mbalimbali ya maji Mkoani Lindi?

(b) Je, ni lini Serikali itahakikisha upatikanaji wa maji safi katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi ili kuepusha uwezekano wa magonjwa ya mlipuko kwa wauguzi na wagonjwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya maji, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Chande,

Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji katika Mkoa wa Lindi, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika maeneo ya mijini na vijijini ya Mkoa huo kupitia Awamu ya Pili ya programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Hadi kufikia mwezi Oktoba, 2018 miradi ya maji katika vijiji 48 ilikuwa imekamilika, miradi katika vijiji vingine 21 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa lengo la kuboresha huduma ya maji Lindi Mjini na vijiji vya pembezoni, Serikali inaendelea na ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Ng'apa ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 92 na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2019.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukarabati mifumo ya maji ya Hospitali ya Mkoa wa Lindi pamoja na kuagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Lindi kutoa kipaumbele kwa Hospitali hiyo wakati wa ugawaji maji. Aidha, mradi mkubwa wa maji wa Ng'apa utakapokamilika utaboresha pia huduma ya majisafi katika Hospitali hiyo ya Mkoa wa Lindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lathifah.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Mradi wa Ng'apa, naona anatuchanganya kidogo kwa sababu katika majibu aliyotoa wakati wa Bunge la Bajeti tulipewa taarifa na Serikali kwamba Mradi wa Ng'apa ulikuwa umekamilika, leo hii tunaambia kwamba huu mradi utakamilika mwakani.

Mheshimiwa Spika, takribani shilingi bilioni 2.6 zilitengwa na Serikali kwa ajili ya miundombinu ya usambazaji wa maji, lakini mara kwa mara mabomba ya maji ambayo yanatakiwa kusambaza maji katika Manispaa ya Lindi yamekuwa yakipasuka kupelekea wananchi wa Lindi kukosa

maji mara kwa mara. Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Lindi wanapata maji bila usumbufu wowote na kwa uhakika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya maji imegubikwa na ufasidi uliokithiri kupelekea miradi mingi kutokamilika na hata ikamilika inakuwa chini ya kiwango yaani *there is no value for money*. Kuna wakati Kamati ya PAC iliwahi kuitaka Serikali iwachukulie hatua watendaji walioisababishia hasara ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya miradi nane ya maji hapa nchini.

**SPIKA:** Sasa swali Mheshimiwa Lathifah.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni hili, kwa kuwa mara kwa mara tumekuwa tukiomba Tume Maalumu iundwe kwa ajili ya kufanya uchunguzi, Serikali imechukua hatua gani katika kuhakikisha ubadhirifu huu unakomeshwa mara moja? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Jumaa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, moja, Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha tunawapatia wananchi maji. Serikali kwa jitihada kubwa imewekeza mradi pale Lindi Mjini zaidi ya *Euro* milioni 11.7 katika kuhakikisha tunaongeza uzalishaji kutoka lita milioni 1.5 mpaka lita milioni tisa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Naibu Waziri wa Maji nilifika katika mradi ule wa Ng'apa, tukamwona mkandarasi wa utekelezaji wa mradi ule anasuasua, amefikia asilimia 92. Kwa kuwa sisi azma yetu ni kuhakikisha tunamtua mama ndoo kichwani, tumemtoa mkandarasi yule na jukumu lile tumewapa wakandarasi wetu wa Wizara watekeleze mradi ule ndani ya mwezi Februari, 2019 uweze kukamilika na wananchi waweze kupata maji saji, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la ubadhirifu wa miradi ya maji, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, nasi kama viongozi wa Wizara tumeendelea kuchukua hatua mbalimbali na Serikali imeunda Tume ambayo imepita maeneo mbalimbali ambapo hata Waheshimiwa Wabunge mlishirikishwa katika kuhakikisha mnatoa maoni yenu. Msimamo wetu kama Wizara, tutaendelea kuchukua hatua, kwa yeyote atakayekula fedha za miradi ya maji lazima azitapike mchana kweupe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mbunge wa Mbulu, Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la msingi la Mheshimiwa Lathifah linafanana kabisa na hali iliyoko Mbulu Vijijini. Kwa kuwa miradi ya maji haijakamika na iko minne na Mheshimiwa Naibu Waziri anaifahamu. Je, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu atanisadia ili miradi ile ikamilike? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, anafanya kazi nzuri sana katika Jimbo lake la Mbulu, na mimi nimeweza kufika katika Jimbo lake nimeona hali ya upatikanaji wa maji. Kubwa nililojionea, tuna miradi mingi lakini ni kiporo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kiongozi wa Wizara ya Maji, nimeomba wataalam wa Mbulu waje Wizarani tuweze kukaa na timu yetu katika kuhakikisha tunawaongezea nguvu ili miradi yake iweze kukamilika na azma ya Mheshimiwa Rais ya kumtua mama ndoo kichwani iweze kutimilika.

**SPIKA:** Tunaendelea. Bado tuko na Wizara ya Maji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Maswa Magharibi, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

Na. 37

### **Mpango wa Kuvipatia Vijiji Maji Kutoka Bwawa la Zanzui**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Vijiji vya Zanzui, Malita, Mwabujiku, Dodoma, Buyubi na Ikungulyasubi kwa muda mrefu viko kwenye mpango wa kupatiwa maji kutoka kwenye Bwawa la Zanzui linalotoa maji kwa Mji wa Maswa.

Je, ni lini mpango huo utakamilishwa na Serikali ili wananchi katika vijiji hivyo wapate maji ya uhakika?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi kitaifa wa Maswa unahudumia Mji wa Maswa pamoja na vijiji 11 vinavyopatikana katika Wilaya ya Maswa. Katika mradi huo Vijiji vya Zanzui, Matila, Mwabujiku, Dodoma na Buyubi vimeshaunganishwa na mradi huo na vinapata huduma ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Maswa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imepanga kufanya upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa maji wenye urefu wa kilometa 55 wa



mradi wa Kitaifa wa Maswa ambapo Kijiji cha Ikungulyasubi kitaunganishwa katika mtandao na kupata maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaki, swali tafadhali.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, mradi huu unaozungumziwa wa vijiji 11 bado haujakamilika. Namwomba tu Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya kumaliza Bunge lako hili tukufu akubali tuambatane pamoja tuangalie hali halisi ya mradi huu halafu tuweze kufanya uamuzi kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, mradi huu wa maji wa Maswa unahudumiwa na bwawa la Zanzui ambapo kuna mradi wa kujenga chujio, lakini kwa muda sasa wa wiki mbili au tatu maji hayatoki kwenye Mji wa Maswa kwa sababu bili ya umeme imekuwa kubwa na *TANESCO* wamekata umeme na bili hii inalipwa na Wizara ya Maji.

Je, Wizara ya Maji inalipa lini bili hii ya umeme kwa *TANESCO* ili wananchi wa Wilaya ya Maswa na vijiji vyake waweze kuendelea kupata maji? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi katika kuwatetea waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba nipo tayari kwa sababu baada ya Bunge tunaanza ziara katika Mkoa wa Kagera. Kwa hiyo, kabla sijapita Kagera nitapita katika Jimbo lake kuangalia hali ya

upatikanaji wa maji ili tuweze kutafuta ufumbuzi utakaowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili la kukatiwa umeme, leo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wakurugenzi wote tumewaita Dodoma, tulikuwa na kikao nao jana na leo, nitamwita Mkurugenzi wa Maswa katika kuona namna gani tunaweza kutekeleza suala hili ili wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, kikubwa nataka niwaambie Wakurugenzi wote wa miradi ya maji, Serikali inawezeza fedha nyingi katika kuhakikisha wananchi wanapata maji. Waswahili wanasema, ukibebwa nawe kiuno kaza. Haiwezekani Serikali iweke mradi lakini wewe kwa vile unafanya biashara, unakusanya lakini huwezi kulipia bili za umeme Serikali ikulipie.

Kwa kuwa wewe ni Mkurugenzi, umewekewa mradi wa maji ni lazima ukusanye fedha katika kuhakikisha unalipia dawa na umeme ili waweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi/ Kicheko)*

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Khatib kiswahili hicho Pemba hakijafika bado. Ukibebwa kaza kiuno. *(Kicheko/ Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo Maswa linafanana kabisa na tatizo lililopo Jimbo la Ikungi Magharibi. Kwa kuwa vijiji vya Misake, Utao B, Utao A, Igliansoni, Isalanda, Masweya, Mduguyu, Mpugizi, Msosa, Mkenene na Mwaru havina kabisa huduma ya maji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vijiji hivyo maji ili kumtua ndoo mwanamke? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Aisharose Matembe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza sana dada yangu Mheshimiwa Aisharose, kwanza ni mwanamke jasiri na shupavu ambaye amekuwa akiwapigania sana wananchi wa Singida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mpango wa Serikali, mpango wetu kama Wizara ya Maji ni katika kuhakikisha tunajenga miradi zaidi ya 2,052 ambayo itakuwa na vituo vya kuchotea maji zaidi ya 38,549 ambapo itahudumia wakazi zaidi ya elfu kumi na tisa na themanini elfu. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie, katika vijiji 2,052, katika utekelezaji naye tutamwalia katika mkoa wake wa Singida katika kuhakikisha akina mama wa pale wanapata maji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimekuona Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi huu unaenda sambamba na ule mradi wa Lindi. Mradi wa Lindi ulikuwa umalizike mwaka 2015/2016, ukaja mwaka 2016/2017, ukaja mwaka 2017/2018 na sasa hivi tuko mwaka 2018/2019. Hata Mheshimiwa Rais alipofika alitoa angalizo na tukaambiwa utaisha mwezi Julai, 2017.

Leo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba ule mradi bado haujakamilika mpaka mwezi Februari. Watu wa Lindi wanapata shida sana ya maji, maji ni tatizo kubwa la wananchi wa Mkoa wa Lindi. Sasa atuhakikishie, mwezi wa Julai umepita, sasa hivi tunaambiwa mwezi wa Februari na wenyewe utapita, tunaomba kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, watu wa Ng'apa pale pale ambapo ndiyo kuna chanzo cha maji, hawana maji. Serikali inatuambia nini juu ya jambo hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya shida hiyo kubwa sana kule Ng'apa na Mjini Lindi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Jumaa Aweso tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Mbunge, mama yangu, waswahili wanasema, ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Mimi kama kiongozi wa Wizara hii nilishafika pale Lindi na nimeona hali ya upatikanaji wa maji katika Mkoa wa Lindi ni changamoto ingawa Serikali imewekeza mradi mkubwa zaidi ya *Euro* milioni 11.7.

Changamoto kubwa ya miradi yetu ni suala la upatikanaji wa wakandarasi na mkandarasi yule tumemwona akisuasua na ujanja umekuwa mwingi sana. Sisi kama viongozi tumechukua hatua ya kumwondoa na tumewaagiza wataalam wetu wa Wizara waifanye kazi ile.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie mama yangu, amenikumbusha siku ambayo nimeapishwa na Mheshimiwa Rais, alituambia anatupa Wizara ya Maji wananchi wapate maji, wasipopata maji tutatumbuliwa, mimi sipo tayari kutumbuliwa. Tutahakikisha ndani ya muda tuliouweka mradi ule unakamilika katika kuhakikisha wananchi wa Lindi wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Wananchi wa Lindi muendeele kuwa na subira kidogo.

Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda. Mheshimiwa Sophia uliza swali lako.

Na. 38

**Upanuzi wa Mradi wa Maji Rujewa**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Mradi wa maji ya bomba katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa, Wilayani Mbarali ni wa zamani, hivyo haukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa.

(a) Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kupanua mradi huu?

(b) Chujio la maji katika eneo la Mtaa wa Igomelo kwa sasa halitumiki kwa kuwa liko chini ya kiwango. Je, Serikali imechukua hatua gani kwa wahandisi waliotoa michoro na kusababisha hasara ya fedha za Serikali na wananchi wakiendelea kupata shida ya maji katika Mji Mdogo wa Rujewa na hasa maeneo ya Igawa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Jumaa Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) na kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa chujio la kuchuja tope (*slow sand filter*) ulianza kujengwa mwaka 2007 na kukamilika mwaka 2009. Chujio hilo hupokea maji kutoka chanzo cha maji ambacho kipo kwenye Pori la Akiba Kipengele. Mnamo mwaka 2009 hadi 2013 matumizi ya chujio hilo yalisimama kutokana na zuio kutoka Ofisi za Pori la Kipengele wakihitaji Taarifa ya Tathmini ya Athari za Kimazingira. Zuio hilo liliathiri ufanyaji kazi wa chujio licha ya kujengwa katika ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza matakwa ya Ofisi ya Pori, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ilifanya Tathmini ya Athari za Kimazingira mnamo mwaka 2012 na kupewa Cheti cha Tathmini (*Environment Impact Assessment*) Namba EC/EIS/643 cha tarehe 17 Desemba, 2012.

Baada ya kukamilisha vigezo hivyo, Serikali imeanza ukarabati wa miundombinu ya chujio hilo na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2018 na hivyo kuanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi kama ilivyotarajiwa. Serikali itafuatilia utekelezaji wa mradi huo na endapo itabainika kuna ubadhirifu, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, katika kumaliza tatizo la maji kwa Mji wa Rujewa na vitongoji vyake, Serikali kupitia fedha za mkopo kutoka Serikali ya India, imepanga kutekeleza miradi katika Miji mbalimbali ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar ukiwemo Mji wa Rujewa. Kwa sasa taratibu za kupata wataalam washauri watakaofanya usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha wa zabuni zinaendelea. Ujenzi wa miradi hiyo unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwaka huu wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kutokana na swali langu la kwanza, swali langu la msingi ni kwamba wananchi wa Rujewa wanalalamika kuhusu mradi ule kutumia pesa nyingi na kutokukamilika. Jibu lake la msingi la Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba kulikuwa na makosa ya kutokufanya tathmini ya mazingira. Je, Serikali itachukua hatua gani kwa wakandarasi pamoja na Mkurugenzi kwa kuanza mradi mahali ambapo hapajafanyiwa utafiti yakinifu wa mazingira?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kwenda kuangalia huo mradi wanaosema unaisha mwezi Disemba, chujio ni kubwa, bomba wanalo-*connect* ni dogo. Naomba Mheshimiwa Waziri twende pamoja tukaangalie ule mradi kwa maana umekwenda kinyume na utaratibu ulivyotakiuwa kufanywa. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia kwenda pamoja mpaka mumuombe kibali Spika. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, lakini kubwa kuona ni kuamini, niko tayari kwenda Mbarali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la utekelezaji wa miradi hii ya maji, nataka niwaambie wataalam wa maji katika Wizara yetu ya Maji na Halmashauri zote, wanapotaka kutekeleza miradi ya maji lazima wahusishe sekta nyingine. Haiwezekani Serikali itake kuwekeza fedha kwa muda uliopangwa kunakuwa na uchelewesaji kwa sababu tu ya taratibu nyingine hazikufuatwa. Nawaomba sana washirikishe sekta nyingine ili mradi uweze kutekelezwa kwa muda uliopangwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho kabisa la nyongeza kwa siku ya leo litaulizwa na Mbunge mpya kutoka Korogwe Vijijini, Mbunge wa Chama cha Mapiunduzi, Mheshimiwa Timotheo Mnzava, tafadhali.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji kwenye Mji Mdogo huu wa Rujewa linafanana kabisa na tatizo la maji kwenye Mji Mdogo wa Mombo ambapo miundombinu yake ni ya muda mrefu, Mji umekua na watu wameongezeka sana. Katika Mji wa Mombo kuna mradi mkubwa wa maji ambao ulibuniwa kuchukua maji kutoka eneo la Vuga ambao umekuwa ukisuasua, mabomba yalishawekwa kwenye baadhi ya maeneo lakini hatua inayoendelea mpaka sasa hivi. Mheshimiwa Naibu Waziri anawaambia nini wananchi wa Korogwe Vijijini hususan watu wa Mombo kuhusu mradi huu wa maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mnaona Wabunge wa CCM hao? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwa mara yake ya kwanza lakini amepata ujasiri wa kuweza kuwatetea wananchi wake. Nataka niwapongeze wananchi wa Korogwe kwa kufanya kazi nzuri sana, wewe ni dogo lakini ni mkombozi katika kuhakikisha tunakwenda kutatua tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mombo pamoja na wa Korogwe Vijijini, sisi kama Wizara ya Maji tunausimamia mradi ule ili ukamilike kama ulivyopangwa ili wananchi wa Mombo waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mkiangalia muda wetu uko pale pale tunapotakiwa tuishie.

Sasa ni matangazo ya wageni ambao tunao katika ukumbi wetu wa Bunge kwa siku ya leo. Nimearifiwa kwamba tunaye kwenye *Gallery* ya Spika, Balozi wa nchi ya Kuwait hapa nchini Tanzania, Mheshimiwa Mubarak Mohammed Al-Shajan. Karibu sana Mheshimiwa Balozi na amefuatana na Maafisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje, Ndugu Ayoub Mndeme na Ndugu Odilo Fidelis. Ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na mgeni wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza ambaye ni rafiki yake kutoka Muleba kule Kagera, Ndugu Christopher Kilaja, Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM ya Mkoa wa Kagera. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni rafiki zake kutoka Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Diwani wa Mbarali, Mheshimiwa Dira Funika. Mheshimiwa Diwani karibu sana na umesikia swali lako likulizwa hapa kuhusu maji Mbarali. *(Makofi)*



Mgeni wa Mheshimiwa Cecil Mwambe ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Lindi, Ndugu Mathew Lupogo. Ahsante. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ambaye ni dada yake kutoka Chamwino hapa Dodoma, Ndugu Zuwena Aweda. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Longido, Ndugu Frank Mwaisumbe. Ahsante sana labda atakuja baadae kidogo. *(Makofi)*

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawaletae mgeni maalum kabisa. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, nawaletae mgeni maalum kabisa naye ni mke wa Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, Ndugu Axavery Mwakasaka. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Shemeji yangu bado hatujakuona vizuri, kuna upande mmoja hawajakuona hivi, naomba usimame tena kwa mara nyingine. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Hawa wamefunga harusi majuzi kabisa, kwa hiyo, bado wako kwenye *honeymoon*. Wanyamwezi bwana wanajua kuchangua kumbe. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, mali ya Geita hiyo.

**SPIKA:** Yuko na shemeji yake Ndugu Herieth, karibu sana. Hongera sana Mheshimiwa Mwakasaka kwa kupata jiko. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea, Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, hoja ya jambo la dharura.

**SPIKA:** Sijakuona.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, niko hapa.

**SPIKA:** *Okay.* Mheshimiwa Makamba peke yako, haya, nakuruhusu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 47 kukuomba Kiti chako kiweze kuahirisha mjadala uliopo ili tuweze kujadili jambo la dharura kuhusu hali ya kidiplomasia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kinachoendelea nchini sasa hivi kuhusiana na Ubalozzi wa *EU*, lakini pia tunafahamu umuhimu wa mataifa yanayoingia kwenye Ubalozzi wa *EU*, mataifa 27/28 na tunafahamu mchango wao kwenye bajeti yetu, tunafahamu mchango wao katika uchumi wetu. Lakini kumetokea tatizo tangu wiki iliyopita na leo ni siku ya nne tangu tumeanza Bunge hatujasikia kauli yoyote thabiti ya Serikali ambayo ingeweza kwenda kutoa msimamo wa nchi yetu juu ya hali ya kidiplomasia kati yetu na Umoja wa Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hiyo kwa umuhimu wake, mahusiano ya kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine yanatakiwa kuchukuliwa kwa uzito na ndiyo maana nimeomba busara ya Kiti chako, tuweze kujadili juu ya habari iliyotokea jana kuhusu wavuvi 36 kule Kenya, lakini pia hali tete ya kidiplomasia inaendelea kutetereka ndani ya nchi yetu kwa habari ambayo tumeipata leo kwa Kamati inayotetea Waandishi wa Habari, watu wawili wameshikiliwa

na Serikali yetu ya Tanzania, kuna Bi. Angela Quintal na Bi. Muthoki Mumo, wameshikiliwa, wamenyimwa hati zao za kusafiria kwa sababu ambazo Serikali inafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa jambo hili, naomba busara ya Kiti chako na niwaombe Wabunge wenzangu waniunge mkono tujadili hali ya kidiplomasia katika nchi yetu. Pia tuionbe Serikali itoe kauli thabiti kwa wadau wetu hawa wakubwa ambao wanachangia kwa kiasi kikubwa pato la nchi yetu na bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba busara ya Kiti chako tulijadili na tuombe Serikali iweze kutoa kauli juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Hana hoja huyo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome.

Kwanza kuna mambo matatu uliyoyaleta, suala la wavuvi 36 huko Kenya sijui limefanyaje hilo.

Pili, kuna Wakenya wawili ambao wameshikiliwa hapa nchini, kwa majina yao kama vile ni Wakenya, kama siyo Wakenya basi *I am sorry*, lakini kwa majina yale ni kama ya nchi jirani, hilo ni suala la pili.

Ia tatu ndiyo hilo la *EU*. Wewe mwenyewe hukujipanga, lakini kubwa zaidi hukuungwa mkono na mtu yeyote. Kwa hiyo, pole sana. Hakuna aliyekuunga mkono.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, tunaendelea, Katibu.

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**KAMATI YA MIPANGO**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa  
Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali Pamoja na  
Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na uchangiaji na ninao wachangiaji wengi wa kutosha, ambacho ningewaomba tangu mapema, tujitahidi zaidi kumshauri Mheshimiwa Waziri kuhusu mipango ya nchi tunakotoka na tunakokwenda badala ya zile barabara za vitongoji vyetu na mambo kama hayo. Pia tuwe makini kwenye lugha zetu ili taarifa, taarifa zisiwepo, mjadala uwe na afya, uwe mzuri.

Haya tunaanza na orodha yote ya vyama vyote ninayo hapa na niwahakikishie mtapata nafasi kama hatutakuwa na vipindi vya kupoteza muda. Tunaanza na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Adadi Rajab halafu tutaendelea na upande mwingine. Mheshimiwa Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua. Naona Serikali yetu imejipanga vizuri, imechagua vipaumbele ambavyo vitasukuma gurudumu la maendeleo la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ukurasa wa 31 namba (xi), kwa ruhusa yako, naomba nisome anasema;

"Aidha shughuli za kiuchumi pia zimeongezeka; vilevile, ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji Mto Rufiji - MW 2100." Hili ni jambo hili ni zuri sana kwa sababu nishati ndiyo dereva mkubwa wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi sana vya nishati, naomba aangalie huko. Ukichukua chanzo cha joto ardhi katika *Rift Valley*, Kenya ina *potential* ya kuwa na MW 1000 mpaka 1500, Tanzania tuna *potential* ya kuwa na MW 5000 kwa joto ardhi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri badala ya kuangalia tu kwenye maji na sehemu nyingine, aangalie kwenye joto ardhi ili tuweze kuwa na nishati ya kutosha kuweza kuendesha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, ukurasa wa 42 ameandika pale kwa ruhusa yako nasoma; "Kuhakikisha thamani halisi ya fedha inazingatiwa katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi kwa kuzingatia misingi ya Kanuni za Ununuzi wa Umma kama *Force Account*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo pana mgogoro. Inaonekana kwenye *unit* ya uzalishaji tuna kawaida ya kumuangalia Mhasibu, Mkaguzi wa Hesabu (*Auditor*) na *General Manager*, hatumwangelii mnunuzi na hapa ndiyo kuna hasara kubwa sana. Hatumwangelii mnunuzi kwa kumpa mafunzo ya kutosha na hatumwangelii kwa makini hasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, sasa hivi Serikali imeamua kutoa fedha za kujenga Vituo vya Afya, Serikali ikatumia ujanja mzuri sana wakawaambia Halmashauri fungueni *account* tofauti, twende kwenye manunuzi tofauti, wakafungua *Force Account*, fedha imetumika vizuri sana, ina maana kuna tatizo kwenye ununuzi. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali angalieni kada (*profession*) ya ununuzi muifundishe na kuiangalia vizuri ili tusipoteze fedha za umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye ukurasa wa 46 kuhusu ujenzi wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji, kwa mfano, reli na nishati. Wazo la kujenga *Standard Gauge Railway* ni zuri sana, litasaidia kwenye bandari yetu na biashara na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwenye kitabu hiki, Mheshimiwa Waziri amesema reli hii inatoka Dar es Salaam kwenda Tabora, Tabora kwenda Mwanza, Tabora kwenda Kigoma na Isaka kwenda Rwanda. Naona Mheshimiwa Waziri amesahau ya Uvinza kwenda Msongati. Naomba tuiangalie sana reli hiyo, kwa sababu nchini Burundi kuna madini mengi sana, kuna *nicol, platinum* ambapo reli hiyo italeti biashara kubwa sana Tanzania. Kwa hiyo, naomba kama Burundi haina fedha, basi Serikali i-*invite* Burundi, m-*negotiate* naye ili reli hii ya kutoka Uvinza kwenda Msongati na kwenda Bujumbura ijengwe sambamba na hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika ujenzi wa reli kwa kuitumia bandari yetu ya Dar es Salaam, reli ya *TAZARA* tuisahau, haihitaji kujengwa upya, inahitaji kuboreshwa tu ili sasa tuitumie vizuri bandari yetu ya Dar es Salaam. Tunapoiboresha reli ya *TAZARA* kwa kuipa umeme na kadhalika, tuangalie bandari kavu ya Inyala pale Mkoani Mbeya ili kutoka pale sasa tuiite Malawi tujenge pamoja reli ya kutoka Inyala kwenda Ziwa Nyasa kwenda Malawi kufanya biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mwenzangu wa Mbeya Vijijini jana alisema nchi za Msumbiji, Namibia na Angola zinaboresha bandari zao kwa kuziangalia nchi ambazo ziko *land locked* za Zambia, Congo na Zimbabwe na sisi tunaangalia huko huko.

Kwa hiyo, naomba tunapojenga reli ya *Standard Gauge* tuboreshe reli ya *TAZARA* ili tuwe na reli tatu. Tutakuwa na bahati kuwa na aina tatu ya reli, tuna *Standard Gauge, Metre Gauge* na *Cape Gauge*. Kwa hiyo, mzungo wowote ule tunaweza kuumudu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, tunaponunua *engine* na mabehewa ya *Standard Gauge*, tununue mabehewa na *engine* ambazo ni *adjustable* ambazo zinaweza zikatumika kwenye reli ya *Standard Gauge* na kwenye reli ya *Metre Gauge* ya TAZARA.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambalaswa, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, mnamwona Mbunge anayechangia Mpango? Anachangia mambo ya kitaifa. Sasa ni *Senator* huyu, huo ndiyo mfano, atakayekuja na habari ya vitongoji namkata hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwambalaswa endelea. (*Makofi*)

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa *compliment* hiyo. *You have made my day* na leo ni *birthday* yangu, nina miaka 66, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoiboresha reli ya TAZARA na Reli ya Kati, naomba tuangalie vilevile uwanja wa ndege wa Songwe. Nimeona kuna sehemu nyingi kuna viwanja vya ndege, tuangalie uwanja wa ndege wa Songwe ambao uko kimkakati sana kwa nchi za Kusini na Mikoa yote ya Kusini. Uwanja ule umekamilika, ni mzuri, lakini bado tu uzio, taa za kuongezea ndege, kumalizia na jengo la abiria. Naomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwanja huu tuukamilishe ili uweze kuleta *value for money* kwa biashara za Mikoa ya Kusini na nchi za jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mtandao mkubwa wa barabara ambao uko kwenye kitabu hiki. Naomba tunapojenga barabara hizi ambazo ni *driver* kwa uchumi wetu, tuiangalie sana barabara ya mchepuko ya kutoka Inyala kwenda kuingia kwenye barabara Kuu ya Tanzania - Zambia pale Mbalizi. Sasa hivi kwa barabara hii inapopita Mkoani Mbeya kuna *congestion* kubwa sana, kwa

hiyo, kuna kupoteza muda mrefu sana. Naomba tuiangalie barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini nakushukuru sana kwa kunipa *compliment* ambayo *you have made my day*, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa kweli imekuwa ni vizuri umekuwa mchangiaji wetu wa kwanza, maana umeweka msingi.

Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab nilikutaja na upande huu mwingine tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Sware dakika tano. Mheshimiwa Adadi Rajab.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi hii kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kusifu sana juhudi ambazo Serikali ya Awamu ya Tano imezifanya katika kipindi cha miaka mitatu. Imefanya mambo mengi ambayo yatakuwa ni historia. Napenda sana kusifu hasa miradi mikubwa ambayo imeanzishwa na ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa mwaka 2017, kuna mambo mengi ambayo ni ya msingi ambayo yameachwa hayakuorodheshwa kwenye Mpango wa mwaka huu na mapendekezo hayo Kamati ya Bajeti imeorodhesha vizuri sana katika *page* namba 13. Pamoja na mapendekezo hayo, napenda kujikita zaidi kwenye mambo mawili ambayo naona ni ya msingi sana na napenda kujua kwa nini yameachwa kwenye mapendekezo ya mpango wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni barabara ya *Chalinze Express Way*. Barabara hii naona imeachwa na sijui



kwa nini imeachwa. Cha msingi tunaona ni muhimu kwenye mapendekezo haya barabara hii ikaingizwa kwa sababu mapato mengi sana yanategemewa kwenye mambo ya *road toll*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikizungumza suala la *road toll* tangu mwaka 2017 lakini naona bado Mheshimiwa Waziri hajaona umuhimu wake, lakini *road toll* ni muhimu sana kwa sababu Mataifa mengi duniani sasa hivi unapoenda unakuta kwamba kuna mageti ambayo yanakusanya mapato na mapato yanaweza kupatikana kwa urahisi zaidi. Najua inawezekana sababu mojawapo ni uanzishwaji wa *SGR*, lakini *SGR* ni kitu kingine na mambo ya barabara ni kitu kingine kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la Bandari ya Bagamoyo. Bandari ya Bagamoyo imeachwa kabisa na sijui ni kwa nini imeachwa. Bandari hii imeshughulikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Nakumbuka mpaka *MoUs* ambazo tumewahi kuzisaini kati ya Serikali yetu na Serikali ya Oman pamoja na Serikali ya China tulifanya sherehe kubwa sana kule kwenye Ubalozzi wetu Oman kusherehekea mradi huu, lakini sasa hivi naona kama mradi huu haupewi umuhimu ambao unatakiwa. Nashauri kwamba mradi huu na wenyewe uweze kuingizwa kwenye mapendekezo ya mipango ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kiwanda pia cha kuchakachua au kusafisha madini sijaona mpango huo kwenye Mapendekezo ya Mpango huu ya Mheshimiwa Waziri. Ningefurahi sana kama na suala hilo pia lingeweza kuingizwa kwenye mpango huu wa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uchimbaji wa gesi asilia. Suala hili naona pia limesahauliwa na sijui ni kwa nini, lakini utakumbuka kwamba gesi yetu asilia tulikuwa na wawekezaji wengi sana kule Mtwara na Lindi, lakini wawekezaji wale wameondoka na sasa hivi wamehamia kwenye nchi jirani tu pale, lakini suala hili halijapewa umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikisoma kwenye mitandao taarifa fulani nikaona kwamba wawekezaji ambao walikuwa wawekeze kule, moja ni Kampuni ya *Shell* sasa hivi imeenda kuwekeza kule na imejenga mitambo ile ya *LNG* Canada kule British Columbia kwa gharama kubwa sana. Sasa tunaona tunampoteza mwekezaji mkubwa kama yule na ilikadiriwa kwamba mitambo hii ambayo ingewekwa hapa nchini, kwa mwaka tungeweza kupata zaidi ya trilioni 10 na kuendelea. Ni vizuri hayo mazungumzo ambayo yamekwamisha wawekezaji kuweza kuendelea kuwekeza kwenye suala hili yakapewa umuhimu ili yaweze kufanyika na kufikia muafaka mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo Kamati ya Bajeti imependekeza ni suala la magofu kwenye shule, maabara na zahanati. Kuna magofu mengi sana na mwaka jana kwenye bajeti tulipendekeza kwamba hela nyingi ziwekwe kwa ajili ya kukamilisha magofu haya, lakini naona kwenye mapendekezo ya mwaka huu hayapo. Ni vizuri aka-*take note* ya mambo hayo ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miradi ya mikakati. Suala hili ni zuri sana kwa sababu najua miradi ya mikakati ambayo ilipitishwa kwenye mwaka wa fedha 2017/2018 ni 17 tu, lakini ni vizuri miradi hii ikasambazwa kwenye kila Halmashauri, kwa sababu najua ni *source* kubwa sana ambayo ingeweza kuleta mapato mengi kwa Serikali kama miradi hiyo itaweza kuwekwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ni vizuri ikagawiwa kwa usawa kwa sababu utakuta ile miradi 17 ambayo imegawiwa, mikoa mingine imepata miradi miwili, mitatu wakati mikoa mingine hajipata mradi hata mmoja. Ni vizuri iangaliwe ili tuweze kupata usawa katika ugawaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo linatakiwa liongezewe fedha. Kwa kweli Wajumbe wengi wameongea hapa na ni muhimu likaangaliwa. Fedha ambazo zinatengwa kwenye sekta ya kilimo ni ndogo sana na ni vizuri

fedha hizo zikaongezwa ili tuweze kusonga mbele kwa sababu kazi kubwa ya Watanzania wengi iko kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji pia ni vizuri liangaliwe. Sasa hivi tumefanya vizuri sana kwenye mambo ya miundombinu, lakini suala la maji bado ni tatizo kubwa, linaleta matatizo mengi sana kwa wapiga kura wetu na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi huu mpango wa *certificate*, tumepeleka *certificates* kule, wakandarasi wamefanya kazi, *certificates* zimekwama kule karibu miezi sita. Sasa Wizara ya Maji sijui inatambia nini kwa sababu linakwamisha na jinsi unavyomkwamisha mkandarasi anaongeza *interest* kwenye ule mradi kufuatana na mkataba ambao upo. Ni vizuri suala hilo likaangaliwa kwa undani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *REA* pia ni vizuri likaangaliwa kwa sababu wakandarasi wapo na kila siku kule wanakwambia kwamba tunasubiri vifaa. Mheshimiwa Dkt. Kalemani amefika Muheza na ameona hali ya kule, mkandarasi yule uwezo wake ni mdogo kabisa, ameweka vijiji viwili tu mpaka sasa hivi. Tangu Mheshimiwa Waziri amekuja kuzindua, hajaendelea tena, ukimwuliza anakwambia bado vifaa vinakuja, hivyo vifaa vitakuja lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la motisha kwa watumishi wa Serikali. Kwenye Mpango huu sijaona kuongezwa mishahara ya watumishi. Mishahara ya watumishi ni kitu cha muhimu sana, hatuwezi kukaa na watumishi miaka mitatu hatujawaongeza mishahara, pamoja na mambo mengine, lakini hawawezi kuelewa. Kwa hiyo, naomba kabisa kwenye Mapendekezo ya Mpango huu kwenye bajeti ijayo mishahara iweze kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab kwa mchango wako. Ni mchango mzuri sana na hasa

ulipomalizia hapo, hata mimi ndiyo maana tulisema lile swali lingine lirudishwe. Masuala ya watumishi yanapaswa kupewa kipaumbele cha aina yake. Kama mtu anakaa miaka kumi hajapandishwa cheo na baadaye hakuna msererereko wala nini itawavunja moyo sana watumishi wetu. Tuwaangalie kipekee sana watumishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dkt. Sware, atafuatiwa na Mheshimiwa Zungu dakika tano tano.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii na mimi niweze kutoa maoni yangu katika mpango ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa kwenye Kamati yetu ya Bajeti kuongea na Serikali kuhusu Mpango huu na ninaomba nirejee tena kwa *issues* nilizozi-raise. Nilikuwa nasema ni ngumu kujua nchi yetu inasimamia uchumi gani na ina mipango gani kwa ujumla wake. Mfano, muhula wa Mheshimiwa Rais Mwinyi alisimamia soko huria na ni kipindi hiki ambacho mashirika mengi na viwanda vyetu vya Serikali vilifungwa. Alipokuja Mheshimiwa Mkapa alisimamia ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na aliimarisha TRA pamoja na kuzingatia zaidi katika ulipaji wa madeni ya nchi. Kipindi cha Mheshimiwa Kikwete yeye alikuwa na kauli mbiu ya maisha bora kwa kila Mtanzania na alijikita zaidi katika ujenzi wa miundombinu. Muhula huu tulionao sasa Mheshimiwa Magufuli amesimamia uchumi wa viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu nilikuwa najjuliza, *core business* ya nchi hii ni nini? Mwanafunzi labda anapojifunza uchumi au jiografia ya nchi fulani uchumi wao ni wa nini? Tunatoa mawazo mbalimbali, Wajumbe wengi hapa wanaongelea kuhusu sekta nzima ya kilimo kwamba wananchi wengi wa nchi hii tumesimamia katika ufugaji, uvuvi na kilimo chenyewe au bidhaa za misitu, ndio *majority* ya wananchi wetu. Katika nchi yetu kila kipindi cha miaka kumi tuna lengo fulani, lakini taswira kubwa ya nchi ni nini? Umaskini upo pale pale na mikakati na mipango hii

tunayojiwekea kila wakati huenda ikibadilika na mara nyingi haifikii hata nusu ya malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika kitabu chetu cha Mpango kwa ajili ya mwaka huu wa fedha unaotaka kuja, vipaumbele vimewekwa katika maeneo nane. Kati ya hayo, saba ni kwenye sekta ya miundombinu na moja imeongelea kuhusu kusomesha kwa wingi wataalam kwenye fani ya ujuzi adimu, mfano uhandisi, urubani, udaktari bingwa na ufundi. Tunarudi kwenye swali nchi yetu inaenda kwa kutegemea nini? Tunarudi pale pale kwenye sekta ya kilimo. Sasa uko wapi huu mfungamanisho wa kile tunachokifanya na hii sera ya viwanda tuliyona sasa hivi? Uko wapi mfungamanisho wa hii sera ya viwanda na shughuli za elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ungetegemea kwamba kwa miaka hii mitano ya muhula huu mpya wa Mheshimiwa Rais Magufuli tunasema kuhusu viwanda, tungeona iko *reflected* kwenye sekta ya elimu, VETA zinafanya nini, vyo vikiu vinafanya nini kwa ajili ya viwanda gani? Tungeona mfungamanisho wa sekta ya viwanda na shughuli za kilimo kwa ujumla wake. Pembejeo zikoje, tuna shida ya masoko, vifaa vya ukulima na vifaa ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabunge yaliyopita kulikuwa na Kamati kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu na tulionyesha ni rasilimali ambayo iko tu hatujaifanyia *investment* yoyote. Tangu niingie Bunge hili nilikuwa naona kuna mipango inaongelea kuhusu bandari ya uvuvi ili kujenga sekta ya uvuvi hususan katika bahari kuu, lakini haipo humu ndani, iko *silent*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Menyekiti, sasa unajuliza Serikali yetu inataka kusimamia nini? Kwa hiyo, inakuwa ni rahisi sisi kama Wajumbe wako kuweza kuchangia katika Mpango, lakini inakuwa ni kama *Q&A*, tunatoa mapendekezo *majority* ya hayo mapendekezo yanakita kwenye sekta ya kilimo, lakini majibu yanayokuja tutarudia pale pale kwenye miundombinu. Miundombinu kwa ajili ya nani na kwa ajili ya

nini? Ni wakati gani unatakiwa u-*invest* katika miuondombinu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea *SGR* inaenda kihatua hatua kwa fedha za ndani, inaishia Morogoro, itaishia hapa Dodoma *and then what?* Tunataka *lane* sita ya kutoka Dar es Salaam, mradi wa Chalinze - Dar es Salaam, ulikuwepo ni mzuri lakini umeishia katikati, tunataka nini? (Makofi)

(Hapa kengele *illia* kuashiria  
kuisha kwa muda wa *Mzungumzaji*)

**MWENYEITI:** Ahsante sana. Dakika tano zimeisha.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zungu dakika tano pia, atafuata Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa dakika tano ulizonipa. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na maendeleo ya nchi yetu yanavyokwenda chini ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimshauri, ni miaka mingi tu namshauri Mheshimiwa Waziri kuhusu biashara ya bandari na maeneo mengine ambayo si *friendly* kwa *importers* na *exporters*. Ukichukua mfano wa *container* la futi 20 ambalo sasa hivi gharama yake kwa Bandari ya Mombasa ni dola 80, wamepunguza kutoka dola 103. Kwa Tanzania *container* la futi 20 *handling charges* zake ni dola 170. Sasa hii haiwezi ku-*attract importes* kutumia Bandari ya Dar es Salaam na kuweza ku-*encourage volume* ya *importation*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam *transit goods* ambazo ndizo tunazozitegemea, ndiyo uzima kabisa wa bandari yetu, *importation container* futi 20 ni dola

100 *handling charges* lakini ukienda Kenya ni dola 60. Kwa hiyo, watu wengi lazima watahamia katika bandari ambayo ina unafuu. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri aendelee kuchukua ushauri wa kutazama ni namna gani *tariffs* za kodi za *importation* za bandari zetu zitashuka, ziwe *friendly* kwa wafanyabiashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine naotaka nimpe Mheshimiwa Waziri ni kutazama gharama za kodi Tanzania. Tulijaribu kumshauri Waziri siku za nyuma ajaribu kutazama na huu ulikuwa ni mpango wa siku nyingi, *VAT* ilipoanza ilikuwa ni 20%, ikashuka to 18% ilikuwa ni utaratibu wa Serikali kuendelea kuishusha *VAT* kuja 16% au hata 17% ili ku-*encourage industries*. *Industries* zikiwa *encouraged* ajira na *growth* zitaongezeka. Kwa hiyo, namuomba Waziri atazame sasa hivi suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *excise duty; soft drinks* sasa hivi Tanzania *production* imeshuka sana kwa sababu gharama ni kubwa na wananchi hawawezi kumudu kununua maji au soda. *Excise duty* ukiipunguza *volume* ya mauzo itakuwa na *production* itakuwa kubwa kwa maana Serikali haitapoteza kitu, itapata mapato yake kwenye *consumption tax*. Mnywaji akinywa soda au maji kodi inalipwa. Kwa hiyo, naomba Waziri alitazame suala hili ili kuona namna ya ku-*encourage growth*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine atazame gharama za *importation* ya *industrial sugar*. Wafanyabiashara wengi wanalalamika, wanalipa *deposit* ya pesa, lakini sasa ni zaidi ya miaka mitatu, minne hawarudishiwi pesa zao na imekwenda juu sasa imefika zaidi ya shilingi bilioni 45 na hii ni mitaji ya wafanyabiashara. Wafanyabiashara wanalipa kodi vizuri, Serikali ikitazama maeneo mazuri ya kukaa na kushirikiana nao mapato mengi ya kodi Serikali itayapata bila kuwa na viwango vikubwa ambavyo vinawakimbiza. Wafanyabiashara wengi sasa hivi wanaondoka kwenda nchi zingine. Ni lazima tu-*attract investors* kwa kuwa na *tariffs* nzuri na *friendly* za kodi nchini mwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Uchangiaji huo, ule nilioueleza, wa Maseneta. Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Cecil Mwambe, sijui atalivuruga. *(Kicheko)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na usipate hofu. Bahati mbaya sana kila mara tunapopewa nafasi tunapojaribu kuishauri Serikali kwa sababu wametubandika jina wanaita vyama vya upinzani badala ya kuita vyama rafiki vya vyama tawala, basi kile tunachokisema mara nyingi wao wanafikiri kwamba tunakuja kupinga. Hata hivyo, kila mara tukija humu ndani tuna mawazo mazuri kabisa, tumeona hotuba yetu ya Kambi ilivyosema, bahati mbaya sana wakati wa bajeti hatukupata nafasi ya kutoa hizi hotuba lakini leo tumewaeleza hapo kuhusiana na huu mpango uliko hapo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hiki kitabu cha mpango wa mwaka mmoja ambao Mheshimiwa Dkt. Mpango ametuletea hapa, sisi kama Wabunge kazi yetu ya kwanza kabisa ni pamoja na kuishauri Serikali. Tumejaribu kushauri mara nyingi lakini Mheshimiwa Dkt. Mpango alikuwa anafikiri kama tunampinga na kubeza, kile tunachokiwaza sisi na mawazo yetu mengi yalikuwa hayachukuliwi ili kuboresha na kulifanya Taifa letu liende pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye hotuba yake kama ambavyo iko mbele yetu kwenye ukurasa wa 34, maeneo mengi yanaonesha ni namna gani mipango mingi iliyokuwa imepangwa itekelezwa mwaka jana haikutekenezeka. Nitatoa tu mfano wa masuala machache. Anasema kutofikiwa kwa lengo la kodi zinazotokana na ajira *(Pay As You Earn)*, anatoa na sababu, kulikosababishwa na kutofikiwa kwa malengo ya ajira mpya na kutoongezeka kwa mishahara. Sasa ni mara ngapi humu ndani tumesimama



tunajaribu kuishauri Serikali iongeze mishahara kwa watumishi ili haya mambo yaweze kufuatiliwa pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kweli kabisa kutoka moyoni na ningetamani sana kabla ya ule mdahalo ambao ulifanyika chuo kikuu usingefanyika kwanza mpaka Mheshimiwa Dkt. Mpango alete huu mpango wake na kulleleza Taifa ni nini kinatokea. Maprofesa walismama pale wakaishia tu kusifu, kutukuza na kupongeza, muda wote ndiyo kazi ambayo waliifanya lakini hawakushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Dkt. Mpango anakuja tena ndani ya Bunge anatumia mwenyewe ni namna gani mambo huko nje hayaendi. Hili ni jambo la sisi wote kumpongeza badala ya kuishia tu kusifia yale mazuri au kusifia yale mengine tunayofikiri kwamba ni ya kujenga lakini kimsingi Mheshimiwa Dkt. Mpango mwenyewe anakiri kwamba mambo hayaendi, uchumi umeporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukieda kwenye *point* yake namba tatu anasema, kushuka kwa biashara za kimataifa kulikopelekea kutofikia malengo ya uingizwaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kama ambavyo ilitarajiwa. Anaendelea kusema kwamba, kuendelea kuwepo kwa madai mbalimbali yakiwemo ya wakandarasi, watoa huduma, wazabuni na watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani kila siku tunakuja na neno uhakiki ili tuweze kuwalipa watumishi wa umma lakini bado wanakiri madai hayo yapo, wakandarasi wa ndani hawalipwi, kwa hiyo, maana yake pesa haizunguki. Hawa wakandarasi wa ndani ndiyo watu ambao wanaendesha uchumi wa nchi yetu, wao ndiyo wanaokwenda kununua kwenye maduka yetu madogomadogo na kufanya uchumi uweze kuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nimwambie kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwamba sisi Chama cha Demokrasia na Maendeleo tumekuja na Sera Mbadala na naomba nikupe hii *copy* kama zawadi ukaisome na jioni nitakuletea *copy* nyingine ikiwezekana umfikishie Mheshimiwa Rais naye asome aone mawazo yetu, alinganishe na hayo ya kwenu muweze kuboresha. Haya yote uliyoyasema hapa ndani na kuyaandika hapo mimi nataka tu nikupeleke katika baadhi ya *pages* kwenye sera yetu halafu wewe utakwenda kusoma zaidi uweze kudadavua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye Sera ya CHADEMA ukurasa wa 17, hapa tumeweka wazi Mheshimiwa Dkt. Mpango na naomba ukasome vizuri tu, tunaongelea kuhusu mikakati jumuishi ya uchumi wa Taifa. Tunasema hivi, kuimarisha uchumi, kukabiliana na changamoto za ajira na bei ya bidhaa, ndiyo ambayo umeyalalamikia huku, sisi tumepata suluhisho, utakwenda kuisoma mwenyewe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili tunasema, kuwa na mfumo wa kodi unaotabirika. Mheshimiwa Zungu hapa ametoka kuchangia sasa hivi anakueleza masuala ya kodi yasiyotabirika (*unrealistic taxes*). Tunakwenda kutoza watu kodi, watu wanalalamika *VAT* hazirudishwi, kodi ya sukari ghafi kwenye viwanda hazirudishwi. Kwa hiyo, tunaomba kuwe kuna mfumo wa kodi unaotabirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunasema hivi, kuhakikisha kuwa kuna uwiano kati ya mauzo ya nje na kuagiza bidhaa za chini. Hii inakwenda sambamba kabisa na unapokuja hapa, sisi tumeanza kutengeneza reli na tulimshauri wakati fulani, tunakwenda kutengeneza Reli ya Kati (*Standard Gauge*), tunanunua chuma nje, wataalam nao wanatoka nje, hivi kwa nini tusifikirie kwanza tukaanza kutengeneza kiwanda mama cha chuma kule Mchuchuma pamoja na kuboresha na kutengeneza Reli ya Kusini ili kwamba chuma yetu ya Mchuchuma tuilete Bandari ya Mtwara ikifika pale Mtwara itaondoka, nyingine itakwenda kuuzwa nje, nyingine itakuja kutengeneza Reli yetu ya Kati.

Ile tutakayouza nje tutapata pesa za kigeni, badala ya kwenda kukopa kule nje tutakuja kutengeza reli yetu kwa kutumia pesa zetu sisi wenyewe. Kwa hiyo, haya ni mawazo ambayo sisi tunayo na yapo kwenye sera yetu, utakapopata nafasi Mheshimiwa Waziri nenda kaisome vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pia ukurasa wa 19, nataka nikuongeze madini ili tuweze kuboresha, tuishauri Serikali ili nchi yetu iweze kusonga mbele kwa sababu sasa hivi imesimama. Tunakuja hapa kwenye uchumi wa viwanda vyenye tija, hiyo ndiyo sera yetu sisi inavyosema. Tunasema kwamba, kutekeleza mkakati wa mabadiliko makubwa katika sekta ya viwanda. Mheshimiwa Dkt. Mpango, nadhani unaona hali ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara lakini tumejaribu kuomba kwa Waziri wa Viwanda watupeleke kwenye viwanda wanavyoviita vilibinafsishwa, viwanda 155 tuweze kujua viko kwenye *status* gani ili tuweze kuishauri vizuri Serikali na kuona namna ya kusonga mbele lakini nikueleze kabisa sijui kama Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Naibu wake wana nia njema kabisa ya kuhakikisha wanamsaidia Rais kwenye kupata viwanda. Sisi kama CHADEMA tumekuja na suluhisho utakapopata nafasi utasoma utaona namna ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tunatamani kufungamanisha uchumi wa ndani na viwanda. Tunaimba kuhusu viwanda, viwanda vinavyofanya kazi ni viwanda vichache vya *tiles*, vya nondo ambavyo vyote vimekuwa *concentrated* huu Ukanda wa Pwani kwa maana ya maeneo ya Mkuranga na kwingine. Sasa atakayekwenda kununua nondo ni nani na anakwenda kuzitumia wapi kama mazao yake ya shambani hayapatai bei bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia sasa hivi hapa kuna hii sintofahamu ya masuala ya korosho lakini ni kwa sababu tu ya kutokuwa na mpango bora kwenye jambo

hili. Wale wanunuzi walilazimishwa kuitikia kwamba watakwenda kununua kwa bei ya Sh.3,000. Kimsingi gharama ya kuitoa korosho sasa hivi kuifikisha India ni zaidi ya Sh.4,000 wakati kule wanauza kwa dola moja na senti tatu sawasawa na Sh.3,800 ya Kitanzaia. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kwanza ikiwezekana warudishe ile Sheria ya *export levy*, iletwe hapa ndani ifutwe kabisa ili kuweza kunusuru hawa wakulima sasa hivi waweze kupata pesa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tuwaombe sasa, kwa sababu hiyo bei iliyopangwa siyo *realistic* na watu wanafikiri kwamba wanaolazimisha hii bei isitokee pale ni watu wa Kangomba. Korosho bei elekezi ni Sh.1,550 ndiyo ambayo ilipangwa pale, mtu anakuja na Sh.2,700 anataka kununua tunamwambia hii bei haijakidhi. Ndiyo ni bei ya chini lakini inategemea na soko. Kitendo cha kuondoa *export levy*, ile pesa ambayo ilitakiwa irudi kwa wakulima zile pembejeo na vitu vingine ndiyo imeleta hii *trickle action*, tunaona sasa athari zake zinazopatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itapoteza mapato kutokana na mauzo ya korosho na uzalishaji umeshuka. Pia Serikali inaweza ikaleta shida zaidi kwamba hizi korosho mwaka huu zisiishe kwa sababu msimu wa maeneo mengine unaanza, korosho yetu inaweza ikabaki, iko nyingi kwenye maghala. Kwa taarifa yako tu, tunavyoongea hapa sasa hivi leo ilikuwa ufanyike mnada wa Tunduru lakini kimsingi hakuna mnunuzi hata mmoja aliyekwenda Tunduru kwenda ku-*bid* kwa sababu hawawezi kutimiza yale masharti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niendeleo na kitabu chetu cha sera. Ukienda pia ukurasa wa 22 katika harakati za kuendelea kumshuari Mheshimiwa Dkt. Mpango tunasema hivi, usimamizi madhubuti, endelevu wa sekta ya madini...

## T A A R I F A

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, nimemuona Mheshimiwa amesimama.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mwambe kwamba hicho kitabu anachosema cha CHADEMA, kwenye uandishi huwa kuna kitu kinaitwa *plagiarism*. Mipango yote ukiangalia iko kwenye mipango ya miaka mitano na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, wange-*cite* kwamba wame-*borrow* kutoka kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tungekwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kumpa hiyo taarifa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Anakukumbusha tu kwamba mmedesa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweza mkaingia wanafunzi wawili darasani mnafanya mtihani halafu yule anayedesa akafaulu vizuri kuliko aliyeingia na desa lenyewe kule ndani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini unaulinda muda wangu, kwa hiyo, anachokifanya Mheshimiwa Innocent sikishangai na hawa ndugu zetu wa Chama cha Mapinduzi wanachokifanya wao wanaongelea kuhusu Ilani, sisi tunaongelea kuhusu sera na sisi tuna mawazo yetu tunataka tuyalete hapo mbele ya safari ili yatumike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba niendeleo, nimesikia alichokisema napokea taarifa yake.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Zitto nini tena?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo ya Taifa si mpango wa chama chochote cha siasa. Mpango wa Maendeleo ya Taifa ni mpango wa Watanzania wote. Ilani za vyama vya siasa vinaona namna ya kuutekeleza huo mpango kwa taratibu zao wao. Kwa hiyo, maelezo ambayo ndugu yangu, rafiki yangu, Mheshimiwa Innocent ameyatoa dhidi ya Mheshimiwa Mwambe si sahihi na naomba tu amuombe radhi Mheshimiwa Mwambe, hapakuwa na *plagiarism*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe, malizia, dakika zako.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za Mheshimiwa Zitto naikubali.

**MWENYEKITI:** Malizia dakika zako zimebaki chache sana.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Naam!

**MWENYEKITI:** Dakika zako zimebaki chache sana, malizia.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mheshimiwa Zitto nimeipokea na yenyewe iingie kama sehemu ya mchango wangu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kwamba kuna jambo ambalo linaendelea pale, suala la usimamizi madhubuti na endelevu wa sekta ya madini. Tunaomba kabisa...

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ni kengele ya pili.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya sana Mheshimiwa Cecil. Ahsante sana. *(Makofi)*

Anakuja Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kupongeza na kuishukuru Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa inayoifanya katika miradi mikubwa ya maendeleo, bila kusahau mradi mkubwa wa umeme ambao utatutoa katika matatizo ya umeme wa *Stiegler's Gauge* ambao Mheshimiwa Rais ameuvulia njuga na tunamuunga mkono; mradi wa reli ambao utaondoa tatizo la usafiri, ikiwa ni pamoja na Wabunge kuja Dodoma itakuwa ni chini ya saa tatu, tunaunga mkono na tuna imani tutainua uchumi wetu kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendeleo kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu ameendelea kutekeleza miradi mikubwa katika maeneo mbalimbali. Pwani tuna mradi wa barabara, Awamu ya I, kutoka Ubungo mpaka Kibaha ambayo ni *six lane* pamoja na Daraja la Ubungo. Nilisikia mtu akisema kwamba Daraja la Ubungo halina thamani kwa wakulima vijijini lakini ukweli ni kwamba mazao ya wakulima yanayotoka katika vijiji yatafika Dar es Salaam na yatanunuliwa kwa bei nzuri na mkulima kule atafaidi lakini hata sisi watoto wa huyo mkulima na ndugu zao tutatumia daraja lile na uchumi utachangamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya yanafanyika kwa ajili ya Watanzania. Mheshimiwa Rais na Serikali yake atajenga miradi hii, haondoki nayo inabaki, tutaendelea kuitumia na atakapomaliza kipindi chake, watoto wetu na wajukuu wetu. Jambo kubwa ni sisi tumuunge mkono Mheshimiwa Rais na Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na tuishauri iendeleo

kufanya kazi nzuri ili maendeleo katika nchi yetu yaweze kuja kwa haraka.

Nataka niseme na kumpa moyo Mheshimiwa Rais kwamba hata wafanyabiashara walio wengi sasa *voluntarily* wanalipa kodi kwa sababu wanaona matokeo ya kodi zao kwamba zinakwenda kufanya mambo makubwa ya maendeleo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu kwamba katika miradi hii, iko miradi mikubwa na ambayo ni *complicated* kuiendesha kama Shirika la Ndege na ninajua ndege nyingine zinakuja, tusiogope kushirikisha *experts*. Tushirikishe *experts* wenye uzoefu kutoka nje, washirikiane na *management* ya Kitanzania ili tuweze kufikia malengo na mafanikio ya miradi hii mikubwa. Nina imani kama tuta-*blend skills* na *expertise* kutoka nje na ndani ya nchi ni wazi kwamba tutaweza kupeleka mbele gurudumu la maendeleo kwa kuhakikisha miradi hii inakwenda kuleta mafanikio makubwa na kuibadilisha kabisa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka vilevile nizungumzie suala la mazingira ya kufanya biashara. Nafahamu ili mipango hii ya maendeleo iweze kufanikiwa ni lazima mazingira ya ndani ya kufanya biashara yaboreke. Najua Serikali imeshachukua hatua ikiwa ni pamoja na kutengeneza ile *blueprint* ya kuhakikisha kwamba taasisi zinazohusika na kudhibiti ufanyaji wa biashara zinakuwa ni msaada kwa wafanyabiashara wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokiomba hapa sasa, Serikali ihimiza utaratibu huu, ile *blueprint* sasa iende kwenye vitendo ili isaidie ukamilishaji na utekelezaji wa miradi hii ya maendeleo na ili kila Mtanzania aweze kufanya biashara katika hali ambayo haina usumbufu na yenye tija. Masuala ya kodi yakae vizuri, masuala ya *compliance* mbalimbali ikiwa ni pamoja na *TBS*, *TFDA* pamoja na taasisi nyingine ziweze kumsaidia mfanyabiashara achangamshe uchumi, kodi zilipwe na hatimaye tufikie malengo yetu. Naomba



*blueprint* sasa iende kufanyiwa kazi na iende kwenye utekelezaji na isiendeele kubakia katika vitabu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imechukua hatua na hatua hii ni hapohapo katika kwenda kuboresha mpango wetu wa maendeleo. Imechukua hatua ya kulinda viwanda vya ndani ikiwa ni pamoja na kuongeza baadhi ya *tariffs* na imechukua hatua hata ya kupunguza kodi katika bidhaa mbalimbali. Lengo na madhumuni siyo kumfaidisha mfanyabiashara peke yake bali pia kumfaidisha Mtanzania aliye kijijini anayetumia bidhaa zile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadhi ya wafanyabiashara sasa hawafanyi hivyo, matokeo yake baada ya kuweka *tariffs* za bidhaa za nje zikaenda juu na wenyewe wanapandisha bei ya bidhaa zao badala ya ku-*capitalize* katika kuuza zaidi kwa sababu bidhaa zao sasa ni bei rahisi. Niombe sana, azma ya Serikali kufanya hivyo ni kulinda viwanda na kumrahisishia Mtanzania kupata bidhaa kwa bei nzuri na kuhakikisha viwanda vinazidisha uzalishaji. Rai yangu hapa, wenye viwanda na wafanyabiashara walichukue jambo hili au wachukue hili punguzo au ongezeko la bei za bidhaa kutoka nje kuzalisha zaidi na wasiongeze bei kumuumiza yule mlaji wa mwisho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi hii mikubwa ya maendeleo ambayo Serikali imejikita ni wazi kwamba utekelezaji wake unahitaji fedha nyingi na ili fedha ziweze kupatikana ni lazima ulipaji wa kodi uwe mkubwa na ili ulipaji wa kodi uweze kuwa mkubwa ni pamoja na Serikali kwa makusudi kuchangamsha biashara za ndani. Ili biashara za ndani ziweze kuchangamka ni pamoja na kuhakikisha madeni mbalimbali ya wafanyabiashara Serikalini yanalipwa kwa sababu, *the main stimulant* ya uchumi katika nchi yoyote ile ni Serikali. Katika uchumi wa nchi yetu ulio mdogo ni wazi kwamba mwajiri wa kwanza wa makampuni madogo katika nchi ni Serikali. Kwa hiyo, nina uhakika Serikali ikijikita katika kulipa madeni siku ya mwisho zile fedha zitarudi katika utaratibu wa kodi na uchumi utachangamka na miradi hii itaweza kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na hakika naunga mkono hoja na tuko pamoja katika kuhakikisha miradi na mipango hii ya maendeleo inatakamilika. Ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha. Nilishamtaja Mheshimiwa Hussein Bashe na atafutiwa na Mheshimiwa Yusuph Kaiza Makame kutoka CUF.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza mimi nianze kwa kumnukuu aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mzee Yussuf Makamba. Mzee Yussuf Makamba aliwahi kusema maneno yafuatayo, binadamu hutazamwa katika maeneo matatu. Jicho la kwanza ni namna wewe mwenyewe unavyojitazama na kujifahamu, Jicho la pili ni namna ambavyo Mwenyezi Mungu anakufahamu na kukuelewa. Jicho la tatu ni namna ambavyo wenzako wanakutazama na kukufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na maneno haya nikichukua maumbile ya binadamu kama nchi na kuifananisha na binadamu. Sisi kama Taifa ni namna gani tunajitazama? Tunajitazama kwa kujiwekea vigezo vya kujipima, lakini wako wenzetu vilevile wanatutazama, wanavyotutazama wanatuwekea vigezo vya kutupima. Sisi kama nchi siyo kijiji, tumeungana na dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango huu utakuwa ni Mpango wa nne. Kwa heshima kabisa, kama hatutaamua kama Taifa ku-*unlock* mambo mawili ambayo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakisema humu ndani kwa miaka mitatu ambayo mimi nimekuwemo hatuwezi kupiga hatua kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taifa letu asilimia 60 mpaka asilimia 70 ni wakulima. Hawa ndio *drivers wa dream* ya kuanzisha viwanda na kufanya kila kitu. Tunajenga reli ambayo tutasafirisha bidhaa, tunajenga barabara ambayo tutasafirisha bidhaa na binadamu; leo mazao yote ya kilimo, ya chakula na ya biashara yanaanguka kwa *factors* za nje na *factors* za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuwa tunashauri katika mapendekezo haya namuomba kwa heshima, hatua ya kwanza ku-*rescue sector* ya kilimo anachotakiwa kufanya ni kuja na mpango wa kuanzisha *Price Stabilisation Fund*. Tusipoanzisha mfuko ambao utakuwa na fedha ambazo zitakuwa zina-*cover* hasara zinazowakabili...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, ni vizuri muwe mnasikiliza mambo haya mengi yanawahusu ninyi wenyewe. Endelea Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutaanzisha *Price Stabilisation Fund*, hatuwezi kupiga hatua kama Taifa. Kwa sababu wakulima ambao ndiyo asilimia 70 tunatarajia auze mahindi yake Nzega akanunue bati. Leo mahindi ni Sh.18,000, Sh.20,000, bati bandari moja imeongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu *almost* mara mbili. Kwa taarifa mazao ya kilimo yanashuka bei kwa zaidi ya 20%; ni taarifa za *NBS* na za Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano zao la korosho, hatuna uwezo wa ku-*control* bei ya soko dunia sisi, lakini sisi tuna uwezo wa ku-*control volumes*. Ili tu-*control volumes* ni lazima tuwape *incentives* wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mfuko wa mahindi wa kilo mbili ni Sh.12,000, nataka niwape hizi takwimu. Mkulima ninayemuongelea ni huyu anayetumia mbegu ya *hybrid* ambayo kwenye heka moja atapata magunia 20 ambayo yatampatia kilo 2,000. Sasa ili alime heka moja atatumia

*tractor* kwa Sh.45,000, tuandike, atafanya *harrow* kwa Sh.40,000, atatumia mbolea ya kupandia kwa Sh.65,000, atapalilia kwa Sh.25,000 mara mbili Sh.50,000, atatumia mbolea ya kukuzia kwa Sh.70,000, atanunua mbegu ya *hybrid* kilo moja Sh.6,000 kwenye heka moja atatumia mifuko nane ambayo ni Sh.48,000. Mkulima huyu ataweka ulinzi, atavuna, atapakia, ataweka dawa, ukichukua gharama yake ni karibu Sh.650,000. Gawa kwa huyo amepata *at the optimal, best production*, tani mbili ni Sh.325, bei leo kilo moja Sh.150. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima, tuchukulie zao la korosho, tumbaku sisi imeanguka leo ni mwaka wa pili wa tatu. Nataka nitoe ushauri na ni ushauri tu, *it is pure administrative*. Leo Mheshimiwa Rais kachukua hatua kasema korosho inunuliwe kwa Sh.3,000, ushauri wangu kwa heshima Mheshimiwa Dkt. Mpango wafanyabisahara wamesema watanunua kwa Sh.2,700 waagizeni nunueni kwa Sh.3,000 sisi kama Serikali tuta-*subsidise* hiyo Sh.300 mnayopata hasara ili mkulima asipate hasara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kutoka, *this is the practise all over the world*. Lazima tutengeneze *a buffer plan* kwa wakulima wetu. Tusipofanya namna hii madhara wanayoyapata wakulima kitakachotokea *demand* na *purchasing power* ya wakulima itashuka, ndio asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unatoka Dodoma. Zao la zabibu, mimi nitampa Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango *World Economic Forum* wamefanya *Competitive Index Report* ya dunia wametumia *rank* sisi 100. Hii siyo *World Bank Report* ambayo imetumia *rank* 140 ambayo tumeporomoka kwa *digit 4*. Hawa watu wa *World Economic Forum* wamefanya *survey* kwa ma-CEO wa Kitanzania. Ma-CEO wa Kitanzania na wafanyabiashara wa Kitanzania wametaja mambo matano ambayo ni matatizo katika nchi yetu kwa ajili ya kufanya biashara. La kwanza wamesema *access to financing*, la pili *right to own properties*, la tatu *tax rate*, la nne *tax regulation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachoshangaa ni jambo moja, Serikali imechukua hatua nzuri ya kutengeneza *document ya blue print*, nachojiuliza kwa nini wasilete sheria na kwenye *document ya mpango kungekuwa na chapter inayoongelea tax reforms* tutakazozifanya kutokana na *document ya blue print*. Nilitarajia nione hili kwamba tutafanya mabadiliko ya kodi na *regulations* katika mwaka huu wa 2019/2020 katika maeneo haya baada ya kuandaa *document ya blue print*, hakuna. Kinachotokea ni nini? Nashindwa kuelewa kwa nini tunaandaa kwa haraka Muswada wa Vyama vya Siasa? Kwa nini tusilete Sheria za Kodi ambazo ni *bottleneck to the economy*, kwa nini? *What is our priority?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuonea huruma sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mimi naona kuna tatizo sana Serikalini Mheshimiwa Waziri Mkuu. *It is either* Mawaziri na wataalam wameamua kutokufikiri ama wameamua kutegeana, hakuna kitu kingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojiuliza tumbaku inaporomoka, *the biggest market* ya tumbaku sasa hivi ingekuwa *Middle East, what are we doing as a country? Far East, what are we doing as a country?* Yaani husikii, tunaambiwa tu tupunguze *production*, tumbaku imekuwa shida. Leo korosho tunaenda kwenye *crisis*. Nataka nishauri, sisi hatuna *control* na bei za dunia, tuna *control* na *volumes* za ndani na ili tuweze ku-*expand volume* lazima tujenge *incentives*. (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia tu. Naomba Wizara ya Fedha njooni na *chapter* kwenye mpango wa Februari wa namna gani mnaokoa kilimo katika nchi hii kwa kuanzisha *price stabilisation*, namna

gani mnafanya *tax reforms* ili biashara ziweze kufanyika katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Eeh, leo uchangiaji wa mpango unakwenda hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Yussuf Kaizer Makame, atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara atafuata.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kusema kwamba miaka mitatu inatosha kujitathmini kile tulichopanga na tulichofanya na sasa tukaja na mpango mpya. Kwa miaka mitatu tulipanga kutumia trilioni kadhaa, mwaka 2015/2016 tulipanga shilingi trilioni 29, mwaka 2016/2017 tukapanga shilingi trilioni 31 na mwaka 2017/2018 tukapanga shilingi trilioni 32 hizo tulizoziandika. Hii inatosha kujitathmini kwamba mipango yetu tulyopanga na kile tunachokifanya ni *realistic*? Kwa hiyo, ni lazima tujiulize *are we realistic* kwa tunachokipanga na tunachokifanya kama Serikali? Hilo ni la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili nililisema kwenye Mpango wa 2016/2017 na jana kalisema Mheshimiwa Siliinde, mimi naona hakuna *succession plan* kwamba awamu hii na awamu hii wanapeana vipi mambo yao. Iivyo sasa awamu hii anatoka na kitabu chake na awamu ijayo anakuja na kitabu chake kipya kabisa *which is quite different*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na suala la Katiba Mpya. Katiba Mpya imetumia mamilioni ya pesa za Watanzania. Sasa hivi watu humu wanapita wanasema aah, ilikuwa mambo ya kisiasa, eeh! Katika *legacy* ambayo ataiacha Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli, katika *legacy* muhimu kuliko zote mnazoziona leo, basi ni kuandika

Katiba Mpya ya Watanzania. Kama leo mnaona *Standard Gauge Railway* na *Stieglers' Gorge* leo ni ya msingi, basi Katiba Mpya ni ya msingi zaidi kwa vizazi na miaka 100 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisema hili kwa sababu, Rais wa awamu iliyopita, Mheshimiwa Kikwete alileta Katiba Mpya, imefikia katika hatua za mwisho kumalizika tumelicha tunasema kwamba hatuna mpango nayo. Sasa hivi awamu hii ya Rais John Pombe Magufuli imekuja na *Stieglers' Gorge*, imekuja na *Standard Gauge Railway*, imekuja na *ATCL*, atakuja Rais mwingine, tumefika Makutupora tunataka twende Mwanza - Isaka kwenye *Standard Gauge Railway* asipokubali...

## T A A R I F A

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa wanataka wakupe tarifa hiyo *railway*. Mheshimiwa taarifa, tafadhali.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji ambaye anaendelea kwamba suala la Katiba Mpya kwanza wa kulaumiwa wa kwanza wanatakiwa wawe UKAWA kwa sababu ndiyo waliosusia mchakato wa Katiba Mpya wakatoka nje ya Bunge. Ahsante. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza ni mambo ya msingi, kwa sababu mimi Mheshimiwa Vuma ni rafiki yangu, acha tu aseme alichotaka kusema hakina shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the issue is* tunatumia rasilimali pesa ya Watanzania, tume-*invest* kwenye Katiba Mpya mabilioni ya pesa lakini sasa suala la Katiba Mpya tumeacha tumeanzisha *Standard Gauge Railway*, awamu itakayokuja 2025/2035 akisema kwamba mimi kipaumbele changu siyo *Standard Gauge Railway*, tunafanyaje? Atakapokuja mwingine akasema kwamba mimi kipaumbele changu siyo *ATCL*, tunafanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoshauri kuwe na Kamati au Tume Maalum ambayo inaratibu hii miradi ya kimkakati kwa nchi ili rasilimali zisipotee burebure, tumepoteza mabilioni ya pesa. Kila mtu akija na kitabu chake, Tanzania maisha yote tutalaumiana, humu tutakuja kuchekeshana, lakini hatutafika pale tunapotaka, ni lazima kuwe na *succession plan*, ni lazima kuwe na Tume itakayoratibu masuala ya Kitaifa ya kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimemsikia Rais mara mbili, mara ya kwanza alisema ataendelea pale alipomalizia Rais wa awamu iliyopita, lakini mara ya pili amesema hana mpango wa kutenga pesa ya Katiba Mpya. Mimi naomba nimshauri Waziri Mkuu, yeye ni msimamizi wa Serikali katika Bunge hili, Rais ni mtu, inawezekana ameteleza, inawezekana amekosea, Mheshimiwa Waziri Mkuu nenda kamshauri Rais juu ya Katiba Mpya, ni lazima irudi kwa Watanzania amalize mchakato huu na *legacy* yake itakuwa kubwa zaidi kuliko kitu kingine chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, Mheshimiwa Waziri Mkuu rudi kwa Mheshimiwa Rais, mimi ni mdogo sana, rudi kwa Mheshimiwa Rais kamshauri, mwambie yeye ni binadamu kama sisi *as long as* amepewa tu mamlaka ya kuongoza nchi hii, ni binadamu anaweza akakosea. Nenda kwa Rais mshauri tena kuhusu suala la Katiba Mpya amalize hapa palipobaki, ataacha *legacy* kubwa kuliko vitu vyote atakavyoviacha kwa muda mwingi utakaokuja au vizazi vyote vinavyokuja Tanzania. (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni mahusiano. Nataka nizungumze kidogo kuhusu mahusiano ya washirika wa Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar na nitazungumza kwenye vitu viwili tu, kwanza suala la VAT kwenye umeme. Suala hili pengine halitakiwi kuzungumzwa lakini tumelizungumza kwenye mipango yote kwamba Zanzibar ni nchi ndani ya Tanzania si nchi nje ya Tanzania. Sisi tunauza umeme, sisi tunanunua umeme VAT hiyo haipo. Kwa hiyo, sasa imefika muda Mheshimiwa Waziri wa Fedha alichukue na alilite kwenye mpango na kwenye bajeti liishe.

## T A A R I F A

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Taarifa, taarifa.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, liishe.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mwenye taarifa ni nani?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi bwana.

**MWENYEKITI:** Haya ruksa, Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nimeguswa na Mheshimiwa Kaiza kwa maslahi ya Zanzibar. Tanzania Bara umeme wananunua Uganda na VAT wanalipa moja, sisi tunaolipa mara mbili ni halali hii? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku...

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea tarifa hiyo ya Mheshimiwa Jaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nachotaka kusema ni kwamba miaka mitatu tunaenda mwaka wa nne tunazungimzia suala hili. Mara tunaambiwa kaeni na Wizara

ya Nishati na Madini ya wakati ule mta-so/ve, mwaka wa pili inaenda hivyo hivyo, mwaka wa tatu hivyo hivyo, huu ni mwaka wa nne, sasa ni muda wa Serikali kutekeleza jukumu lenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni nchi washirika. Zanzibar siyo Rwanda au Burundi, Zanzibar ni nchi ndani ya Muungano huu, ni washirika, hatuwezi kuuziwa umeme tofauti. Mnawauzia umeme Zambia lakini hakuna VAT hii, Kenya mnanunua Kenya mnanunua hakuna VAT hii, kwa nini Zanzibar?

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf, tunakushukuru.

**MHE. YUSSUF KAIZA MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda haupo upande wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Zitto, utafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Waitara kama nilivyosema na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze kwa uongozi wako wa kuhakikisha kwamba tunaitekeleza ipasavyo Katiba yetu Ibara ya 63(3)(c). Wewe unafahamu siku za nyuma tulikuwa hatufanyi hivi, lakini tangu tumeanza Bunge hili kila mwezi Novemba tumekuwa tukikutana na kutekeleza matakwa ya kikatiba. Kwa hiyo, napenda nikupongeze wewe binafsi kwa uongozi wako katika jambo kama hili, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia niende kwenye baadhi ya mambo ambayo napenda kuchangia kwa ajili ya kuboresha mpango kama jinsi ambavyo wenzangu

wametoka kuzungumza. Jambo la kwanza ni eneo la vipaumbele vya mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama tuna hotuba tatu sasa tangu tumeanza, kuanzia 2016 mpaka sasa. Ukichukua hotuba ya 2016, ukatazama vipaumbele vya mpango, wakati ule vililitwa miradi ya kielelezo, ukaenda 2017, 2018 jambo moja ambalo naliona ni kukosekana kwa *sequencing*. Unaanza na mambo fulani mwaka unaofuata una-*drop* baadhi, hata ambayo hayajatekelezwa kabisa, mwaka unaofuata una-*drop* mengine, hata ambayo hayajatekelezwa kabisa, matokeo yake ni kwamba kila mwaka tunakuwa tunaanza upya bila kufanya yale ambayo tungekuwa tumepaswa kuyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama mwaka 2016 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mpango ukurasa wa 18, jambo la kwanza kabisa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga. Ukienda mwaka 2017 ukurasa wa 29 lipo lakini kuna jambo la Mji wa Kilimo wa Mkulazi limegeuzwa kuwa shamba, halafu ukija 2018 hayapo kabisa na ni kwa sababu huko nyuma tumekuwa tukishindwa kuyatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama hilo maana yake ni kwamba tunakuwa tunapiga *mark time*, tunakutana, tunajadiliana, tunatoa mawazo, mwezi Februari yanakuja tunayaidhinisha vizuri, tunaenda kwenye bajeti, tunaweka bajeti na nitakuja kwenye hiyo hoja ya bajeti *credibility* halafu hakuna kinachofanyika. Mfano dhahiri kabisa ni hili jambo la Mchuchuma na Liganga ambalo tangu 2016 linaonekana kwenye mpango kama mradi kielelezo, kufika sasa limeondolewa kabisa kama mradi kielelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hili lifanyiwe marekebisho. Tujaribu kurudi 2016 tuangalie ile miradi vielelezo na tui-*update* utekelezeaji wake. Kuna ambayo imetekelezwa kama Reli ya Kati na kadhalika na ile ambayo

imeachwa tuweze kuiboresha ili tutakapokuja mwezi Februari, tuwe na kitu ambacho tumeanza nacho kuanzia mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni suala la *credibility* ya tunachokijadili hapa. Mwaka 2016 tulijadili na kukubaliana kwamba Serikali ikatenge shilingi trilioni 13.2 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo ambao tunaujadili kwa siku tano, wakaenda wakatoa trilioni 5 tu. 2017 tukasema zikatengwe shilingi trilioni 12, zikaenda zikatengwa trilioni 6 tu. Mwaka 2018 ndiyo tunapendekeza sasa zikatengwe tena shilingi trilioni 12. Hii inaonesha dhahiri kwamba kama hatutakuwa makini na kuanza kuhitaji uwajibikaji upande wa Serikali, tunapiga porojo. Kwa sababu kile ambacho tunakubaliana kukifanya wenzetu wakakifanye hakifanywi vile ambayo tumekubaliana kikafanywe. Hiyo ni *problem* ya *credibility* ya mpango na bajeti yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la tatu, limezungumzwa kidogo na Mheshimiwa Bashe, tuna tatizo kwenye *exports*. Mwaka 2016 tuli-*export* bidhaa za dola za Kimarekani bilioni 9.8, kwa mujibu wa taarifa ya Serikali yenyewe. Sasa hivi kwa taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri Mpango ametuletea leo *exports* zetu zime-*drop* kwa dola bilioni moja. Tayari mwezi wa Agosti tumepata *negative balance of payment for the first time in the last three years*. Sekta ambazo zimekuwa zikituokoa hasa mwaka jana ni tatu, utalii, *transit trade* bandarini pale na korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana korosho zimetuingizia fedha za kigeni zaidi ya kahawa, pamba, chai, tumbaku, karafuu, pareto, katani *combined*. Mwaka huu *production* inashuka sana, kwa hiyo tunakwenda kwenye *balance of payment crisis*. Serikali inafahamu hatuendi huku kwa sababu ya bahati mbaya labda *natural calamities* au nini, tunakwenda huko kwa sababu ya kwanza mipango mibovu lakini pili utekelezaji mbovu wa mipango hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitarajia leo tungeweza kuletewa kwamba tunaenda kwenye *crisis* maana mafuta yanaenda kupanda bei na Mheshimiwa Waziri Mpango anafahamu sasa hivi tuta-*import* sana kwa sababu ya miradi mikubwa ambayo tunaitekeleza. Tuna-*import* mataruma ya reli, aibu lakini ndiyo hivyo tuna *import*. Maana yake ni kwamba *by* Desemba tunaweza tukawa na *crisis* kubwa ya *balance of payment*. Ni nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha tunaongeza huo uzalishaji? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imezungumzia katika utekelezaji wa mwaka huu suala la *ASDP II*. Katika *ASDP II* kuna suala la mbegu za *GMO*, mbegu ambazo sote tunajua zinakwenda kuielekeza nchi yetu kuwa koloni la kampuni kubwa za mbegu duniani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nita-*share* na Mheshimiwa Waziri wa Fedha barua ambayo mtafiti mmoja wa Kitanzania amefanya, anaitwa Dkt. Richard Mbunda ambaye aliandika barua kwa Mheshimiwa Rais kuhusiana na suala hili kwamba tunaenda kuua mbegu za asili, tunaenda kuwaua wakulima wadogo, tunajikuta sisi kazi yetu ni ku-*import* mbegu kutoka kwa Monsanto na kampuni kubwa za mbegu na hatimaye ule uhuru wetu wa chakula (*food sovereignty*) tunakwenda kuiondoa. Napenda tupate kauli ya Serikali hasa sera yetu kwenye *GMO* ni nini, tunakubali kwenda kujinyonga na kuwa nchi ambayo inategemea kampuni kubwa kuleta mbegu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni jambo ambalo napenda Wizara ya Fedha ilitazame vizuri. Tuna tatizo la *reporting accounting*, nitaliandika vizuri kwenye mchago wa maandishi. Ukitazama taarifa ya Serikali ya sasa hivi tunarudi kwenye lile tatizo la 1.5 trilioni tena. Ukitazama kwenye *report* ambayo Serikali imetoa, *page* 10 na *page* 11 utaona taarifa ya mapato ambayo Serikali ime-*report* kuwa imeyakusanya mpaka mwezi Juni na taarifa ya matumizi ambayo Serikali imesema imetoa fedha hizo kwenda kwenye mafungu, kuna tofauti ya shilingi trilioni 2.1. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, ukitazama hotuba ya Mheshimiwa Waziri ya mwaka 2017, kama ingekuwa imezingatiwa hii na *Treasury* tatizo ninalolizungumza sasa ambalo *PAC* wanalifanyia kazi la 1.5 trilioni lisengekuwepo kwa sababu wali-*report* sahihi vile ambavyo wamekusanya na vile ambavyo wametoa, wakatazame ukurasa wa 11 na 12. *CAG* baadaye alionyesha kwamba kilichokuja kuripotiwa kuna hiyo tofauti ya 1.5 trilioni; sasa hivi 2018 tatizo limejirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kusema kwamba kuna wizi, namjua Mheshimiwa Dkt. Mpango si mwizi na sisi watu wa Kigoma hatuna historia ya wizi lakini kuna tatizo kubwa la *accounting*. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, kengele ya pili.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mpango unatakiwa uje utoe shule kwa Mheshimiwa Zitto na wengine kuhusu hii *disparate* ambayo inatokea hiyo ya 1.5 siji 2 *point* ngapi, mara nyingi siku zote hivyo vitu havi-*balance* Mheshimiwa Zitto, hukukutana nacho kule shuleni? (*Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba niseme tu kwamba kwa mara ya kwanza nasimama kwenye Bunge lako Tukufu kuchangia nikiwa mtu huru sana. *I will speak out my mind*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la kwanza ni kwamba unajua *life is real*, kuna maisha halisi na kuna maisha ya

kuigiza. Kwa hiyo, kwenye mijadala humu Bunge, Mheshimiwa Mpango na Serikali wajue kwamba kuna watu wanazungumzia maisha ya watu na kuna watu wanazungumzia maisha yao. Wale waliopewa dhamana hiyo ya kuzungumza mambo ya Watanzania, wanyonge, maskini wafanye hivyo, wasikilize kidogo wa-*base* kwenye mambo ambayo wameamua wao ambao ndiyo mkataba kati yao na Watanzania walio wengi, hili ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo naunga mkono miradi yote ambayo imetajwa hapo ya kimkakati, ujenzi wa reli, Shirika la Ndege na umeme wa maji wa Rufiji. Ni muhimu watu wajue kwamba haya yote, kujenga reli, kuliboresha shirika la ndege na umeme wa maji ya Rufiji wala hauhitaji Katiba Mpya. Kwa hiyo, haya yatekelezwe mapema, wale ambao wanasubiri Katiba Mpya watafanya watakapopata Katiba Mpya, kwa sasa haya yafanyike, huhitaji Katiba Mpya katika kutekeleza haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko suala la maji. Wenzangu walipokuwa wanazungumza, maana leo nimepata uzoefu mpya kabisa, mimi ni Mwalimu, yaani ni kama ulikuwa unawafundisha wanafunzi halafu unampa mmojawapo swali halafu unakaa unamsikiliza, nimewa-*enjoy* sana ndugu zangu wale watasubiri kweli, watasubiri sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mchangiaji mmoja anasema kuna mradi wa maji kule Njombe haujakamilika au umekamilika lakini hautoi maji lakini anasema hatua hazikuchuliwa. Mwingine anasema watu hawana amani, watu wana vinyongo yaani wana hofu hofu. Kwa nini mtumishi wa umma, kama ni Mkuu wa Idara ya Maji, Injinia wa Maji una hofu wakati ni mtaalam na umepewa dhamana katika eneo lako? Unasema mradi umekamilika lakini hautoi maji, huyo ambaye amekula pesa awajibishwe na hapo ndiyo inakuja dhana ya kutumbuana, hHuyu hawezi kuonewa huruma. Kama tunazungumza habari ya maji hayapatikani lazima miradi ya maji ikamilike na wale ambao hawakutimiza

wajibu wao wawajibishwe na hiyo ndiyo kazi ya Serikali ya Awamu ya Tano, naunga mkono jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la maji likifanyika nchi nzima, kila jimbo, kila wilaya, kila mkoa maana yake habari ya upinzani haitasikika, watu wataimba CCM wataimba Magufuli, wataimba Majaliwa, wataimba Ndugai, hakuna mjadala, watu wanataka maji hawataki Katiba Mpya. Nani ameitisha mkutano watu wakawaambia alete Bungeni suala la Katiba Mpya, watu wanataka maji, barabara...

**MWENYEKITI:** Rafiki zangu msikilize vizuri. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo maneno ya Katiba Mpya ni yao, wananchi kule mtaani wanataka waondolewe kero zao. Hiyo ndiyo kazi Mheshimiwa Magufuli anayoifanya na sisi tunamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwamba kule Ukonga kuna shida ya majia miradi inaendelea na kwenye mpango huu imetajwa katika Mkoa wa Dar es Salaam kuondoa kero ya maji ikiwepo Jimbo la Ukonga, Temeke, Kigamboni na Ubungo. Hata na Majimbo mengine kule ambayo wenzangu wapo, akina Mheshimiwa Mnyika na wengine na CCM kwa kweli pale haijabagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu. Kuna mwenzangu mmoja hapa amesimama akasema hakuna ajira, mimi nilikuwa naangalia kwenye mtandao wa ajira. Kwa mfano Serikali imekarabati Shule Kongwe za Jangwani, Azania, Pugu, Kilakala, Vyu vya Ualimu, Tarime TCC, Mbeya kule Mpuguso, hii kazi imefanyika na mabilion ya fedha zimetumika. Tunapozungumza kuna walimu wapya wa sekondari wameajiriwa zaidi ya 4,800 wa hesabu na masomo ya sayansi. Kuna nyumba za walimu zimejengwa, maabara, hosteli za wasichana, kule kwangu Mbondole imejengwa. Haya mambo lazima ukubali na upongeze kidogo. Sisi wengi



hapa ni Wakristo hasa upande ule unatakiwa ushukuru hata kwa kidogo. Kuipongeza Serikali ni kuipa moyo kwamba hapa umetatua kero hii lakini bado kuna hili na lile si dhambi. Sasa ukikaa hapa unajadili habari ya kupongeza inaonekana siyo sawasawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu. Elimu, kwa maana ya shule ya elimu ya awali, shule za msingi na sekondari Serikali imefanya vizuri sana baada ya kuondoa ada na kutoa ile elimu bure. Sasa kuna vyuo vya ufundi na teknolojia, kuna vyuo vya elimu ya juu, hapa inabidi Serikali iweke nguzo. Unapozungumza habari ya ajira, ukiwa na vyuo maana yake ni kwamba utapata vijana wengi wakimaliza *form four, form six*, watakuwa na ujuzi watajiajiri hawatasubiri ajira ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lazima Serikali ichukue hatua. Kuna mchिंगiaji mmoja jana amesema kwamba mikopo ya elimu ya juu itolewe na benki, benki haiwezi, hawa ni vijana wamemaliza shule hawana kazi, wanakaa mtaani muda mrefu. Kwa hiyo, lazima Serikali yenyewe ichukue wajibu wa kusomesha Watanzania watoto wa maskini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vya mikopo ya elimu ya juu, naipongeza sana Serikali kwa sababu wakati nikiwa Rais wa Mlimani 2005/2006 tulikuwa tunagoma ndipo unapata mkopo. *This time around* vijana wanakaa kwenye mabweni yao, fedha zinaingia, wanaenda kwenye mitandao Serikali imefanya kazi kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, cha muhimu vigezo viangaliwe habari ya kuambiwa tu kwama baba yake alikuwa mtumishi amestaafu amesoma *private* sasa hawezi kupata mkopo siyo sawasawa. Mimi hapa ni Mbunge na wenzangu kesho nikistaafu maana yake kipato hiki hakipo, mwanangu atakosa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani vigezo viangaliwe na hali halisi ya mazingira kulingana na wakati.

Suala la kuwasomesha vijana wa Tanzania, ni jambo mahsusi, ni jambo maalum lisimamiwe na litekelezwe. Watoto ambao wamefaulu kwenda vyuo vikuu wasibaki mitaani hawasomi itakuwa si sawa, hilo tunaliunga mkono lifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya. Kuna mtu jana anasema kwa nini mnazungumza habari ya vifaa tiba. Tukubaliane kuwa wakati tunapanga kupunguza maradhi ya aina mbalimbali katika hii nchi ni lazima pia haya yaliyopo tuyatibu na kujipanga vizuri, hili jambo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia takwimu, kwa mfano wamejenga nyumba za madaktari 313, vituo vya afya 350, zahanati mpya 38, hospitali za wilaya 221 na Kivule Ukonga ipo na Bunda kule kwa Mheshimiwa Ester Bulaya ipo, imetajwa hapa na fedha zimepelekwa. Sasa katika eneo hili lazima tukubali kwamba kazi inafanyika kubwa, tuunge mkono wenzetu lakini tuboreshe namna ya kwenda mbele, hilo ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo la vijana, wanawake na walemavu...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika muda ambao nimekaa na Mheshimiwa Mwita Waitara humu Bungeni, sijawahi kuona akichangia vizuri kama safari hii. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Yuko huru.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba *life is real* na niko kwenye maisha halisi, nimerudi kwenye enzi zangu na *I will speak out my mind throughout this Bunge*, kwa hiyo hakuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itajitahidi, kuna suala la vijana, akina mama na walemavu, zile asilimia nne kwa akina mama, nne kwa vijana na mbili kwa walemavu, changamoto kubwa ni kwamba mahitaji ni makubwa kuliko

uwezo uliopo na halmashauri zetu hazina uwezo kwa kuwa zina shughuli nyingi sana. Serikali iangalie namna ya kupata fedha iwezeshe makundi haya maalum, hawa ndiyo wapiga kura na ndiyo Watanzania. Hawa akina mama, vijana na walemavu wakiwezesha watapungaza utegemezi, wakienda kupiga kura wataiunga mkono Serikali kwani imewawezesha. Hili lifanyiwe kazi haraka sana na halihitaji Katiba Mpya, linahitaji utashi na maamuzi na fedha itafutwe ifanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora, hapa nina maneno kidogo. Kuna watu hapa wamesimama mtu anaita mkutano wa hadhara anatukana mwanzo mpaka mwisho, akikamatwa anasema ameonewa, nani kamtuma akatukane watu kwenye mkutano wa hadhara? Ameita waandishi wa habari anasema watu wameuawa, sisi tunakwambia tusaidie uthibitisha waliouawa unasema unaonewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanazungumza utawala bora, tarehe 4 Novemba, Kambi Rasmi ya Upinzani ya CHADEMA walikutana maana wana urafiki wa mashaka kati yao na CUF walikutana. Yuko Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Nyarandu, yuko na mwingine wanapanga namna ambavyo Bunge hili, yaani kikao chako hiki Mheshimiwa Mwenyekiti kitavurugwa na maazimio yao wanapanga hata kwenda nje ...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Sasa kama mnakubaliana, mnapanga namna ya kuvuruga mahusiano ya kimataifa na mnamtuma Nyalandu aende, halafu hapa mnatuambia habari za utawala bora, mnataka mwongozo wa Spika; nakushukuru Mwenyekiti kwa kupiga chini taarifa zisizo na maana hawawezi kutuingiza huko...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru. Unapozungumza habari utawala bora ni lazima uanzie ndani. Ni muhimu sana na lazima tukubaliane.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Zitto, naomba utulie utapata nafasi yako. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Naomba tumsikilize Mjumbe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu anavunja Kanuni.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavunja Kanuni.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Waheshimiwa Wabunge naomba mnisikilize, nachosema hapa hoja yangu ya msingi...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavunja kanuni, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...hatuwezi kuwa na Watanzania wanakutana kwenye magenge yao, wanapanga kuvuruga amani ya nchi, wanapanga kuvuruga mahusiano, halafu wanakuja Bungeni ili tupoteza muda kujadili mambo yao. Wamepanga wao, wamejadili wao, watupoteze muda, hatuwezi kuruhusu mjadala ukafanyika humu ndani. (*Makofi/Vigelele*)

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo tunamuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni namna ambavyo anaweza kuchukua hatua kwa watu ambao wamefuja mali za nchi.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kama kuna watu wanafanya biashara hawafuati utaratibu, hawalipi kodi wamevuruga miradi wakikamatwa wanasema hawana amani, wahalifu lazima washughulikiwe, hata Mwalimu Nyerere alifanya hivyo. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Arusha lilikuja kuwawajibisha watu ambao ni wazembe, sasa Mheshimiwa Dkt. Magufuli amewaelekeza watendaji wenzake na hili linahusu ma-DC na Wakuu wa Mikoa.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Mbunge ni tofauti na kazi ya DC na RC, wale ni *executive*, kama kuna mahali kuna mradi haujafanyika mtu amesimamia jengo limekuwa hovy hovy anakamatwa anaisaidia Serikali ili kazi ifanyike.

**MBUNGE FULANI:** Piga, piga.

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, ahsante sana muda wako umeisha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kwa hiyo, nidhamu ni muhimu sana.

**MHE. KABWE Z.R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara.

**WABUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais amefanya ziara kule Nyamongo, amesema wananchi watalipwa fedha zao za muda mrefu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara inatosha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Sasa yameshughulikiwa wananchi wanaishi kwa amani. Mheshimiwa Dkt. Kigwangala nenda ukashughulikie mambo haya msingi yaishe. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho...

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na kwa mara ya kwanza katika historia ya Bunge, naomba niunge mkono hoja kwa nguvu zote asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Naomba nikutunze.

**MBUNGE FULANI:** Uuu, uuu, uuu.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu linaongozwa na Kanuni nawe hapo mwanzo wakati Mheshimiwa Mwambalasa anazungumza umetu-*guide* kuhakikisha kwamba tunajadili mambo ambayo yamo ndani ya mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a) inatuelekeza Wabunge kutotoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Kipengele (b) kinasema, Mbunge hatuzungumzia jambo ambalo halipo kwenye mjadala na (g) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge aliyetoka kuzungumza sasa hivi sijui anaitwa nani na sijui anatoka Jimbo gani...*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge huyo amezungumza mambo ambayo mimi naamini hayana ukweli na anapaswa kulithibitishia Bunge. Hao Wabunge aliowataja walikaa wapi na lini kupanga hicho kinachoitwa kuvuruga shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu linahusu heshima ya watu. Unazungumza Wabunge, unamzungumzia Kiongozi wa Upinzani Bungeni, unamzungumzia Mbunge *senior* na ambaye amemfundisha yeye kazi ya Ubunge. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina wasiwasi sana kwamba ukihama chama ukatoka Upinzani ukaenda Chama cha Mapinduzi akili yako inabadilika kidogo. (Makofi/Vigelegele/Kicheko) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, maneno yako ya mwisho nayafuta kwenye *Hansard*...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ni maneno ya kuudhi yameenda kinyume kabisa na ulipoanzia.

Tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi.



**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi. Mara nyingi huwa na-avoid kuwa mtu wa vijembe, lakini kuna wakati mwingine inabidi kunogesha na nitanogesha kama ifuatavyo...

**MBUNGE FULANI:** Nogesha tu!

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajuwa mtoto aliyebemendwa akapata mtu akampa lishe matokeo yake unayaona, sasa haya mambo ya Waitara. Ukishaenda kwenye lishe unaweza ukapata picha. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kunogesha, kwanza kabisa...

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa .

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtaharibu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Naomba nitoe taarifa.

**MWENYEKITI:** Mambo madogo madogo mvumilie tu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Naomba nitoe taarifa tu.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana ndiyo anaanza tu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nataka nimpe taarifa juu ya maneno aliyoyaongea, neno kubemendwa ni matusi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe kaa, endelea Mheshimiwa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuendelea tena na vijembe inatoshwa, nisije nikaharibu hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuanza kwa mambo mawili. Kuna mtu anaitwa Beno Kakolanya na kuna mtu anaitwa Cletus Chota Chama au sisi watu wa Simba tunamwita *triple C*, kwamba mtu anapofanya jambo jema anastahili kupongezwa, wala si dhambi kupongeza. Ndiyo maana mashabiki na wapenzi wa Yanga na hata wa Simba siku ya Simba na Yanga tulimpongeza Beno Kakolanya kwa sababu aliokoa magoli mengi ya wazi. Ndiyo maana hata wapenzi wa mashabiki wa Yanga wanampenda na kumpongeza Cletus Chota Chama kwa kwa sababu anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi, nakubaliana na wewe na mimi nilikuwa mgeni rasmi siku ile kwa kweli Yanga waliponea tundu la sindano. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Kuna mambo yamefanyika ni wajibu wetu kama Wabunge kupongeza na kuitia moyo Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaenda kwenye mengi nitaenda kwenye afya tu ukurasa wa 30, ukarabati wa hospitali za wilaya 10, vituo vya afya 295 na nyumba za watumishi 306. Kama hiyo haitoshi nikienda ukurasa wa 33 kwenye suala la elimu tumeona ongezeko la watoto kutoka milioni 1.5 mpaka milioni 2 kutokana na elimu bila malipo. Hawa watoto laki tano maana yake ni kwamba wangekosa masomo, wangekosa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hatua hizi tunazopiga kuna tabia inataka izuke katika taifa letu la kuzua taharuki, ni lazima tuikemee. Kuna watu wapo tayari wao kuzua sura ya hofu. Nitatoa mfano, watu wanatoa hoja hapa, hivi mimi kwa mfano kwetu Mafinga familia yangu imemuita mke wangu Mafinga, hivi wewe nyumba ya tatu

unaanza kuperuzi kwa nini ameitwa kwenda mafinga kujadili mambo yao ya familia? Watu wamemuita Balozi wao wanaenda ku-*discuss issue* zao *why do you speculate* wanaenda kujadili nini, uitake Serikali ikuambie eti ameitwa kwa nini? *Thus is none of your business. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hii hali ya kupenda kuzua hofu, jambo dogo tu...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** ...kulikuza na kuleta hofu hofu; na ndiyo maana na mpongeza sana Katibu Mkuu...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa mwenyekiti, taarifa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:**... Dkt. Bashiru katika mdahalo mmoja alipoeleza kuhusu hofu, alisema wenye hofu ni mafisadi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, anaongea uongo.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unafanya kazi zako, unawakilisha wananchi wako kama Chumi hapa, kwa nini usiringe?

Kwa hiyo, lazima sisi kama viongozi tuwe mstari wa mbele kueleza yaliyo mema na kuonesha mstakabali kwa lugha njema na zaidi ya yote sisi kama Bunge kushauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu hapa wamesema hapa *FDI (Foreign Direct Investment)* zimeshuka.

Nataka niwaambie *globally* zimeshuka kwa asilimia 23 siyo sisi tu, kutoka trilioni za Kimarekani 1.37 mpaka trilioni 1.43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Afrika zimeshuka kwa asilimia 21, katika *East Africa* zimeshuka kwa asilimia 25.3 kutoka dola za Kimarekani bilioni 8.8 mpaka bilioni 6.6 na hapa anguko hilo katika East Africa sisi tuna nafuu. Ukienda Kenya ndiyo ime-*record the highest* anguko ni asilimia 60.6 yaani kutoka bilioni 1.8 mpaka dola milioni 717.7, Uganda anguko ni asilimia 14.2 sisi Tanzania asilimia 7 yaani ni Rwanda na Burundi tu ndiyo ambao wamekuwa na afadhali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Rwanda kutoka dola za Kimarekani milioni 600 mpaka dola milioni 1.2, hata Burundi kutoka dola za Kimarekani milioni 65 mpaka dola milioni 146. Kama una akili timamu unaweza kulinganisha dola milioni 186 ambazo zimeingia Burundi na sisi ambao tumeingiza hapa nchini dola bilioni 3.3 kama *FDI*? Kuna nchi zimepongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi si takwimu za Cosato Chumi, nenda kwenye ripoti ya *UNCTAD (United National Conference on Trade and Development), The World Investment Report* ya 2018. Katika *FDI* zilizokuja hapa *East Africa* sisi ndiyo *the highest*. Katika dola bilioni 4 zilizokuja katika *East Africa* sisi tumepata *share* ya 1.2 bilioni FDI, Uganda 0.7 bilioni dola za Kimarekani na Kenya 0.67 bilioni. Kwa hiyo, hata katika East Afrika yaani sisi tume-*attract the highest*. Sasa haya mambo pamoja na mapungufu yake lazima tupongeze halafu tuangalie sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye *Easy of Doing Business* bado hatupo vizuri, maana yake tukiwa vizuri tutavutia zaidi ya hii tumevutia. Kwanza kabla sijaenda kwenye hiyo, hizo *FDI* maana nisiseme tu *FDI* zimeleta nini? Katika *East Africa* sisi zimezalisha ajira zaidi ya 20,000 sawa na asilimia 20 waliotuzidi ni Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nachotaka kushauri, tumesema Bunge kazi yetu ni kushauri, katika ile *Easy of Doing*

*Business Index* sisi tume-*fall*, tupo namba 147 ukilinganisha na Rwanda ambao ni 29 na ni kwa nini tumeanguka? Kuna mambo mengi, Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na jitihada hizi za kujenga mazingira wezeshi, miundombinu, nishati na kadhalika tunalo jambo moja kama Serikali kuchelewa kufanya maamuzi. Kwa hiyo, ni lazima tuambizane ukweli Serikali kuchelewa kufanya maamuzi na kwa wakati ni tatizo. Mtu amepata *work permit Labour* akienda *Immigration* anachelewa kupata *residence permit*. Kuna *contradiction* ya maamuzi katika maeneo mbalimbali ya mamlaka, tukiweza hili maana yake ni kwamba tutavutia uwekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuboresha mazingira tuangalie pia na ndani. Haiwezekani umetoa mbaao Mafinga unapeleka Mwanza unaambiwa usafiri mchana tu ikifika saa 12.00 umesimamishwa, uta-*run* vipi uchumi? Gari kwenda Mwanza inatumia siku nne ingetumia siku mbili au siku moja maana yake kwanza hiyo gari ingejaza mafuta mengi na Serikali ingepata *fuel levy*. Kwa hiyo, haya ndiyo mambo ya kuboresha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kumaliza, lazima nimpongeze Mheshimiwa Kangi Lugola. Hata ukienda nchi za watu kuna maeneo wanafanya biashara saa 24. Huwezi ukazuia biashara za watu saa tano, hivi wewe uende pale Mikumi uwaambie wale akina mama ikifika saa tano wafunge biashara wakati wao biashara yao wanategemea watu ambao wako *on transit*. Uje Mafiga uwaambie kina mama ntilie wafunge biashara saa nne wakati wao *client* wao wanategemea vijana waliotoka msituni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna maeneo tujaribu kuboresha na wala si sheria, ni kanuni ambazo Mawaziri wanaweza wakazirekebisha ile *Easy of Doing Business* ikawa nzuri tukavutia *foreign investment*, tukapata mapato mengi ili huu mpango tukaugharamie ipasavyo kwa sababu tumeona mikopo kutoka nje na misaada haiji kwa ile *pace* tuliyotarajia. Kwa hiyo, kikubwa lazima kitoke ndani,

kitatoka ndani vipi ni kwa kuboresha mazingira ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu awabariki kwa kunisikiliza, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Safi sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Hili la mwisho bwana kwa kweli tunampongeza Mheshimiwa Kangi, yaani ikifika tu saa tano usiku hata hapa Dodoma, yaani nchi nzima kote mlipotoka, ikishafika saa tano usiku polisi wanaanza kupita funga biashara, funga, funga. Sasa mimi huwa najiuliza, haya maneno gani haya? Kwa sababu watu wakifanya biashara Serikali si inapata hela? Sasa Serikali gani haitaki hela eti kwa sababu imefika saa tano usiku? Kwa hiyo, hili tuliangalie kidogo, uchumi lazima uzunguke inasaidia. Hii kusema watu wote lazima tulale saa tano usiku...*(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Salome Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga. Mheshimiwa Salome taratibu. *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla sijaanza kuchangia, naomba Bunge hili lijue mimi ni mjumbe wako wa Kamati ya Kanuni za Bunge na wewe kama Mwenyekiti wangu umenifundisha kweli kweli kuzisoma kanuni hizi na kuzizingatia. Kwa taarifa hiyo, naomba niwakumbushe Wabunge wenzangu kwamba tutumie tu lugha nzuri pale tunapokuwa tunachangia na tusiseme uongo Bungeni, tunamlazimisha Mheshimiwa Spika wakati mwingine kutubeba lakini si jukumu lake, tuwe na busara. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kama Waitara.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa *quotation* ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Hassan Suluhu alipokuwa akiutubia katika sherehe za utoaji za tuzo za heshima, wakati ule alikuwa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais

Mazingira na Muungano. Mama Samia Suluhu alisema yafuatayo, imeandikwa kwa Kiingereza tafsiri nitakayoitoa haitakuwa ya moja kwa moja lakini alisema; *“On the bilateral front the European Union is Tanzania key development partner both in terms of magnitude and financial support”*.

Akaendelea kusema zaidi; *“Let me therefore avail this opportunity to express our sincere gratitude and appreciation for the European Union in valuable assistance which has enabled the Government of Tanzania in many ways undertakes social economic development programs for sustainable development”*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wajomba zangu kama Mheshimiwa Mzee Musukuma, Mama Samia Hassan Suluhu wakati anahutubia mkutano huu...*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuwa anamaanisha kwamba anatambua mchango mkubwa wa wadau wa maendeleo ambao wanatuchangia...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Musukuma tulia, Musukuma tulia. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo. Alikuwa anatambua mchango mkubwa...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** ...wa wadau wakubwa wa maendeleo na na bajeti yetu ya Tanzania. Mama Samia Hassan Suluhu ambaye sasa ni *Vice President* alitambua kabisa kwamba ili tuweze kutengeneza mpango wa maendeleo

unaotekelezeka Tanzania haiwezi kujiendesha kwa pato la ndani peke yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome kulikuwa na taarifa kwa Mheshimiwa Musukuma. *(Makofi/Kicheko)*

## T A A R I F A

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kweli Salome ni mjomba wangu na ninajisikia fahari kunitolea mfano. Sasa sikuelewa mfano ule ulikuwa una maana kwamba sikuwa nasikia alivyokuwa anazungumza Kingereza, lakini niliwa kusema ni bora uka-*declare* kuliko kuwa kama yeye kwa sababu yeye mwenyewe kusoma Kiswahili alishindwa ikabidi aanze halafu akumbuke. nakushukuru. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoniita Salome ameniita kwa Kisukuma, ni mjomba wangu.

**MWENYEKITI:** Wasukuma wanapambana wenyewe kwa wenyewe. *(Kicheko)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia Hassan Suluhu, nikianza kwa kum-*quote* alitambua mchango mkubwa wa wadau wa maendeleo kwenye bajeti yetu akiamini kwamba ili tuweze kufikia malengo ya mipango tunayoitengeneza ni lazima tuheshimu na tuthamini wadau wakubwa wa maendeleo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo hivi sasa katika nchi yetu, mimi naomba nisisitize, kuna hali ya sintofahamu kubwa sana kati ya mahusiano yetu na wadau wetu wa maendeleo. Labda nianze na ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara kama tulivyoahidiwa wataishi kama mashetani wanaishi kama mashetani. Wafanyabiashara hawana *security*. Juzi



tumeshuhudia *billionaire* mdogo Afrika ametekwa, amejirusha mwenyewe, halafu ameenda kuhojiwa akiwa nyumbani kwake na Serikali ipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu pale Shinyanga tunao wafanyabishara wa maduka ya kati. Siku za hivi karibuni kwenye vyombo vya habari, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mlishuhudia, Mkuu wa Mkoa amekwenda pale anafanya operesheni sijui ya ukaguzi, maana operesheni zimeshakuwa nyingi siku kila mtu anafanya; kwenye operesheni ile amefunga kwanza maduka yote ya pale mjini bila kujali athari za kiuchumi za matendo ambayo anayafanya. Kafunga maduka yale, kawachukua wafanyabiasha kaita vyombo vyote vya habari, anawasimamisha mbele ya vyombo vya habari anawaambia wafanyabiashara wale eleza ulichokifanya, haya kiri kwamba ulifanya hivi, haya eleza hivi, kinyume na haki za binadamu, utu, sera ya biashara na sera ya uwekezaji. Ndipo tulipofika kwa sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho na kahawa zinakufa. Mazao yote ya biashara ambayo kimsingi kama walivyoeleza Wabunge wenzangu ndiyo yanayochangia kwa kiasi kikubwa tuweze kutekeleza mpango huu ambao leo tumekaa Dodoma tunaujadili yanakufa lakini *nobody cares*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupe taarifa iliyotokea jana. Jana kwenye *Citizen TV* kwa Wabunge wenzangu ambao mmetazama, wavuvi 36 wa Kenya wamezuiliwa kwenye Ziwa Victoria wakisemekana kwamba ni wavuvi haramu na wamekatwa na watu wa Usalama wanaambiwa hawawezi kuachiwa mpaka walipe faini ya milioni 26. Je, watu wa Usalama wanatoza faini? Uvuvi haramu mamlaka husika zinajulikana lakini sasa ndipo tulipofika leo, tunasema refa wewe, mchezaji wewe, mfunga goli wewe, mtu mmoja anafaya kila kitu na niliwahi kusema humu ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka kusema asubuhi habari ya watu ambao ni watetezi wa waandishi wa habari Tanzania. Kuna sintofahamu kubwa, watu wamekuwa *detained* hotelini wamenyang'anywa *passport*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema leo Serikali itoe kauli kukemea vitendo hivi ambavyo vinaweza kutuingiza kwenye migogoro ya kidiplomasia, hatuelewani humu ndani. Mpaka natamani neno diplomasia lingetafutiwa neno lingine labda ni msamiati mgumu ambao viongozi wa Serikali hawaelewi. Wale watu wamekuwa *detained* BBC na CNN wame-report. Hivi inaleta *image* gani kwa nchi yangu leo kudhalilika namna hiyo kimataifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mahiga alitoa *statement* baada ya Balozi wa EU kuondoka, akasema eti ameondoka kwa anavyojua mwenyewe, amepangiwa kazi nyingine sisi hatuwezi kujua. Hata hivyo, Balozi wa EU ametoa *statement* kwenye tovuti yake, anasema kuwa alifanya na mazungumzo na Serikali ya Tanzania na akaeleza *grievances* zake kwamba Tanzania hawaelewani na EU kwa sababu kuna uvunjifu mkubwa haki za bidanamu, Tanzania kuna shida kubwa ya utawala wa sheria, ameeleza *black and white*. Alikuwa akafanya mazungumzo mpaka anaondoka *nobody cares*. Serikali, Waziri mkongwe mdiplomasia ninayemuamini anatoka *public* anasema ameenda kupangiwa kazi nyingine mimi sijui bwana, inawezekana tukaletewa mtu mwingine, *recalling of an Ambassador is not a joke...*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Inaharibu *image* ya nchi...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama leo hapa kutaka kukuonyesha kwamba hawa *European Union* inachangia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Naam!

**MWENYEKITI:** Naona umeamua kuwa Balozi wa Ulaya, maana Balozi hakuna. Mheshimiwa Mlinga, una neno?

### T A A R I F A

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nina neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Salome Makamba kuwa wale waandishi waliokamatwa walikamatawa kwa sababu walikiuka mashari ya *visa, visa* yao ilikuwa ya matembezi lakini wale walikuwa wanafanya mikutano na wanahabari. Kwa hiyo, walishikiliwa ili kuhojiwa kwa nini walikiuka masharti ya *visa*. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe Watanzania wenzangu kwamba leo tunapozungumza hapa ndani kwenye kwa Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka huu 2018, *European Union* yenye nchi 27,28 imechangia kwenye kahawa dola milioni 149. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salome Mkamba, tunakushuru kwa mchango wako. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mayenga, sasa hivi naenda na Wasukuma tu basi. (*Kicheko*)

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipatia nafasi hii walau na mimi niweze kutoa mawazo yangu kwenye mpango huu ambao umeletwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa mpango huu mzuri. Naomba kumpa moyo sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake. Haya maneno mengine ambayo yanasemwa uyazoe tu kwa sababu leo wanasema, kesho wanasifia, ndivyo walivyo baadhi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda nimpongeze sana kwa nafasi ya kipekee Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtendaji mkuu, ni kiongozi wa shughuli za Serikali ndani ya Bunge. Anafanya kazi nzuri sana, anafanya kazi kubwa sana na mimi napenda sana *style* ambayo huwa inakuwa ya kimya kimya, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa leo tunajadili mpango lakini yapo mambo ambayo mbele huko tunaona mwanga mkubwa sana na wa kijani. Hata hivyo, mafanikio haya yatakamilika endapo na sisi wenyewe kama Taifa tutakaa katika mstari na kufanya yale mambo ambayo kweli tunajua kabisa yatatufikisha kule tunapotaka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Mipango ambayo tumekuwa tunajiwekea kuanzia 2011 - 2016 na Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2020-2025, tumekuwa tunajinasibu na tunasema kwamba tunataka tuwe Taifa la uchumi wa katika *by* 2020-2025. Hata hivyo, mimi nikiwa mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara ninajiuliza jambo moja, hivi kweli tupo tayari? Ninajiuliza hivi kweli Serikali ipo pamoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu sioni *inter-connection* kati ya Wizara na Wizara. Kuna tatizo kubwa sana kwamba tumejinasibu sasa hivi kwamba

tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda lakini ukiangalia Wizara hii inafanya jambo pekee yake na hii inafanya jambo pekee yake. Kwa utaratibu huu hatuwezi kufikia malengo na matokeo yake viongozi hawa wakubwa, Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu tutakuwa tunawapa kazi kubwa sana, watakuwa kama vile ni Mawaziri wa Wizira zote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano moja, kuna Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), mimi mpaka nawaonea huruma wale watendaji wa TIC kwa sababu yapo mambo ambayo yanatakiwa kufanywa na Serikali. Jamani, tunajinasibu kwamba tuwe na uchumi wa viwanda lakini tunashughulikia yale matatizo ambayo tunaona kabisa kwamba yanatukwamisha huko ambako tunataka kwenda? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee to mfano, TIC iko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa heshima kubwa itolewe chini ya Wizara hii. Kwenye nchi za wenzetu ambazo zimeendelea kituo hiki huwa kinakuwa chini ya Ofisi ya Rais au Ofisi Waziri Mkuu. Zamani kituo hiki kilikuwa chini ya Ofisi ya Rais, baadaye kikatolewa kikapelekewa chini ya Ofisi ya Waziri lakini baadaye kimepelekwa chini ya Wizara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watu kazi yao ni kuratibu mamlaka zote za Serikali kwenye masuala yote yanayohusu uwekezaji. Hata hivyo, kama tunavyojua watendaji tulio nao Serikalini ni kweli wana mawazo yale ya uwekezaji? Zipo sheria kwa mfano Sheria za Uhamiaji mwekezaji akiwa ametoka nje ameingia hapa Tanzania ameleta mtaji wake mkubwa anakuja kuwekeza sheria inasema akiwa mwekezaji mkubwa kwa *class A* atapata kibali cha kuishi hapa kwa kipindi cha miaka 10. Akiwa kama ni mfanyakazi, labda ni mtaalam anapewe kibali cha miaka miwili, lakini kibali cha Uhamiaji kile cha ukaazi wa hapa, anatakiwa arudi kule kwao aje *a-apply* tena miaka miwili mingine baadaye tena arudi kwao aje *apply* mwaka mmoja. Hivi kweli mtu anakuja kuwekeza pesa zake nyingi,

hii haipo sawasawa hata kidogo. Mimi nimekuja kuleta pesa zangu halafu ninyi mnaanza kuniambia eti kibali kikiisha inabidi uondoke, mbona ni vitu vidogo vidogo! Hawa watu ambao wapo kwenye Serikali kwa nini hawashughulikii vitu kama hivi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni Sheria ya Kazi. Wote tunajua kwamba kama wewe ni mwekezaji umekuja hapa Tanzania maana yake ni kwamba unataka kuleta wataalam. Hata kama mimi Lucy Mayenga nataka kufungua ofisi, nataka nitafute mtaalam toka nje, nikimtafuta yule mtu kuja kumleta hapa, kwanza lazima tukubaliane kwa mfanyabiashara au kwa mwekezaji yeyote suala la kumleta mtaalam kutoka nje si kwamba wanapenda sana wakati mwingine ni kutokana na mazingira. Ndiyo maana nimefurahi sana kwamba michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge wanasema tuongeze uwekezaji na tuongeze usimamizi mkuu kwenye mafunzo ya ufundi. Hawa watu wakati mwingine wanaleta mtu si kwa maana pengine labda hapa anaweza kukosa mtu lakini sisi tunajali sana masuala ya vyeti na elimu za makaratasi, wenzetu wakati mwingine wanajali pia uzoefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta Sheria ya Kazi mtu amekuja hapa kama mwekezaji lakini wakati huo huo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha ujaribu kuliangalia hili na uzuri Mheshimiwa Prof. Ndalichako, Waziri ambaye namwamini sana, naomba ulifanyie kazi jambo hili, vibali vya walimu wa *international schools* ambao wanatoka nje naomba Serikali ianze kuangalia sasa hivi havipo katika utaratibu ambao unaeleweka. Sasa mwekezaji amekuja mnamwambia karibu lakini hajui ampeleke mtoto wake shule ipi? Wenzetu hawa wanajali sana familia, hicho tu peke yake kinaweza kikamfanya akasema siwezi kukaa hapa kwa sababu elimu ya watoto wangu haipo sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Ardhi huko ndiyo kabisa! Mtu anakuja kama mwekezaji kutafuta eneo kwa ajili ya kuwekeza inamchukua takribani mwezi mzima

wanazunguka tu kwa kuwa hatuna *data base* ya ardhi kwa ajili ya uwekazaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingine ni Sheria za Kodi. Ni lazima kama Taifa tuwe *predictable*. Haiwezekani kila mwaka tukikaa hapa tunakuwa na *Public Finance Act*, leo tunabadilisha hili, kesho linakaa hivi. Mwekezaji na mfanyabiashara yoyote anataka kuwa na uhakika na kodi anayolipa kwamba leo nalipa kodi hii, kesho nalipa hii, kesho kutwa nalipa hii siyo kwamba leo analipa hii lakini hajui kesho atalipa nini, ni vitu vigumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba kama Taifa na sisi kama Wabunge tukubaliane jambo moja, kuwa Mzungu au mtu anayetoka nje aidha ni Balozi au ni Mzungu mtaalam wa jambo lolote umekuja hapa tuheshimiane, hii ni nchi huru. Naiomba sana Serikali, mtu yeyote ambaye atakuja hapa akienda kinyume na utaratibu wa Taifa letu aondolewe saa 24. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kusema kwamba eti kwa sababu ni Mzungu, eti kwa sababu ni hivi, tunataka wale ambao watakuja wawe na malengo mema na sisi. Wawe na malengo mema kwamba mtu anakuja anasaidia, ni mdau kweli wa maendeleo. Siyo mtu anakuja anapiga blabla, mara anakwenda chini kwa chini anafanya mambo mengine, wengine wanajiingiza kwenye mambo ya siasa, tutakufukuza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wangu, ni Rais ambaye kwa nafasi ya kipekee na naomba kwenye hili baadhi ya Mawaziri tuweze kukaa na kutega masikio yetu vizuri kuhusu utendaji wa Mheshimiwa Rais wetu. Wizara jamani acheni mambo ya kupeleka matatizo ya ndani ya Wizara zenu kwa Mheshimiwa Rais yashughulikieni ninyi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Yaani nyie mnamchokoza Mheshimiwa Lucy kwa sababu kamaliza? Naweza kumpa dakika nyingine, si mnamfahamu au mmemsaheu? *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Mpeeee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Mayenga wanakutania hawa wamesahau.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Gerson Lwenge atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia machache kwenye mwongozo wa mpango wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam kwa kutuletea mapendekezo ya mpango. Tunapata nafasi ya kuchangia kwa sababu kuna kitu kilicholetwa. Kwa hiyo, nawapongeza, mmeleta maeneo mengi ambayo manafikiria kwamba tukiyatekeleza haya yatakwenda kujibu haja ya wakulima na wafanyabiashara wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango mzuri ni ule ambao hautaleti manung'uniko kwa wananchi. Tunasema kwamba uchumi unakua na pia wananchi wetu wameweza kuzalisha chakula cha kutosha ndiyo maana nchi inakuwa na amani, kama kuna njaa nchi haiwezi kuwa na amani. Pamoja na kuwa na hali hiyo ni vizuri tuangalie hawa wakulima ambao wametufikisha katika hali ya kuwa na utulivu, maana wanalima, hasa wakulima wa mahindi, wamelima miaka miwili mfululizo lakini hakuna anayewasemea wapi watauza mahindi yale na ndio maana kuna hii ziada. Kwa hiyo, mpango huu tunaoutengeneza ni lazima uende kujibu kwamba sasa mazao yao yatanunuliwa kama



tunavyozungumzia mazao mengine ya biashara, hilo lilikuwa la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mapendekezo ambayo nafikiria ni kwamba ili mpango huu uweze kutekelezwa ni lazima tuone ni namna gani tutaongeza ukusanyaji wa mapato. Katika mapendekezo yaliyoletwa ni kwamba mwakani tunatarajia tukusanye shilingi bilioni 23, kwa maana ya TRA pamoja na Halmashauri zetu, sasa hii mradi ambayo tumeshaweka mikataba ni lazima tuhakikishe kwamba mikataba ambayo imeshasainiwa tunaitafutia fedha zake tuweze kutekeleza. Sehemu kubwa ya fedha hizi, kama alivyo sema, zinatokana na mapato ya ndani. Kama hatuna mikakati mizuri ya kupata fedha hizi tutakuwa tunaingia mikataba halafu tunashindwa kulipa mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi tumeingia mkataba kwa mfano miradi ya umeme kupeleka vijiji 555, ni jambo zuri lakini haiendi kwa kasi kwa sababu wakandarasi wale hawalipwi ama hawalipwi kwa wakati. Tumeingia miradi mingi kwenye upande wa maji wakandarasi wengi kwenye miradi mingi hawalipwi *certificate* zao. Kama tunakuwa na mpango mzuri lakini hatuwezi kuwa tunawalipa wakandarasi mwisho wake inakuwa kwamba hatujibu haja ya wale wananchi kwamba wanapata maji na huduma nyingine ambazo zinatarajiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba katika miradi ya kipaumbele ambayo ameielezea kwenye ukurasa wa 34, iko kama 14 lakini nafikiri tuibadilishe. Mawazo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni mengi, tuwe na namna ya kuweza kubadilisha vipaumbele vilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kipaumbele cha kwanza ambacho wananchi wetu wanategemea sana ni ile miradi ambayo tuliwahamasisha wananchi wachangie nguvu zao kujenga zahanati, madarasa na maabara, ni miaka saba Serikali haijapeleka fedha. Nadhani hiki ndiyo kiwe kipaumbele cha kwanza ili wananchi hawa waone kweli tunatengeneza mpango ambao wananchi

wanaukubali pamoja na kulipa madai ya kazi ambazo zimeshafanyika hasa za wakandarasi na yale madeni ya ndani, hiki kingekuwa kipaumbele cha kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha pili, katika miradi ile 14 nafikiri mradi wa kwanza ungekuwa wa kujenga Liganga na Mchuchuma, kingekuwa ndiyo kipaumbele chetu katika fedha tutakazokuwa tumezipata. Tumezungumza mradi zaidi ya miaka mitano lakini hatuoni hatua zinazoelezeka kwa wananchi kwamba Serikali inafanya nini. Tunazungumza miaka yote, hivi kuna tatizo gani mradi wa Liganga na Mchuchuma hauwezi kutekelezwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tunataka Tanzania ya Viwanda, hatuwezi kuwa na viwanda bila kuwa na chuma chetu. Kwa hiyo, nafikiri mradi huu uchukue nafasi ya kwanza katika ile miradi mingine ya kielelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, miradi ile ambayo tayari Serikali imeshaweka mkataba, tunaipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa Reli ya Kati kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma tayari mikataba imesainiwa, fedha zake zile lazima tuzitenge. Isifike mahali wale wakandarasi wanasimama kwa sababu hawalipwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Mradi wa *Stigler's Gorge*, mkataba umeshawekwa fedha yake iwepo katika mpango huu. Pia na miradi ya *REA* nayo ni muhimu fedha zake ziwepo tuwe na uhakika. Ile mikataba ambayo imeshasainiwa fedha ziwepo. Viwanda vinavyohusiana na kilimo vipewe kipaumbele cha kwanza kwa sababu hizo ndizo shughuli ambazo wananchi wengi wanajihusisha na kutakuwa na mzunguko wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua Dodoma kuwa Makao Makuu, sasa Dodoma iwekewe kipaumbele katika miradi ya kuondoa msongamano. Imetajwa Dar es Salaam na Mwanza lakini tuanze na Dodoma maana tusipotengeneza sasa hizo *Flyover* na barabara za mchepuko

tutakuja kuwa na tatizo hapo baadaye. Kwa hiyo, nilifikiri hilo jambo liwekwe kwenye vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu namna ya kupata fedha, ndiyo *TRA* inajitahidi lakini peke yake haitaweza kukusanya mapato tunayohitaji kuweza kutekeleza miradi hii. Kodi za nyumba (*property tax*) mmeamua *TRA* wakusanye lakini kwa ukiritimba wao hawataweza kukusanya kodi hii. Nafikiri Halmashauri zetu za Wilaya zikusanye hii *property tax*. Mheshimiwa Rais, alisema kila nyumba Sh.10,000, ni kitu rahisi kwa wale wa Tawala za Mikoa kukusanya fedha hizi kuliko *TRA*. *TRA* wanakwenda kufanya *valuations* kiasi kwamba mtu hawezi kulipa kodi zile. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais nyumba za kawaida shilingi 10,000 na ghorofa shilingi 50,000, tukikusanya fedha hizi tuna mahali pa kuanzia. Kwa hiyo, nafikiri kwamba Halmashauri wakusanye kwa niaba ya *TRA* ili tuweze kuongeza mapato na kuweza kutekeleza mipango hii tuliyojiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, pamoja na kwamba umeleta mpango mzuri lakini mawazo ya Waheshimiwa Wabunge uyaweke na utakapoleta majumuisho tuone ni jambo lipi ulilolipokea. Maana haya yanayoongelewa miaka yote huwa yanaongelewa lakini tujue ni lipi umelipokea na tuone maboresho ya mpango huu ili uweze kutekelezwa na kukidhi haja ya Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Gerson Lwenge. Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie mapendekezo ya mpango yaliyo mbele yetu. Pia nami niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara hii kwa kutelelea mpango ambao unaonekana kabisa kwamba ni

mwendelezo wa utekelezaji wa mpango wetu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sehemu mbili, ya kwanza itakuwa ni kilimo. Kuna watu ambao wanabeza kwamba hatuwekezi vya kutosha katika kilimo lakini ukiangalia ukurasa wa 29 wa kitabu cha Waziri tunaona kabisa kwamba sekta hii mwaka jana ilipanda kwa asilimia 7.1, hongera sana. Kuna uwekezaji ambao unafanya kwenye sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye mazao ya kimkakati. Tumeona anahangaika na kawaha, chai, mchikichi vile vile amehangaika na tumbaku na pamba kwa kiasi kikubwa sana. Nampongeza kwa sababu jitihada zake kwa kiasi kikubwa zimechangia ongezeko hili la sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma sasa takwimu utakuta zao la korosho ndilo lililochangia zaidi kwenye mafanikio hayo. Kwenye zao la korosho kwa miaka mitatu mfululizo kuna ongezeko la uzalishaji. Mwaka 2015/2016 tulikuwa na tani 155; mwaka 2016/2017 tani 265; na mwaka 2017/2018 kuna tani 315,000. Hili ni ongezeko kubwa na linatokana na uwekezaji mkubwa ambao ulifanywa kwenye zao hili la korosho. Rai yangu kwa Serikali, korosho bado inahitaji uwekezaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado Serikali ina mambo ya kufanya ili kuhakikisha uzalishaji wa korosho unaendelea kuongezeka kama takwimu zinavyoonesha. Kwanza lazima tuwe na mipango sahihi ya kupatikana kwa pembejeo. Tusiachie wafanyabiashara binafsi walete pembejeo ambazo hatuna uhakika na ubora wake na wanawauzia wakulima wetu kwa bei ya juu. Kwa hiyo, Serikali bado kuna kitu inahitajika kufanya ili kuhakikisha zao letu la korosho halishuki kwa uzalishaji kama tunavyoona kwenye takwimu za miaka hiyo mitatu iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye korosho kuna changamoto mwaka huu. Takwimu zinaonesha hadi sasa kwa Mkoa wa Mtwara tu Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala (*TANECU*) wana tani 30,000 na Chama cha Ushirika cha Mtwara, Nanyumbu na Masasi (*MAMCU*) kuna tani takribani 30,000 zimekusanywa lakini hadi sasa ni tani 2,200 zimenunuliwa. Hapa kuna changamoto ya soko la Dunia lakini vilevile mwaka huu kuna *syndicate* ya wanunuzi wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yangu, hawa wanunuzi wamewasilisha barua kuhusu punguzo la kile ambacho Mheshimiwa Rais na nimpongeze anavyosimamia ununuzi wa korosho mwaka huu, kwa sababu amekuwa akifuatilia siku hadi siku nini kinaendelea kwenye soko la korosho. Kwa hiyo, naishauri Serikali yangu ifanye mashauriano na hawa wafanyabiashara, kama kweli madai yao ni ya msingi basi itafutwe mbinu ya kufidia ile Sh.200 ambayo wanaomba wapunguziwe ili waende sokoni wakanunue korosho. Kama madai yao si sahihi basi lile pendekezo au wazo la Mheshimiwa Rais, kwamba korosho zitanunuliwa na Serikali yetu, muda umefika sasa Serikali itoe tamko ili korosho zikanunuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu tuna wiki tatu tu ambazo sisi tuna nafasi ya kuuza korosho ikishafika mwezi Desemba korosho za nchi nyingine zinakuwa tayari na wanunuzi wataenda maeneo mengine. Kwa kuwa Serikali yangu ni sikivu haya watayafanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuondoke hapa nini kifanyike? Tuwekeze kwenye ubanguaji. Siku za nyuma tulifanya kazi kubwa sana ya kuwekeza kwenye viwanda, tuna viwanda 12 vya ubanguaji wa korosho. Viwanda hivi umefika wakati sasa tufanye maamuzi magumu. Wale wanunuzi walionunua viwanda hivyo ambao hawafanyi kazi ya ubanguaji wanyang'anywe viwanda hivyo. Kuna Kiwanda Mtwara, Newala, Masasi, Nachingwea, Mtama, Likombe, Lindi, Kibaha, Tanita I, Tanita II, Newala II na Tunduru. Viwanda

hivi havifanyi kazi ya kubangua korosho, kuna viwanda vingine sasa hivi vinatumika ma-*go-down*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali ifanye maamuzi magumu. Wale ambao wamevichukua viwanda hivi na kuvifanya ma-*go-down*, hawabangui korosho wanyang'anywe ili wapewe wawekezaji wapya ambao wameonyesha nia ya kubangua korosho yetu hapa hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, tutaondokana na tatizo la kupeleka korosho ghafi India ambako kwa njia moja au nyingine wafanyabiashara wa nchi hii huwa wana kawaida ya kupanga bei na hivyo kumdhoofisha mkulima wa zao la korosho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu vilevile naomba nichangie kuhusu eneo maalum la uwekezaji na hasa eneo la Mtwara. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika upanuzi wa Bandari wa Mtwara. Tumeona kuna uwekezaji mkubwa sasa hivi umefanyika kwenye Bandari ya Mtwara na sasa hivi meli za mafuta zimeshaanza kutia nanga na hivyo kurahisisha upatikanaji wa mafuta Kanda ya Kusini Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na hata nchi za jirani Malawi na Msumbiji. Vilevile tunaona kuna ukarabati mkubwa ambao umeanza kwa uwanja wa ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili eneo hili la Mtwara liwe rahisi kuwekeza kuna kazi mbili zimebaki sasa hivi. Kwanza kuna suala la barabara yetu ya uchumi, barabara ya Mtwara-Nanyamba-Tandahimba-Newala-Masasi, km 210. Barabara ile matengenezo yameanza kwa km.50. Tunaomba sasa mpango ujao zitengwe fedha za ujenzi wa barabara kuanzia Mnivata-Newala-Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara nyingine muhimu sana, barabara ya ulinzi ambayo ipo Kusini mwa Tanzania na inaunganisha Wilaya zote na pembeni mwa Mto Ruvuma. Barabara hii haitengewi fedha za kutosha. Tunaomba katika mpango ujao zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo makubwa ya barabara yetu ya

ulinzi kwa ajili kuimarisha ulinzi wa nchi yetu. Kama mnavyofahamu kwamba kule wenzetu Msumbiji kuna nyakati kunakuwa na changamoto za ulinzi, kwa hiyo, barabara yetu iwe inapitika muda wote na vijana wetu wa ulinzi na usalama waweze kuitumia kwa ajili ya kulinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine utajikita kwenye suala la kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu. Kuhusu elimu na ujuzi, hapa lazima tuwekeze vya kutosha. Mpango ujao unatakiwa utenge fedha za kutosha kwa ajili ya sekta ya elimu. Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi ambao ulitekelezwa kuanzia mwaka 2002 kulikuwa na ujenzi mkubwa wa madarasa pamoja na nyumba za walimu, lakini madarasa yale yanahitaji ukarabati mkubwa sana. Wote mtakuwa mashahidi zilitengwa fedha takribani shilingi milioni tatu na laki moja kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha darasa kwa miaka hiyo. Ujenzi uliofanyika kwa wakati ule muda wa kukarabati majengo hayo sasa umeshafika. Naomba mpango ujao utakaowasilishwa zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya elimu ya msingi kama vile vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na ujenzi wa matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, bado kuna suala la motisha kwa walimu. Walimu wetu wanahitaji motisha na kupata mafunzo kazini. Ni mwaka wa tatu sasa mishahara ya walimu na watumishi wengine bado hajaongezwa.

Mimi ninawasemea walimu kwa sababu ni kundi kubwa na ni asilimia 60 ya watumishi wa umma wa nchi hii. Watumishi hawa wakikata tamaa basi kazi zote ambazo tunawekeza katika maeneo mengine hazitakuwa na maana. Kwa hiyo, naomba katika bajeti ijayo tutenge fedha za kuongeza mishahara ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Nawashukuru sana kwa uchangiaji unaoendelea na niwahakikishie wote wale ambao wamejiandikisha kuchangia kwa siku ya leo, watapata nafasi mpaka jioni tutakapomalizia kwa siku ya leo. Niwapongeze, kwa kweli uchangiaji umekuwa mzuri na wenye mawazo mengi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na timu yao yote, tuendelee hivyo.

Basi kwa hatua hii, naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tatu, Kikao chetu cha Tatu, kipindi cha jioni. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa  
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na  
Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya  
Serikali kwa mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, Katibu tena.



**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mkutano wetu. Kama alivyokuwa ameeleza Katibu, sasa ni wakati wa michango mbalimbali na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake wako tayari kuendelea kutusikiliza. Tuanze na Mheshimiwa Kanyasu halafu Mheshimiwa Haonga ajiandae huku nikiendelea kurekebisha orodha yangu. Mheshimiwa Kanyasu tafadhali nimekuona.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuja kusimama tena kwenye Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Naunga mkono pia miradi yote ya kimkakati ambayo Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wameileta. Naomba nitumie nafasi hii kuipongeza pia Serikali yangu kwa miradi yote ambayo imekuwa ikiendelea nchi nzima. Tumekuwa tukiona mambo mazuri yanaendelea kufanyika katika nchi nzima. Naamini kwamba haya yanayoendelea yanatokana na kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali nzima pamoja na Wizara yenyewe ambayo anaisimamia Mheshimiwa Dkt. Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na tatizo dogo ambalo lipo sasa hivi. Wakati tunahamasisha ununuzi wa *EFD* tulikuwa na makampuni mengi ambayo tumeyapa *license* ya kufanya kazi hiyo. Ipo kampuni ilikuwa inauza mashine za Prima, hawa walikuwa wanaitwa *Boston Solution Ltd*, mashine zao zinalalamikiwa kwamba hazifanyi kazi na inasemekana wamevunja mkataba na *TRA* na sasa wale walio na mashine hizo wanaambiwa wanunue mashine nyingine. Kwa hiyo, nataka kupata ufafanuzi kutoka

Mheshimiwa Waziri na pia kuomba suala hili liangaliwe vizuri kwa sababu kama mzabuni amemaliza mkataba halafu mashine zile zinakosa kazi tutakuwa tunawarudisha nyuma wananchi wetu ambao wananunua mashine hizi bei ghali sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze TRA kwa makusanyo mazuri ya kodi. Wameendelea kufanya vizuri na kuwa na lugha nzuri kwa wananchi katika maeneo yetu tunayofanya kazi. Nadhani *speed* ya ku-*recruit new tax payers* ku-*enlarge tax base* imekuwa ndogo kwa sababu tunaweza tukaendelea kukusanya hela nyingi kwa walipa kodi walewale na kama *tax base* haiongezeki basi tatizo letu la kuwa na bajeti finyu litaendelea kuwepo, nadhani hata mwaka jana nilijaribu kusema haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye mpango kwenye Wizara ya Kilimo. Tunajenga viwanda na nilisema mwaka jana, lakini watumiaji wa bidhaa za viwanda zaidi watakuwa ni Watanzania ambao zaidi ya asilimia 70 ni wakulima. Tuna bahati mbaya sana kwamba katika nchi yetu jua likiwaka hasara ni ya mkulima, mvua zikizidi hasara ni ya mkulima, mazao yakipungua na yakizidi pia hasara ni ya mkulima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema kuhusu *Price Stabilization Fund*, bado sioni kama ni *solution* namba moja hiyo peke yake. Nafikiri Wizara na wahusika wajaribu kufanya *market intelligence* kwani yapo maeneo ambayo wakati wakulima wanaingia kwenye kilimo unaweza uka-*forecast* ukaona mwaka huu tutakuwa na mahindi mengi, dengi nyingi na vitu vingi, unajaribu kuwatengenezea wakulima soko mapema kabla ya kwenda kwenye mgogoro huu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye vipaumbele vya kilimo pale, suala la kutafuta masoko kwa maana ya sehemu ya kuuzia mazao haya halimo, lipo suala la kujenga maghala na masoko ya mazao kwenye maeneo ya wakulima. Kwa hiyo, nafikiri kwamba ikipatikana *surplus*,

Serikali kwa sababu inaweka *restrictions* za kuuza mazao haya nje, tuwe na uwezekano wa kuchukua ile *surplus* ili isionekane ni laana tena mkulima anapovuna mazao yake. Inapoonekana kwamba sasa Serikali imetoshwa kununua yale mazao basi tuwe tayari na *information* kwamba wanaweza kupeleka wapi hawa wakulima mazao yao. Hivi tunavyozungumza watu wengi wanakimbia kilimo kwa sababu wanaona sehemu zote zina hasara, jua likiwaka na mvua zikinyesha kuna hasara na suala hili lina hatari sana siku zijazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia kwenye suala la bidhaa za viwanda. Sasa hivi tunapozungumza hasa sisi tunaotoka pembezoni mwa nchi kama Geita bidhaa zote hata zinazozalishwa Tanzania ni bei kubwa sana. Amesema hapa mchangiaji mmoja mimi nikawa nakumbuka bei ya nondo ya milimita 16 imetoka Sh.15,000 kwenda zaidi ya Sh.28,000 mpaka Sh.30,000. Sasa tunajuliza hizi bidhaa zote zinazalishwa Tanzania, tatizo liko wapi? Ukiangalia bei ya bati imetoka Sh.160,000 mpaka Sh.450,000, tatizo lipo wapi na ni ndani ya miaka mitatu. Watumiaji wakubwa wa bidhaa hizi ni wakulima, kama wataendelea kuona bidhaa hizi zinapanda maana yake ni kwamba wataacha kulima na watahamia mjini. Kwa hiyo, tutaanza kutengeneza mgogoro wa watu kutoa vijijini kwenda mjini kwa sababu kile anachokifanya kijijini hakimlipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wenzangu wamesema inawezekana ni utitiri wa kodi, lakini inawezekana tunahamasisha wawekezaji waje na wakati huo huo hatujaangalia ni kwa namna gani huyu mtumiaji wa mwisho hii *product* inamfikia. Sasa hivi maeneo yetu yale ni rahisi kuagiza bati za kutoka Uganda na Kenya ukazinunua kwa bei rahisi kuliko kununua bati za Tanzania, sielewi tatizo lipo wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la elimu. Naipongeza sana Serikali mwaka jana ilitenga pesa kwa ajili ya kukarabati shule kongwe, naipongeza sana. Lipo tatizo naliona kuhusu shule za msingi. Nilikusikia juzi unasema hapa

ipo shule ina watoto zaidi ya 5,000, mimi kwangu Geita Mjini nina shule tatu ambazo zina watoto zaidi ya 4,500 kwa shule moja na madarasa yapo 16 au 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni mmoja, kama inawezekana tuje na mpango kabambe kwenye mpango huu wa kuboresha miundombinu ya shule za msingi, halmashauri zetu haziwezi. Shule yenye watoto 5,000 maana yake ndani ya 5,000 kuna shule 7, lakini miundombinu iliyopo ni ya shule moja. Watoto wanaingia asubuhi wanatoka saa sita, wengine wanaingia saa sita wanatoka saa nane, mwalimu mmoja anafundisha watoto 400, hakuna *uniformity*. Huyu mwalimu hata angekuwa *genius* namna gani watoto hawawezi kuelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba kama tulivyofanya kwenye vituo vya afya na zile shule maalum, tuje na progamu maalum ya kuboresha hizi shule za msingi. Tuzitoe hizi shule kwenye watoto elfu moja na kitu twende kwenye watoto 800 au 1,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hapa kwenye shule, lipo tatizo la watoto ambao wanamaliza sasa darasa la saba na hawawezi kuchukuliwa wote kwenda sekondari za Serikali na hata sekondari za Serikali zenyewe zimejaa. Nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Elimu, unajua zamani ilikuwa watu wote tunafanya mtihani unaambiwa haukuchaguliwa, si kwa sababu walikuwa hawapendi twende shule, walikuwa wanaangalia uwezo wa shule. Sasa siku hizi shule moja ya sekondari *form one* inapokea watoto 700, miundombinu iliyopo ni ya watoto 120, kwa hiyo, miezi sita ya kwanza yote Halmashauri inahangaika kuwatafutia watoto pa kusoma, hawa watoto watakuja kupimwa na mtihani ule ule wa watoto walioanza Januari, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tu-*come up* na mfumo, tujue kwamba Halmashauri hii ina nafasi 2,000, watoto watakaochaguliwa ni watoto 2,000 na watakaobaki watafute shule nyingine, ndiyo maana zamani watu walikuwa

wanasoma kwa bidii. Hauwezi kuwa na mfumo wa kuchukua watoto wote, haiwezekani kwa sababu itakuwa kila mwaka hakuna halmashauri ambayo imekamilisha miundombinu. Tulikamilisha madawati mwaka juzi, sasa hivi hakuna shule yenye madawati ya kutosha na tulikamilisha madarasa hakuna shule yenye madarasa ya kutosha kwa sababu mfumo tullionao sekondari ni kuzoa watu wote, hauwezi kuwa na mfumo wa namna hiyo. Kwa hiyo, ni lazima tufike mahali tuseme kwamba nafasi tulizonazo ni hizi na kunakuwa na *cutting point* kwamba hapa tumekata *cutting point*, kama nafasi zipo ziende sehemu nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo pia la watoto sasa ambao inaonekana kwamba wanapomaliza darasa la saba au wanamaliza *form four* katika shule binafsi wanakwenda chuo kikuu halafu inaonekana kigezo cha kupata mkopo chuo kikuu unatakiwa uwe umesoma kwenye shule ya watu wanyonge, hiki kigezo si sahihi. Tunafahamu kwamba wapo watumishi ambao walikuwa na uwezo wa kusomesha watoto wake wawili kwenye shule nzuri lakini amestaafu, sasa kama kigezo ni hicho maana yake ni kwamba watoto wengi sana watakosa mikopo na ndicho kinachotokea sasa hivi, watoto wote wanamaliza darasa la saba wanakwenda kurundikwa sekondari ya Serikali kwa sababu anahofia mwanaye asikose mkopo chuo kikuu. Mimi nashauri, kama inawezekana mtoto yeyote aliyefaulu kwenda chuo kikuu apatiwe mkopo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi, tulipiga kelele sana hapa Bunge lililopita kuhusu uvuvi. Tunashukuru kwamba Serikali ililifanyia kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia sentensi yako.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Serikali ililifanyia kazi. Hoja

yangu hapa ni ndogo, wavuvi wa sangara sasa hivi kwenye Kanda yetu ya Mwanza wanalalamika bei imepungua na kosa lilikuwa ni moja. Wakati sisi tunafanya operesheni kubwa wenzetu Kenya na Uganda walikuwa wanaendelea na kuvua na kuuza Ulaya. Kwa hiyo, matokeo yake walikamata masoko yetu kule na sasa hivi wavuvi wetu Kanda ya Ziwa wanakosa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri sasa Serikali, kwa sababu lipo tatizo la wamiliki wote wa viwanda vya samaki kuwa ni wa aina moja, wanafanya *cartel*, wanakaa wanapanga. Tutafute uwezekano wa kutafuta mtu wa kukaa katikati pale ili asiwe anakubaliana na lugha moja wanayozungumza wale wenye viwanda vya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Pascal Haonga na Mheshimiwa Eng. Edwin Amandus Ngonyani ajiandae. Mheshimiwa Haonga, tafadhali.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba sasa na mimi niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la watumishi wa umma. Watumishi wa umma katika mpango huu naona kabisa kwamba wamesahaulika na kama si kipaumbele. Nimeangalia karibu kurasa nyingi sijaona mpango wa kuwaongeza watumishi wa umma mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo kwa kweli limetengeneza vidonda vikubwa sana mioyoni mwa watumishi wa umma katika Taifa letu. Watumishi wanalalamika tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani haijawahi kuwaza wala kufikiria kuwapandishia watumishi wa umma mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia kwa mfano kwenye kitabu hiki cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukurasa wa 85 wanasema ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za sekondari na ujenzi wa mabweni.

Pia ukienda kwenye kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, wanazungumzia ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya, nyumba takriban 306. Hata tukiwajengea maghorofa watumishi wa umma, kwa maana ya watumishi wa umma kwenye afya, idara ya elimu na kilimo, kama hawakuongezewa mishahara tutakuwa tunafanya kazi bure. Watumishi wengi wamekata tamaa, walimu wamekata tamaa na hali ni mbaya kwa sababu Serikali hii haijawahi hata mara moja kuwaongezea mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani inawezekana kuna tatizo aidha mmeshindwa kumshauri Rais afanye hivi au mnamuogopa. Sasa sijui, lakini kama mnamuogopa mtakuwa mmetenda dhambi sana kwa watumishi wa umma ambao tunawafanyisha kazi nzito lakini hali ni mbaya kuliko kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wapo watumishi waliostaafu wana miaka mingi hawajawahi kulipwa mafao yao lakini sioni kwenye mpango huu kama kuna jambo hilo ambalo limeeleza hawa watumishi wanalipwa lini. Watu wanastaafu na wengine wanafariki kwa sababu ya *stress* za maisha lakini mafao yao hawajalipwa. Nadhani sisi kama Taifa bila ya kujali itikadi za vyama vyetu kuna jambo sasa la kufikiria namna gani hawa watu wanaweza kulipwa ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kuhusu mazao yote ya wakulima. Nimesoma kwenye hii hotuba ya Waziri amezungumza kwenye zile changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Bajeti wa mwaka 2017/2018,

ukisoma changamoto namba sita, anasema changamoto ya masoko na bei ndogo za mazao kwa wakulima. Hii imeelezwa kama changamoto lakini nimekuja kuangalia nikadhani kwamba unapoeleza kama changamoto lazima utuambie kwamba sasa suluhisho la masoko itakuwa ni ipi ili wakulima wetu waweze kupatiwa bei nzuri ya mazao yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo zao la kahawa hali ni mbaya bei ipo chini na mahindi hali ni mbaya. Wamezungumza baadhi ya Wabunge waliochangia humu ndani asubuhi, leo mkulima kwa mfano ukienda Mikoa ya Songwe, Mbeya, Ruvuma na Rukwa debe la mahindi linauzwa shilingi 2,500 na gunia moja linauzwa shilingi 15,000. Ili uweze kununua mfuko mmoja wa mbolea ya kupandia DAP ambao unauzwa shilingi 70,000 na ukisafirisha kutoka mjini kwenda kijijini kwenye mashamba ni shilingi 75,000, kwa hali kama hiyo unaona mkulima anauza bei ndogo mazao yake lakini wakati huo huo pembejeo zipo juu.

Sasa ndiyo hayo mambo ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango ulitakiwa utuambie namna gani mnaenda kushusha bei ya pembejeo kama mbolea lakini pia mnaenda kutafuta masoko ya mazao ya wakulima. Mazao yote nchi nzima, mahindi, kahawa, mbaazi ambayo ilikuwa shilingi 2,000 sasa hivi wanauza shilingi 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho ambalo ndiyo tulisema ni zao pekee lililokuwa limebaki angalau lilikuwa linatuingizia fedha za kigeni nyingi sana katika Taifa letu, leo korosho hali ni mbaya, wakulima wanalia na viongozi wanakuja na matamko wanasema kesho Serikali inaenda kununua korosho kama hazikununuliwa na wafanyabiashara. Sisi tunaomba mkanunue kweli kwa sababu mmeshaahidi kwa wananchi kwenda kununua. Soko huwezi ukatumia mabavu, soko lina *principle* zake siyo suala la kutumia mabavu. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu kwamba, kama alivyochangia ndugu yangu hapo, Mheshimiwa Kanyasu, leo asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania ni wakulima, mazao yote bei iko chini tafsiri yake ni kwamba hawa wakulima hata uwezo wa kununua bidhaa utakuwa ni mdogo sana na bidhaa zote zimepanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza hapa kuhusu vifaa vya ujenzi; saruji, bati, mafuta, hali ni mbaya, lakini mazao ndiyo kama hivyo hali imekuwa hivyo. Sasa hapa haitakiwi Wabunge walalamike halafu na Mheshimiwa Dkt. Mpango ambaye aliaminiwa na Rais na yeye analalamika kwenye hotuba yake ule ukurasa wa 35, analamika changamoto ya masoko, bei ndogo za mazao kwa wakulima, anatakiwa atuambie kwamba atafanya nini kutafuta masoko kwa wakulima, siyo suala la kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake kama Mheshimiwa Waziri analalamika anatakiwa apishe kiti hicho ampe mwingine mwenye uwezo wa kufanya kazi hiyo, mwenye uwezo wa kutafuta masoko ya wakulima. Kwa hiyo, nadhani hilo ndiyo jambo kubwa zaidi, atuambie kwamba utafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naliona...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, usimsingizie Waziri, halalamiki, ameitaja kama moja ya changamoto, sasa changamoto siyo malalamiko, endelea kuchangia.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa unalalamika kiongozi, Waziri, kwamba ni changamoto umeitaja, utuambie na *way forward*, utafanya nini kama changamoto ni soko, utatafutaje masoko sasa. Hapo hajatueleza vizuri, ameeleza changamoto *page* mbili lakini pale kwenye *way forward*, namna gani anakwenda kutatua hizo changamoto...

**MWENYEKITI:** Yaani jambo hilo yeye kaleta mapendekezo, sasa wewe katika kujadili na kufanya hivi mnasaidiana na yeye kuona *way forward*, sasa na wewe unalamika; unataka wafikiri, wewe hutaki kufikiri.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto inapojirudia mara kwa mara maana yake imeshindwa kutatuliwa, ni malalamiko tayari hayo, kwa hiyo niseme tu kwamba hili ni vizuri akalipokea akaangalia namna ya kulfanyia kazi. Sisi kazi yetu kama Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, ndiyo kazi yetu hiyo. Hayo masoko wakayatafute...

**MWENYEKITI:** Ushauri unatakiwa utoe badala na wewe kulalamika, unapoteza muda wako kulalamika tu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi natoa *suggestion* wakatafute masoko ya mazao ya wakulima, hiyo ndiyo *solution* ninayotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba nizungumzie kidogo suala la kuhusu hizi changamoto zilizoelezwa hapa. Nadhani kuna changamoto moja kubwa sana imesahaulika na hii changamoto Mheshimiwa Dkt. Mpango naomba akafanye utafiti na Serikali hii ya Awamu ya Tano ikafanye utafiti na hii changamoto isipofanyiwa kazi itaenda kulimaliza Taifa; hili suala la kufanya chaguzi za marudio, pesa nyingi tunapeleka kwenye chaguzi za marudio, sasa hii lazima tuitafutie ufumbuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mbunge alikuwa chama fulani anasema leo naamua kuhamia chama kingine na kuna mmoja nimemsikia asubuhi anazungumza anasema kwamba eti niliondoka huko sasa niko huru, niliondoka CHADEMA niko huru upande wa pili, lakini alizungumza kwamba mimi nimekimbia kwa sababu nilitaka nigombee Uenyekiti na Mbowe halafu nikaona Mbowe amekataa, sasa leo ameingia CCM, tuone kama atakwenda kugombea

Uenyekiti na Rais Dkt. Magufuli, tuone, kama ninyi mnaruhusu namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunahitaji kwamba viongozi ukichaguliwa na wananchi umalize miaka yako mitano, hizi fedha za uchaguzi wa marudio ni fedha nyingi sana...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, huo nao ni mpango?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, ni sehemu ya changamoto.

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa ngapi?

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwongezea Mheshimiwa Dkt. Mpango, ni sehemu ya changamoto, angeiweka, kutumia fedha za Watanzania, fedha za wavuja jasho kwenda kwenye chaguzi za marudio, hizi fedha tungeweza kuwasaidia wakulima wetu, tungeweza kulipa mishahara kwa watumishi, tungeweza kufanya mazingira mazuri sana. *(Makofi)*

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Umeyataka mwenyewe sasa Mheshimiwa Haonga, unaona unavuruga mambo, taarifa hiyo, haya iko wapi?

## T A A R I F A

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji namheshimu sana, lakini nampa taarifa ya kwamba sasa hatutakuwa tena na upotezaji wa fedha, sasa hivi mtu akitoka huko akija huku kwetu atapita bila kupingwa na hilo limeshaanza kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Haonga, kwamba garimoshi linateleza tu. *(Kicheko)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote kama mtu ulikuwa kwenye chama ambacho watu walikuamini na wakakuchagua kwenye chama hicho ukahamia Chama cha Mapinduzi, lazima hata uwezo wako wa kufikiri huweza kupungua, ndiyo unachokiona, ndiyo madhara yake hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga, tafadhali, lugha yako ni ya kuwadhalilisha watu na ni lugha ambayo Kibunge haikubaliki, tunataniana, tunafanya hivi lakini usifike mahali pa kuwafanya wenzio kama vile... hawa ni watu wazima, siyo watoto, wamefanya *decisions* zao; *you have to respect other people's decisions*. Kwa hiyo, usiendelee na lugha hiyo, wewe endelea kuchangia tu. *(Makofi)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kuna sentensi moja ya Kizungu inasema *an empty stomach is not a good advisor*, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba wakati mwingine tumbo likiwa wazi linaweza likakushauri vibaya, ngoja tuwaache tu mwisho wa siku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya ni kengele ya pili, kwa hiyo ahsante sana Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Eng. Edwin Amandus Ngonyani, niende upande wa *CUF* sasa atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Bungara; eehee, haya Mheshimiwa Eng. Ngonyani tafadhali. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni yangu mbele ya Bunge lako Tukufu na kwa sababu muda ni mdogo naomba niende moja kwa moja kwenye mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, kwa kitu hiki kizuri alichotuletea cha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2019/2020. Ndugu zangu, mkusoma vizuri mpango wa mwaka jana na mwaka juzi na huu, mpango huu uko tofauti kabisa. Mpango huu umekuwa rahisi kuuelewa, umetumia lugha ambayo hata sisi watu ambao siyo wa uchumi tumeweza kuelewa kwa undani sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kazi nzuri hiyo aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu katika eneo la ujenzi wa barabara akifananisha na mpango wa mwaka jana alikuwa umeorodhesha baadhi ya barabara na kwa kweli ukiangalia hata katika utekelezaji wenzetu wa ujenzi walikuwa wanafuata kile kilichoandikwa katika mpango. Kwa hiyo, naomba mpango huu utakapokamilika nimwombe Mheshimiwa Waziri aoneshe vilevile na orodha ya barabara zitakazohusika ili zitoe mwongozo kwa Wizara husika ili kwa mfano kubwa zaidi barabara ambazo bado hazijakamilika hadi sasa tungeomba sana zikamilishwe, zitengewe bajeti iingie katika mpango ili kukamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizo ni pamoja na Barabara ya Likuyufusi hadi Mkenda ambayo inaunganisha Tanzania na Msumbiji kupitia Jimbo la Peramiho. Vilevile barabara nyingine ni barabara ya Lumecha – Kitanda – Londo – Kilosa kwa Mpepo – Lupilo – Ifakara hadi Mikumi. Barabara hii iko sehemu kama robo hivi imetekelezwa hadi sasa na niombe sana tuendelee kutenga fedha ili barabara hii ikamilike, hasa kipande kile kinachoanza Lupilo – Kilosa kwa Mpepo hadi Lumecha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo inatuunganisha sisi na Wilaya ya Mavago ya Msumbiji ambayo inaanzia Mtwara Pachani – Ligeri – Lusewa – Magazini – Lingusenguse hadi Nalasi. Nimwombe sana Mheshimiwa Dkt. Mpango barabara hii aliitengea fedha mwaka jana kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hizi barabara zote ziingie katika Mpango ili Wizara inayohusika iweze kuingiza barabara hizo katika utekelezaji wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhandisi, kuna taarifa hapa.

#### T A A R I F A

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza, nafikiri umetoa ushauri hata asubuhi, anapaswa kuchangia mpango wa nchi. Sasa ameanza kuchangia barabara zake za mitaa kule, sasa yeye amekuwa Mbunge, amekuwa ni Waziri kwa muda mrefu, lakini bado anakwenda tofauti kabisa. Kwa hiyo tunataka tumrudishe achangie mpango wa nchi na siyo hicho ambacho anakizungumza. Hizo barabara za kuunganisha sijui mtaa gani na mtaa gani asubiri kipindi cha bajeti atakuja kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, endelea kuchangia.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa sababu haelewi kwamba nilikuwa natoa hiyo kama mifano na tunaongelea barabara

za Tanzania nzima. Katika barabara ndani ya mpango nimesema barabara zile ambazo zinatakiwa ziendele zisiondolewe katika mipango yetu ya mwaka huu. Kwa hiyo, siongelei barabara moja hii nilikuwa natoa mfano tu, nadhani hatuelewani kwa sababu tuko katika *levels* tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa ujenzi wa reli niipongeze sana Serikali kwa kuendelea na ujenzi wa reli ya kisasa ya kutoka Dar es Salaam – Morogoro hadi Mwanza na sasa tupo – kwa maana ya kupatikana kwa wakandarasi mpaka Dodoma. Naomba sana kazi hiyo iendele kufanyika ili mtandao wote wa reli wa kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza; Isaka hadi Rusumo; Tabora hadi Kigoma; Uvinza hadi Msongati na Kaliua hadi Karema zote zikamilike ziingie katika mpango. Vilevile reli ya kutoka Tanga hadi Musoma na reli ya kutoka Mtwara kupitia Tunduru – Namtumbo hadi Mbambabay nayo iingie katika mpango ili tuhakikishe kwamba kazi kubwa hii ambayo Mheshimiwa Rais ameianza ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu napenda sana Serikali hii ya Awamu ya Tano isiondoke kabisa kabla kazi hii ya kukamilisha mtandao huu wa reli haijakamilika. Kwa hiyo, naomba sana hata kama itachukua miaka 30 ni vyema tu tukakubali kwa sababu tunafahamu kitu kinachofanyika ni kwa manufaa ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuongelea masuala ya kilimo, hususani mazao makuu. Tukiangalia katika mazao makuu yanayotajwa, mengi sana yamewekwa kwenye mpango lakini kuna mazao kama mawili hayakuwekwa ndani ya mpango, yanatajwa kama mazao ambayo ndiyo tunapata hela za kigeni kwa wingi ikiwa ni pamoja na tumbaku, lakini kwenye mpango zaidi ya kutaja kwamba kama ni chanzo chetu cha fedha lakini hakuna kitu chochote ambacho tunakielezea au tunafanya nini kuliendeleza zao hili la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri katika kazi zinazotakiwa kufanyika katika zao hili la tumbaku ni kitu ambacho hata fedha hazihitajiki. Kinachotakiwa, moja ni kufungua masoko tu na soko kubwa ni soko la Misri ambapo ndiyo mlango wa kuingilia nchi za Ghuba na nchi zote za Kiarabu. Ningeomba sana wenzetu wa *Foreign Affairs*, Wizara inayohusika na masuala ya biashara pamoja na Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara ya Kilimo zitufungulie soko hili la Egypt ili hata sisi tunaopata fursa ya kulima tumbaku pamoja na wenzetu wa upande wa magharibi na kaskazini tuweze kupata kiasi kikubwa zaidi cha mgao wa tumbaku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa sasa nikitoa mfano tu; katika Wilaya ya Namtumbo kwa mfano uwezo wa kulima ni zaidi ya tani 4000 lakini sasa hivi tunaazimia kulipa chini ya tani 1000 kwa sababu ya ukosefu wa soko na hiyo ni kwa sababu hatujaingia katika soko kubwa la nchi za kiarabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana, nimeongea mara nyingi na Mawaziri husika, watusaidie tuingize katika mipango yetu ili tunaposema mazao haya matano na sasa ni mazao sita, yanayotuletea kipato kikubwa cha fedha za kigeni tutekeleze vile vikwazo vidogovidogo vinavyozuia mazao haya yasituingizie fedha za kutosha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji nimefurahi sana mpango umeelezea vizuri kwamba sasa tunakwenda kushughulikia vile vikwazo vinavyozuia upatikanaji wa maji usitimilike kwa haraka. Kikwazo kimoja kikubwa ni uhakika wa upatikanaji wa fedha. Naamini Mheshimiwa Dkt. Mpango safari hii katika mpango huu ambao tunakamilisha sasa hivi ametuletea mapendekezo, aje na mapendekezo au Serikali ikubali kutenga ile Sh.50/= ya nyongeza ili hatimaye iwe Sh.100/= iingie katika Mfuko wa Maji ili tuhakikishe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*



**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Ngonyani, muda hauko upande wako, malizia.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Hongera sana kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi. Nilikuwa nimemtaja...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Bwege.

**MWENYEKITI:** Huyu namruka. Mheshimiwa Selemani Bungara. Taratibu lakini Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii leo na kwa kuwa umeniambia taratibu basi leo nitakuwa taratibu kabisa. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amewapa akili Watanzania na akili kazi zake mbili tu, kujua ukweli na uongo, ndiyo kazi ya akili, hayo mengine kupata Uprofesa na nini, hayo mengine tu, lakini kazi ya akili ni kujua ukweli na uongo, nyeupe na nyeusi, ndiyo kazi yake hiyo hiyo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kusema tunamnukuu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mungu amuweke mahali anapostahili, alisema ili tuendelee tunahitaji vitu vinne; ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Nchi hii vitu vyote hivyo vinne vipo, ardhi ipo ina kila kitu, watu ndiyo wengi tu, tunafika milioni 50 na ngapi sasa hivi, siasa ipo na tangu mwaka 1961 mpaka leo chama cha siasa kinachoongoza katika nchi hii ni Chama cha CCM, kwa hiyo siasa ipo na uongozi upo, lakini unaotakiwa ni uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mipango yote mnayopanga hii, yote hii, kama siasa haikuwa safi na uongozi haukuwa bora, sawasawa na hakuna. Tangu nimeingia Bunge hili mwaka 2010 mipango inapangwa kweli kweli lakini utekelezaji hakuna. Kwa hiyo, mimi ni mwanasiasa na huwezi

ukaendelea kama siasa ikiwa mbaya. Naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali sikivu, huu uwanja wa siasa kama tukiuchezea hali itakuwa mbaya sana katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango yote hii wanayopanga, angalia sasa hivi, tumepanga mipango mikubwa, limekuja jambo hili la kununuliwa Wabunge, hela zote ambazo tulipangia katika mambo ya maendeleo zinakwenda katika bajeti ya kufanya uchaguzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitunzie muda wangu, mimi namjua dada huyu, lazima asimame tu huyu, nikisema mimi tu basi. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Bungara leo anazungumza taratibu sana lakini kwa mujibu wa kanuni zetu, Kanuni ya 68(1) na Kanuni ya 64(1)(a) na Kanuni ya 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimwarifu Mheshimiwa Bungara kwamba hili analisema kwamba miradi iliyoshindwa kutekelezwa ni kwa sababu fedha zote zimetumika kuwanunulia Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimthibitishie Mheshimiwa Bungara kwamba hakuna fedha yoyote iliyotumika kumnunua Mbunge, haijaletwa fedha iliyotumika kumnunulia Mbunge na hivyo naomba tu Mheshimiwa Bungara jambo hili aliondoe tu kwa sababu halina uhalisia na siyo jambo la ukweli, amuache tu Mheshimiwa Dkt. Mpango aendelee na mpango wake na mpango huu umetekelezwa na matokeo ya utekelezaji wa mpango yanajidhihirisha. Tumetoa hesabu ya zahanati zilizojengwa, vituo vya afya, barabara, miradi ya maji, viwanja vya ndege, barabara za juu. Kwa hiyo, hayo yote yanajidhihirisha kwamba miradi imetekelezwa na siyo kile ambacho anakisema. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema fedha zimetumika katika uchaguzi. Uchaguzi ambao ulikuwa hauna sababu yoyote na hiki kitabu cha Mheshimiwa Dkt. Mpango, mwenyewe kasema katika ukurasa wa 44 kwamba fedha triloni tisa hazikupatikana na mambo mengi ya maendeleo hayakufanyika, lakini fedha hizo zilienda katika uchaguzi. Sasa unachosema kwamba kununuliwa hata mimi si nilifuatwa! Hata mimi mwenyewe nilifuatwa, sasa ukitaka ushahidi anaitwa nani yule Mheshimiwa Jenista uje, tukutane baadaye nikwambie walikuja nani na nani walitaka kuninunua mimi nikakataa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hela Wabunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Kwanza uongee na kiti.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya basi.

**MWENYEKITI:** Usiongee na Mbunge mmoja mmoja.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuelewa, samahani.

**MWENYEKITI:** Halafu pili usiingie kwenye kumi na nane zangu kwa sababu zitakupa shida.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo ukitaka haya mambo ya ushahidi na nini basi tutapelekana huko itakuwa taabu!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Inshallah*, lakini nilifuatwa. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara usinilazimishe.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi, mzee mwenzangu basi yaache tuendelee.

**MWENYEKITI:** Ukilipenda hilo na mimi nalipenda kweli hilo.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee mzee mwenzangu.

**MWENYEKITI:** Lakini nina hakika litakupa taabu.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee mzee mwenzangu.

**MWENYEKITI:** Haya.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Dau alisema jambo kubwa sana katika Bunge hili na mimi nasikitika sana, Waziri Mkuu anachaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na anathibitishwa katika Bunge hili. Kwa hiyo, Waziri Mkuu anachaguliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dau jana alisema kwamba kuna Waziri mmoja wa Ujenzi alimwambia habari ya boti lakini akajibiwa majibu mabaya na Waziri wa Ujenzi. Sasa hiyo siyo mara moja tu, Mheshimiwa huyu Waziri wa Ujenzi alikuja Kilwa hivyo hivyo nikamwambia kuna mradi wa maji wakati huo alikuwa Naibu Waziri wa Maji, nikamwambia nimeonana na Waziri Mkuu na yeye akanijibu kama alivyojibiwa Bwana Dau, akasema Waziri Mkuu nani, bwana! Mimi namtambua Mheshimiwa Magufuli tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme Waziri Mkuu ambaye amechaguliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wwa Tanzania na kuthibitishwa na Bunge hili na mimi nilimpigia kura ili awe Waziri Mkuu. Halafu kuna mtu mmoja ambaye anachaguliwa tu lakini wala hathibitishwi na Bunge anamdhalilisha Waziri Mkuu. Mimi nikifikiri anadhhalilisha ninaposema mimi mpinzani tu, kumbe hata akisema Mheshimiwa Dau wa Mafia naye anaambiwa hivyo hivyo hii siyo desturi nzuri Waheshimiwa, huyu ni Waziri Mkuu asidharauliwe na najua watu wa CCM nimewaambia jana vipi wamesema bwana sisi tukisema sana tunaitwa katika maadili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, uko kwenye shughuli yako ya kuchonganisha ili watu wagombane huku?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nanukuu ya jana. Jana hiyo hiyo kuna Mheshimiwa Sugu hapa kasema kwamba watu wanauliwa akatoka Waziri mwingine akasema hajauliwa. Sasa nina ushahidi kwamba Polisi wa Tanzania wameua watu wangu Kilwa ndani ya msikiti na yule Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alisema kwamba kama kuna ushahidi atoe, mimi ushahidi ninao kwamba Polisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walimuua Ismail Bweta katika Msikiti Chumo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mwigulu akaniita wakati huo akiwa Waziri wa Mambo wa Ndani

akaniambia niwalete hao watu, nikaja nao watu kwa Waziri Mwigulu, baba wa marehemu na yule mtu aliyetolewa jicho na Polisi. Mheshimiwa Mwigulu alipopewa taarifa akasema jambo hili zito umpeleke kwa Waziri Mkuu. Namwambia tu huyo Mheshimiwa anasema kwamba Polisi hawajaua watu. Nikawapeleka wale watu Waziri Mkuu wakamwambia, kidogo alie akasema kweli Serikali imefanya kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo mambo yapo nchi hii na mnaua, mnateka na mimi ushahidi ninao, hii yote tunasema ili tuendelee tunahitaji vitu vingapi vinne ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Kitendo cha watu kuuliwa na taarifa mnapata... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mpango kuna mipango hiyo ya mauaji nani?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si utawala bora alisema hapa Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Ukurasa wa ngapi?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa tena! Tunapanga mipango ya nchi kwamba kama siasa itakuwa mbaya. Nimeanza kusema kwamba siasa mbaya mipango yote itakuwa hakuna kama siasa itakuwa mbaya sasa uelewi tu, mzee mwenzangu huelewi ninachokisema?... *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili hiyo bahati mbaya.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haa, bado.

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya namalizia kwamba, naomba sana Serikali muwe makini, muwe wakweli, kwa sababu Mtume anasema utakuja wakati viongozi watakuwa waongo na watu watawajua kuwa waongo, lakini watawapigia makofi na kuwachinjia nyama ili hali watakuwa waongo viongozi hao. Basi msitegemee rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mwisho wa yote, naomba korosho zote wakanunue kwa sababu waliahidi wakanunue ili mambo...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** ...watu wetu wa Kusini mipango yao iende vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mipango bila korosho kununua hakuna mipango. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa anafuata Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Leah Komanya kama yupo ajiandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia. Napongeza mapendekezo ya mpango kwa kweli ni mazuri isipokuwa naomba nijikite katika eneo moja au mawili hasa kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu umuhimu wa kilimo. Pamoja na kuwa tunasema kilimo ni uti wa mgongo ndiyo sekta itakayoleta ajira nyingi sana kwa vijana na itaondoa umaskini kwa kiasi kikubwa sana. Pamoja na kuwa na mikakati na miradi mingi ya kuendeleza kilimo katika nchi yetu mingi naiona bado iko katika mipango, utekelezaji bado haujaonekana kwa maana ya uboreshwaji wa kilimo ambacho kwa kiasi kikubwa takribani asilimia 65 mpaka 70 kinafanywa na wanawake vijijini ambayo ni nguvu kazi kubwa lakini wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana. Changamoto zinafahamika na tungependa kuona kwenye mpango sasa jinsi gani hii mikakati na miradi mikubwa iliyoletwa akina *ASDP II*, *SAGCOT* na mikakati mingine yote katika sekta za uvuvi na ufugaji zinatiririka sasa kwenda kwa wale ambao ndiyo hasa wazalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko njia nyingi za kuendeleza kilimo kwa kukiboresha. Muda mrefu sana tumekuwa tukizungumzia mnyororo wa thamani, hiyo ilikuwa ni njia moja nzuri sana ya kuhakikisha kwanza kilimo chetu kinakuwa na tija lakini kinaleta ajira, kinaongeza thamani ya mazao yetu na kuwezesha soko la ndani kujihimili katika kujitosheleza kwa mahitaji yake na hata kuuza nje ya nchi. Hali ilivyo sasa hivi Serikali na wakulima wanagonganisha vichwa, kila tunakoenda wakulima wanalalamika sana na wana haki ya kulalamika kwa sababu wanatumia nguvu yao wenyewe nyingi, wanapoteza fedha nyingi lakini wanachokuja kupata baada ya kulima ni kitu ambacho kwa kweli hakiwatoshelezi wao hata Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kuwa wakulima wengi ni wanawake lakini vilevile ajira nyingi zinaweza zikazalishwa kwa vijana kwa kutumia kilimo, ufugaji na uvuvi. Nini kifanyike, ni kuhakikisha kuwa zile changamoto



zilizoainishwa ndiyo ambazo Serikali inaziwekea mkakati wa kuhakikisha kuwa wanazitatua. Upatikanaji wa mitaji kwa wakulima bado ni mdogo na unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo Benki ya Wakulima iliyoanzishwa bado ina-*deal* na watu wa ngazi za juu, inataka vikundi vilivyosajiliwa na watu ambao wako kwenye mfumo rasmi, wakulima wetu wengi na vijana wetu wengi hawako kwenye mifumo hiyo. Kwa sababu hawako kwenye mifumo hiyo tulikuwa tunategemea benki ingeji-*restructure* iwakute hawa. Tanzania siyo peke yake inayofanya hivi, ziko nchi nyingi na zimefanikiwa kwa kuhakikisha kuwa mifumo yao ya kutoa mitaji kwa ajili ya kilimo inakwenda sambamba na aina ya wakulima tulionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la kuongeza thamani. Mnyororo wa thamani ndiyo utakaotuhakikishia kuwa kwanza tunaunganisha kilimo na sekta binafsi. Kwa sababu kwa upande mmoja sekta binafsi ndiyo inaingia katika mambo ya *value addition* na masoko na kwa kutumia weledi na nyenzo bora wanazotumia wao wanaweza kusaidia hata wakulima katika ngazi za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu ambao wameendelea kwenye kilimo, kwa mfano Vietnam, South Korea, Thailand, wakulima wao wote bado ni wadogo lakini wametafuta hizo *linkages* na *private sector*, watumia *outgrower schemes*, *irrigation schemes* na ku-*link* na wanunuzi wakubwa wa nchi za nje kwa kutumia Serikali na wakafanikiwa sana. Sasa hivi wanatumia kilimo katika kuhakikisha kuwa wana *export* kwa wingi zaidi kutokana na hao wakulima wadogo wadogo. Naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango angalieni jinsi gani mtaboresha mikopo na huduma za muhimu za ugani kwa wakulima wadogo ambao ni wengi na hapo ndiyo mtakapooni tija ya kilimo itakavyokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kuhakikisha kuwa nyenzo bora zinapatikana. Wakulima wengi ni wanawake, tuna *TEMDO*, *CAMARTEC*, *TIRDO* na *SIDO*,

wanafanya nini kuhakikisha kuwa akina mama hawa wanatengenezewa nyezo zitakazofaa kutumia wao kufuatana na nguvu zao na uwezo wao na jinsi ambavyo wanajikita kwenye mashamba yao. Tuna taasisi, makampuni na mabenki tunachotakiwa sasa kama Serikali ni kuwaunganisha hawa sasa na wakulima, vijana kwa wanawake ili sasa tija ipate kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalalamikia masoko, lakini hata soko la ndani lenyewe hatujalitosheliza kwa bidhaa hasa zile muhimu zinazohitajika. Tunaagizaje *tomato paste*, *tomato sauce* na *chill sauce*, wakati nyanya zinaoza mashambani. Vijana wamekaa hawana kitu cha kufanya wakati teknolojia ya kufanya hivyo ni ya nyumbani kwa mtu, unajifungia *store* unatengeneza *tomato paste*, *tomato sauce* na *concentrate* za *tomato* ambazo unaweza kuuza mpaka nchi nyingine au unaweka wakati ambao siyo msimu unatumia, kwa nini bado hatujalifikiria hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala la umwagiliaji. Tanzania nafikiri ni nchi ya pili kama siyo ya tatu kwa wingi vya vyanzo vya maji lakini mpaka leo kilimo chetu kinategemea mvua. Napenda sana kuona zile *scheme* ambazo zimeshatengenezwa tayari lakini hazifanyi kazi zirekebishwe, zikarabatiwe ili wananchi walime kilimo cha umwagiliaji. Kila wilaya utakuta kuna *scheme* za umwagiliaji zimekufa au zina vitu vidogo tu vinavyohitaji matengenezo lakini havifanyiwi kazi tunafikiria mambo makubwa. Mambo makubwa ni mazuri lakini haya madogo ni mazuri zaidi kwetu sisi tunaotaka kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuzungumzia *SAGCOT* pamoja na *ASDP II*. Hii yote ni miradi mizuri sana na inalenga kutukwamua lakini kwa kiasi kikubwa sana inategemea fedha ya nje. *SAGCOT hundred percent I think* ni hela ya nje. Sasa ikikosekana na wakati tunaona kabisa *SAGCOT* ndiyo ambayo inaelekeza sasa kilimo cha kisasa kwa kutumia mfumo wa sekta binafsi lakini tunawategemea watu wa nje. Napenda kuona Serikali na yenyewe inaingiza mkono wake kwa kuweka fedha ya kutosha kwenye *SAGCOT*

ili sasa tuwe na uhakika kuwa huu mkakati utaendelea na kuwavuta watu wengi zaidi kuingia katika mfumo rasmi wa kuendesha kilimo na kukiendeleza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudi kwenye suala la vijana wetu, ajira nyingi sana za vijana zitatoka kupitia kilimo, ufugaji na uvuvi. Tujiulize kwa nini vijana hawapendi kuingia kwenye kilimo, ufugaji au uvuvi wa kisasa? Changamoto zao zinajulikana, vijana siyo watu wanaotaka kushinda shambani kutwa nzima na jembe. Ndiyo maana mpaka sasa hivi wengi wanaolima ni watu wazima na vijana wanawake lakini vijana wanaume wengi hawalimi kwa mtindo huu tunaoendelea nao sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuona Serikali inakuja na mkakati wa ku-*involve* vijana kwenye kilimo *specifically*. Wale vijana wachache walioweza kulima wameona faida zake na huwaondoi huko. Kulikuwa na mradi wa MUVI ambao umekuwa ukisaidia vijana, wengi sasa hivi wamejikita kwenye kilimo na wanafurahia sana lakini bahati mbaya sasa na wenyewe wanakosa masoko kwa sababu hakuna ule mnyororo wa thamani ambao umeunganishwa katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kabla kengele haijaliala Wizara haziongei, Wizara hazizungumzi, hakuna *interconnection* kama alivyosema Mheshimiwa Lucy asubuhi. Wizara ya Kilimo wana mikakati yao wanaendelea nayo huku na Wizara ya Viwanda wana mikakati yao wanaendelea huku wakati hawa ndiyo wanaotakiwa kuungana. Mpango utakapokuja sasa tuone kabisa ile *link* ya moja kwa moja kati ya kilimo na viwanda, uvuvi na viwanda, ufugaji na viwanda pamoja na ajira zao. Hii itaweza sasa kuona ile *integration* nzuri ya uchumi kuelekea uchumi wa viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la jinsi gani nguvu kazi watu inatayarishwa. Tuna miradi mikubwa mingi sana ambayo inaendelea sasa hivi, je, tunao wafanyakazi, vijana au watumishi wenye taaluma watakaokuja kufanya kazi

kwenye miradi hii? Kwa hiyo, haya yote ni mambo ambayo ukiangalia lazima yawe *linked*...

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janet, malizia muda tayari.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono lakini napenda sana kuona *integration* ya sekta zote muhimu au Wizara zote muhimu ku-*converge* kwenye uchumi wa viwanda. Hiyo ndiyo itakuwa njia peke yake ya kuhakikisha kuwa uchumi wetu na huu mpango unaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Janet Mbene kwa mchango mzuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Leah Komanya na Mheshimiwa Justin Monko atafuatia.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu jioni hii ya leo, nikimshukuru Mungu kwa kuniweka niweze kutoa maoni. Awali ya yote, napenda nipongeze Wizara kwa kutuletea mpango mzuri ambao umeambana na utekelezaji wa shughuli za maendeleo uliotekelezwa kwa vipindi vilivyoainishwa katika kitabu cha mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango utajielekeza kwa kupongeza Serikali kwa kazi ilizozifanya kwa kuwa tumeletewa utekelezaji wa miradi ya maendeleo pia na kutoa ushauri katika Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumshukuru kwa ziara aliyoifanya Mkoani Simiyu mapema mwezi Septemba ambapo alifungua Hospitali ya Mkoa ya Rufaa. Kufunguliwa kwa Hospitali ya Mkoa katika

Mkoa wa Simiyu kutaenda kuwapunguzia wananchi kutembea umbali kwenda Hospitali ya Rufaa ya Bugando pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyango ambapo kulikuwa kuna umbali wa kilometa 140. Kwa kufanya hivyo pia tutaweza kunusuru vifo ambavyo vilitokana na kusafirishwa kwa mgonjwa na kufariki kabla ya kupatiwa hata huduma wakati wa kufika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais akiwa Mkoani Simiyu alizindua vituo vya afya, maabara pamoja na wodi 39 na aliweka jiwe la msingi katika Daraja la Mto Sibiti na utekelezaji wa daraja hilo uko kwa asilimia 79.8. Daraja hilo litakapokamilika litakuwa lina manufaa kiuchumi katika Mkoa wa Simiyu na mikoa mingine ya jirani kwa sababu itasaidia bei ya vifaa vya ujenzi kupungua. Kwa mfano, *cement* katika Mkoa wetu inauzwa kwa Sh.18,500 kutokana na gharama kubwa ya usafirishaji. *Cement* mpaka ikafike mkoa huo inazungukia Mkoa wa Shinyanga ndiyo irudi kuingia katika Mkoa wa Simiyu. Kwa hiyo, kuna manufaa ya kiuchumi kuwepo kwa Daraja la Sibiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walikuwa wakisafiri kwenda Dar es Salaam kwa muda wa siku mbili. Walisafiri mpaka Shinyanga na kulala Shinyanga na kuanza safari ya kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo, kuwepo kwa daraja hilo kutasaidia wananchi kusafiri kwa muda mfupi na kuokoa fedha zao ambazo wangezitumia katika usafiri wa siku mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijikita katika mpango, naomba nishukuru Serikali kwa ujenzi wa reli kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Wakati Kambi Rasmi ya Upinzani ikiwasilisha hotuba yake ilisema kwamba *Standard Gauge* haitakuwa na manufaa kwa sababu muda mwingi itasafirisha abiria, siyo kweli, yapo manufaa ya kiuchumi kwa kutumia reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Standard Gauge* ina manufaa katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa pamoja na

Magharibi. Tukumbuke kwamba Kanda ya Ziwa pamoja na Mikoa ya Magharibi haina viwanda vya *cement*. Kuwepo kwa *Standard Gauge* kutasaidia kuokoa gharama ya usafirishaji wa saruji. Kwa mfano, saruji kutoka Pwani pamoja na Mbeya kwa malori ingesafirishwa kwa gharama kubwa lakini kuwepo kwa *Standard Gauge* tutaweza kuokoa Sh.5,000, kwahiyo bei ya saruji pamoja na vifaa vingine vya ujenzi itapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Ziwa inazalisha pamba ya kutosha, marobota yanasafirishwa Dar es Salaam kwa kutumia magari. Kuwepo kwa reli hiyo marobota ya pamba yatasafirishwa kutoka Kanda ya Ziwa kwa gharama ndogo. Wafugaji watasafirisha ng'ombe zao kwenda Dar es Salaam na mikoa mingine kwa kutumia reli hiyo, kwa hiyo, tutaokoa gharama za usafirishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia itatumika kupeleka na kutoa mizigo katika nchi jirani ya Rwanda. Kwa hiyo, wanaobeza kwamba *Standard Gauge* haina manufaa ya kiuchumi, manufaa ya kiuchumi yapo. Nashauri sasa katika mpango waweke fedha ya kutosha kwa ajili ya usanifu wa mazingira ambapo mradi huo utapitia ikiwemo pia ulipaji wa fidia. Serikali ifanye juhudi ya kumpata mwekezaji kwa ajili ya kujenga kipande cha Isaka-Rusumo. Kanda ya Ziwa inategemea bandari ya nchi kavu iliyopo Isaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niishukuru Serikali ndani ya miaka mitatu imeweza kuongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 mpaka shilingi bilioni 269. Hii hatua ni kubwa sana, imeweza kusaidia upatikanaji wa dawa ambao siyo chini ya asilimia 80. Wauzaji wa dawa binafsi wanalalamika biashara yao imekuwa mbaya, hii ni kwa sababu kuna dawa za kutosha katika hospitali zetu. Serikali imewasaidia wananchi kuwapunguzia gharama za kununua dawa katika hospitali na *pharmacy* za watu binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri yanayofanywa na Wizara ya Afya kuna changamoto katika

kutoa huduma kwa wazee. Wazee wetu wanapewa huduma kwa kupewa vitambulisho lakini ikumbukwe kwamba vitambulisho hivyo vinatolewa ndani ya Wilaya. Wazee wetu wanapopata rufaa vitambulisho vile havikubaliwi. Nashauri kuwepo na mpango wa kuweka fedha kwa ajili ya kuwakatia bima ya afya sambamba na kupatiwa dawa muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wetu hawa wanaugua magonjwa ya moyo, sukari ikiwemo saratani, ni dhahiri kwamba magonjwa haya mengine hayatibiwi katika hospitali za Wilaya. Kwa hiyo, wazee wanayo changamoto ya kutokuwa na fedha ya kutosha kwa ajili ya kwenda kutibiwa nje kwa sababu vibali vile havikubaliki. Kwa hiyo, nashauri kuwepo na bima ya afya kwani itasaidia kuwepo na mzunguko wa fedha katika Hospitali za Wilaya. Wazee wetu wanatibiwa bure na Serikali kwa sasa hivi haifanyi marejesho ya fedha walizotibiwa wazee. Nashauri wazee hawa wapatiwe bima ya afya ambayo itazisaidia hospitali zetu kuwepo na mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja mkono, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya. Nilikuwa nimeshaahidi kwamba anayefuata ni Mheshimiwa Justin Monko na Mheshimiwa Mussa Mbarouk ajiandae. Mheshimiwa Justin Monko.

**MHE. JUSTIN M. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa mpango huu ambao ametuletea hapa Bungeni ili sisi nasi tuweze kuupitia na kutoa mapendekezo na maoni yetu. Wamefanya kazi kubwa na tunaanza kuona kwamba upo mwanga mkubwa wa kuweza kutekeleza miradi mingi

ambayo tumeikusudia na ambayo ipo katika mpango wa miaka mitano wa 2016-2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la ukusanyaji wa mapato. Katika taarifa tulizozipata na za kiutendaji katika mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018 zinaonyesha kwa kiasi fulani tumeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato. Pamoja na kwamba TRA wamefanya kazi kubwa lakini tumeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato na hatimaye mipango au miradi ya maendeleo mingine imeshindwa kufikia asilimia 100 kwa namna tulivyokuwa tumepanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe na nishauri, zipo changamoto ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja, nami nataka nijikite katika baadhi ya changamoto hizo ili kusudi tuweze kuona namna gani ambavyo tunaweza tukapata mapato au kubadilisha mbinu za ukusanyaji wa mapato na kuweka miradi mingine ambayo pia inaweza ikatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo limeelezwa hapa ni ugumu wa ukusanyaji. Tunao ugumu wa ukusanyaji wa mapato kwa sababu ya uwepo wa sekta isiyo rasmi ambapo tunaishindwa kukusanya mapato yake. Nakubaliana na changamoto hii na wewe mwenyewe ni shahidi, mimi natoka Mkoa wa Singida na wewe hapa Dodoma sisi ni wakulima wa alizeti. Tunazo biashara nyingi sana ambazo zinafanyika kwenye barabara. Wakulima wanakwenda wanakamua alizeti, wanaweka kwenye madumu, wanafanya kazi ya kusubiri wanunuzi kwenye barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili likiwekewa utaratibu mzuri tunaweza kabisa tukapunguza ukubwa wa tatizo hili la biashara zisizo rasmi. Mfano tunatumia fedha nyingi sana katika kuingiza mafuta ya kula kutoka nje na sisi ni wazalishaji wazuri wa mbegu za mafuta yakiwemo ya alizeti. Ni kwa nini katika mpango huu tusipunguze kiasi cha fedha za ununuzi wa mafuta na tukawekeza katika ununuzi



wa mashine za kufanyia *double refining* ili kuongeza thamani na ubora wa mafuta yetu tukaweza kuuza kwenye masoko ya ndani na masoko ya nje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kukusanya mafuta yote ambayo yanauzwa barabarani na wananchi upo tukiwa na viwanda vya kutosha vya *double refining*. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewatafutia wakulima wetu masoko yenye uhakika maana watakuwa hawana sababu tena ya kusubiri barabarani, wanaweza wakapata masoko kule kule wanakokamua alizeti na viwanda vya *double refining* vikachukua mafuta yale kwa ajili ya kwenda kuyachakata kwa mara ya pili na yaweze kwenda kwenye masoko ya ndani na nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, tutakuwa pia tumepunguza changamoto hiyo ambayo imeelezwa katika kipengele cha sita, changamoto ya masoko na bei ndogo za mazao. Wakulima wetu hawa wanapokuwa wanafanya biashara zisizo rasmi wanapoteza muda mwingi. Walioko barabarani walipaswa wauze yale mafuta na waende wakafanye shughuli nyingine badala yake wamekaa wakisubiri na mafuta yanaweza yakakaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto ambayo imeelezwa iliyopunguza mapato yetu, nayo ni kukosekana kwa ajira. Pamoja na juhudi kubwa ambazo Serikali yetu imefanya za kuongeza ajira lakini bado tunao upungufu mkubwa sana wa ajira katika maeneo yetu. Nitatolea mfano katika Halmashauri yangu ya Singida DC, kwenye sekta ya kilimo peke yake tunao watumishi 23 kati ya 105, kwa hiyo, tuna upungufu wa watumishi 88, sekta ya elimu ya msingi tuna watumishi 831 kati ya 1,629, sekta ya mifugo, watumishi 23 kati ya 84 na sekta nyingine nyingi, tunahitaji walimu wa sayansi 70 katika halmashauri pale, kwa hiyo, utaona zipo nafasi nyingi za ajira. Niiombe sana Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuajiri kwenye maeneo haya ambayo yana upungufu mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona madhara yake, kwa mfano kwenye sekta ya elimu. Mkoa wa Singida ni moja ya Mikoa ambayo haijafanya vizuri sana kwenye sekta ya elimu lakini tuna upungufu mkubwa wa walimu kama nilivyowaeleza na walimu wengine wanafundisha madarasa zaidi ya wanafunzi 100 hata wengine kufikia 150. Katika hali hii hatuwezi tukatoa elimu iliyo bora na elimu itakayotosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta ya kilimo unahitaji kuongezwa. Sekta ya kilimo ndiyo inayochangia sana katika uchumi wa wananchi wadogo. Serikali hii ya Awamu ya Tano ndiyo imejipambanua kuwa Serikali ya wanyonge ambao zaidi wako vijijini. Kwa hiyo, niombe sana Serikali, nimuombe sana Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, utakapokuja na mpango tungetarajia tuone asilimia ngapi ya bajeti ambayo itakuwa imetengwa kwenda kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa tukiomba kufikia asilimia 10 ya bajeti nzima lakini hapa sasa tunaona bajeti ya maendeleo kwa asilimia 37 lakini tungependa tuone sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo imetengewa asilimia ngapi. Tumeomba kwa muda mrefu, Mheshimiwa Dkt. Mpango najua wewe ni msikivu, muende mkafanye utaratibu ili kusudi tuweze kugusa maisha ya wananchi walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilisema, tuna umasikini wa asilimia 28.2, kwa hiyo, tunayo kazi kubwa ya kufanya. Bila kugusa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi hatuwezi kugusa kundi hili kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa miradi ya maji, zipo takwimu zimeonyeshwa hapa, viko vituo vingi ambavyo vimeongezeka na mimi niipongeze sana Serikali kwa kuongeza vituo vingi lakini mashaka yangu makubwa ni katika idadi ya wanufaika ambayo imeelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye ukurasa wa 31. Inawezekana katika visima mabavyo tumechimba hasa

vijijini, unaweza ukachimba kisima kimoja, visima viwili, visima vile kama tunaweza tukachukulia kwamba ndiyo vinatoa maji safi na salama kwa kijiji kizima tutakuwa tumefanya makosa makubwa sana. Tunataka tuone ni kwa kiasi gani tumetekeleza Ilani ya CCM ya kuweza kusogeza huduma za maji karibu na wananchi angalau kwa mita 400. Basi utakapokuja Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango tuone tumetekeleza Ilani kwa kiasi gani katika eneo hili la miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika sekta ya elimu. Wananchi wetu wamejitahidi kwa muda mrefu zaidi ya miaka mitano katika kujenga miundombinu ya elimu ikiwa ni pamoja na madarasa, nyumba za walimu na maabara.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin Monko malizia.

**MHE. JUSTIN M. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali tufanye juhudi za makusudi kukamilisha miradi hii ya wananchi ambayo imekwishakuanza na kuwatia moyo wananchi wetu waendeleo kuchangia kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia uliyonipa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Justin Monko. Kama nilivyokuwa nimesema, sasa atafuata Mheshimiwa Mussa Mbarouk na Mheshimiwa Joel Mwaka ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia afya njema na kuweza kuendelea na shughuli zetu za Bunge kama kawaida. Pili, wakati wote sitaacha kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo langu la Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa maendeleo wa Taifa, naanza na viashiria vya uchumi kama vilivyoelezwa katika kitabu alichotusomea Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa mujibu wa takwimu ambazo tumezipata au Taarifa ya Fedha kupitia Shirika la Fedha Duniani (*IMF*) imezungumza kwamba uchumi wa dunia unakua kwa asilimia 3.9 na kwa upande wa Afrika Mashariki, Nchi yetu ya Tanzania na Rwanda ndizo zinazoongoza kwa uchumi wake kukua kwa asilimia 7.2 dhidi ya asilimia 7.1 ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua tu kwamba katika hili, mara nyingi wananchi wamekuwa wakituuliza sisi viongozi tunapopewa takwimu hizi za kukua kwa uchumi lakini mbona tukiangalia sisi wananchi hali kila siku inakuwa afadhali ya jana? Nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na mipango mizuri aliyokuwa nayo ya kukua kwa uchumi lakini uchumi usikue kwenye makaratasi na makabrasha, uchumi ukue mpaka mifukoni kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu mfumuko wa bei kila siku unapanda. Kwa mfano, mwaka jana sukari kilo moja ilikuwa ni kati ya Sh.1,500 mpaka Sh.1,800 lakini sasa hivi mfumuko wa bei umepanda ni Sh.2,600. Ukienda kwenye petroli kwa sisi watumiaji wa vyombo vya moto bei haishuki inaendelea kupaa. Jana bei imepanda tena kwa hapa Dodoma ni takribani Sh.2,445, bei inapanda. Sasa tunapoambiwa uchumi umekuwa hata sisi Wabunge inatushangaza. Naomba hii mipango ya Serikali ifike mpaka kwa wananchi nao waone kwamba kweli uchumi umekua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nalotaka kuzungumzia ni kuhusu hili sual la mikopo na madeni. Kwenye kitabu humu imeandikwa kwamba kuna mikopo tuliyopata kutoka nje takribani shilingi trilioni 7.05. Kati ya hizo kuna deni la ndani na la nje, deni la nje ni takribani shilingi trilioni 1.35, lakini deni la ndani ni karibu trilioni 5.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe katika madeni haya, maneno yale tunayosema kwamba deni ni himilivu kwa kweli tunawadhuru na kuwafilisi wazabuni wanatoa huduma mbalimbali kwa Serikali. Kuna watu wanadai mpaka miaka mitano hawajalipwa, wamepeleka huduma mbalimbali katika sekta mbalimbali za Serikali. Naomba katika mipango yetu hii tuwalipe. Wengine wanapelekwa Mahakamani, wengine mali zao zinapigwa minada hali ya kuwa wameihudumia Serikali yetu. Kwa hiyo, naishauri Serikali iwalipe, kwanza asilimia kubwa ni maskini, wana-*tender* tu hizo za Serikali lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu walipwe madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwenye kitabu alichotusomewa Waziri hapa iko ukurasa wa 12. Nianze na ufuaji wa umeme wa maji (*hydro-electric power*). Tunashukuru Serikali juhudi inazofanya kila siku miradi kuja lakini miradi mingine inakuwa inaishia njiani. Huu mradi wa *Stiegler's Gorge*, naishauri Serikali na kuiomba kwamba iwekeze fedha huu mradi ukamilike isije ikawa kama ule mradi wa gesi wa Mtwara ambao umeanza mpaka umefikia mwisho tunaambiwa watumiaji wa gesi ni asilimia 6 tena ambayo ni *TANESCO* peke yake hali ya kuwa gesi ni kitu kinachohitajika sana katika shughuli mbalimbali duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nishauri Serikali mradi wa *Stiegler's Gorge* ufanikiwe kwa asilimia 100 ili hii Tanzania ya viwanda tunayoisema viwanda bila umeme haviwezi kwenda. Tunaanzisha reli ya *Standard Gauge* ambayo itakuwa ni treni inayotumia umeme kama umeme wetu utakuwa sio wa uhakika iko siku treni itakujaishia katikati ya mbuga ya wanyama ya Mikumi na hapo sasa abiria wajiandae kuliwa na simba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali tunapoanzisha miradi tuihakikishe inakamilika kwa asilimia 100. Nashauri umeme uwe wa uhakika ili wawekezaji wa viwanda watakapokuja wasiwe na matatizo ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine katika huu umeme, bei ya umeme Tanzania ni kubwa kuliko nchi zote. Haya siyo maneno yangu hata Mheshimiwa Rais aliwahi kusema hivi na akaiomba *TANESCO* ipunguze bei ya umeme kusudi wananchi wetu waweze kutumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nikupe mfano, Watanzania ndiyo tunaongoza kwa matumizi ya kuni na mkaa chini ya Jangwa la Sahara. Unaposafiri kati ya mji mmoja kwenda mji mwingine ni Tanzania peke yake ndiyo utakuta pembeni kulia na kushoto mwa barabara kuna magunia ya mkaa na kuni. Tunataka tuondoe matumizi ya kuni na mkaa tutumie umeme na gesi ili tuweze kuokoa misitu yetu ambayo itatuletea mvua za uhakika na tuweze kupata umeme wa kutosha unaotokana na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la utalii. Kwenye utalii hapa naona kama tunafanya mchezo au tunafanya masihara kwa sababu haiingii akilini Tanzania tuna vivutio vingi sana vya utalii, tuna mbuga za wanyama, Mlima Kilimanjaro, Mapango ya Amboni ya Tanga, Tongoni *Ruins* na mambo mengine ya kiutalii lakini hatutangazi, ndiyo tatizo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hapa ilipitishwa bajeti ya shilingi bilioni 2 kama sikosei, mmoja wa Wabunge akatoa mfano Kenya wenzetu wanatumia shilingi bilioni 70 kwa matangazo. Ukiangalia hata matangazo katika ligi za Ulaya katika viwanja vya mipira wenzetu wengine wanatangaza lakini sisi Tanzania kuna tangazo moja ambalo lipo katika *EPL*, ligi ya Uingereza. Kwa nini tusitangaze katika Bundesliga ya Ujerumani, La Liga ya Spain na katika maeneo mengine ambayo yanakusanya watu wengi ili tukaweza kuingiza watalii wengi ambapo sekta ya utalii ni chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali yote duniani kama utasimamiwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali tutangaze utalii wetu, tuna vyanzo vingi vya utalii lakini hatuvifanyii kazi.

Kuna mbuga pekee ya Saadan lakini haitangazwi kama inavyotakiwa kutangazwa. Nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama kweli tunataka mapato kwenye utalii tutumie fedha nyingi sana kwenye matangazo, matangazo ya biashara ndio yanayovutia wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye uvuvi bahari kuu. Kazi yetu kubwa kama Serikali ni kuanzisha operesheni na operesheni ile ilikuja mpaka ndani ya Bunge samaki wakaja wakapimwa kwa rula hapa *canteen* lakini tumeacha meli kubwa zinazovua katika bahari kuu. Wavuvi wadogo wadogo wa kwenye maziwa na bahari tunakamatana nao, nyavu zinakamatwa zinachomwa, nyumba za wavuvi zinachomwa moto na mashua zao zinachomwa moto na kupigwa mashoka, lakini tunaacha meli kubwa zinazovua katika bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai wa hili, miaka michache iliyopita palipatikana samaki wakawa wanaitwa samaki wa Magufuli. Sasa hebu fikiria ikiwa meli moja tu inaweza kuwa na tani 60,000 za samaki wakagaiwa magezani na taasisi mbalimbali za Serikali, je, meli zaidi ya 300 zinazovua sasa hivi tunavyozungumza kwenye bahari yetu na *TRA* hawachukui kodi hata shilingi moja tunapoteza kiasi gani? Kwa nini tuwakamate wavuvi wadogo hali ya kuwa kumbe bahari peke yake ni uchumi kama tutaisimamia vizuri itaweza kutuingizia mapato makubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati yetu tumewahi kupata taarifa kwamba kuna shilingi bilioni 3 za *feasibility study* ambapo inatakiwa ikafanyike uchunguzi tu katika bahari kuu kuona tunawezaje kuwekeza kwenye bahari kuu tuweze kukusanya mapato. Kwa hiyo, naishauri Serikali kama tumeamua kufanya uvuvi katika bahari kuu tununue meli za uvuvi, ndege tulizonunua zimetosha sasa twende kwenye meli za uvuvi ili tuweze kukusanya mapato yanayotokana na bahari yetu. Japan, Singapore, Vietinum,

Thaiwan na China ndiyo wanaonufaika na bahari yetu sisi wenyewe tunaendelea kuwa maskini. Kwa hiyo, naishauri Serikali tununue meli za uvuvi tuanze kuvua katika bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulisema ni suala zima la bandari. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 50 -51 limezungumzwa suala la bandari na reli kwamba kutakuwa na ujenzi wa bandari ya Mwambani Tanga. Mimi naishauri Serikali bandari ile ya Mwambani ijengwe.

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde 30 tu kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zitengwe ili tuweze kujenga bandari ile ambayo nayo itakuwa ni kichocheo cha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho siisahau barabara ya Pangani. Barabara ya Pangani nayo itatuokoa kwanza kuokoa muda wa usafiri lakini pia wakazi wa Tanga watumia muda mfupi sasa kutoka Tanga hadi Dar es Salaam kwa sababu barabara ya Pangani ni njia ya *shortcut*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nasema nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Joel Mwaka na atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Massay.



**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumza masuala muhimu kwa kuipongeza kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake yote ya Fedha na Mipango. Nami sitabaki nyuma, naomba nichukue nafasi kuipongeza sana Wizara hii na Waziri mwenyewe kwa kazi kubwa kwa mpango huu waliotuletea hapa mbele. Ni mpango unaoonekana kabisa unaenda kutuvusha maana tuna lengo la kuvusha Tanzania toka hapa tulipo kuipeleka kuwa Tanzania ya viwanda ili tuingie katika uchumi wa kati mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba nijikite katika masuala matatu hivi katika kitabu hiki tulichopewa cha Mapendekezo ya Mpango, kwanza nizungumzie suala la elimu. Suala la elimu kama ilivyoorodheshwa katika kipengele namba 4.5.1.1(b), kuboresha mazingira ya utoaji elimu katika ngazi za shule za awali, shule za msingi, shule za sekondari ikijumlisha ujenzi wa madarasa, mabweni na maabara, hili ni jambo zuri sana. Tunapozungumza kutaka kulivusha Taifa kutoka hapa kuingia katika uchumi wa kati elimu ni kitu cha msingi sana. Elimu yetu ni lazima ianzie huko chini awali, msingi, sekondari baadaye ndiyo tunakuja kupata elimu za ujuzi na stadi mbalimbali pamoja na elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa wananchi wa Tanzania wamekuwa wakijitolea sana kufanya shughuli za maendeleo kuunga mkono Serikali yao katika sekta hii ya elimu. Wamezungumza baadhi ya wasemaji waliopita kwamba wananchi wamejitolea wamejenga shule yamebaki maboma, wamejenga zahanati yamebaki maboma, wamefanya kazi nyingi sana lakini yamebaki maboma, Serikali ina mpango gani juu ya hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napenda kabisa niungane na wazungumzaji waliopita nikim-*cite* ndugu yangu

Mheshimiwa Kanyasu kwamba Serikali ina haja ya kufikiria sasa inafanya nini na maboma haya yanayobaki kila wakati. Halmashauri zetu hazina uwezo, haziwezi hata dakika moja, maboma ni mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hilo halitoshi kuna suala zima la watu kujikusuru, wamejenga madarasa mawili kwa uchache ili tusiendelee kuweka maboma mengi, unajenga madarasa mawili mnaezeka mnayaweka sawa. Mkitaka kuanzisha shule, tumesikia shule zina wanafunzi wengi sana wa kuzidi kabisa haifai shule kuwa na wanafunzi 7,000 lakini wananchi wetu wanajitolea wamejenga madarasa mawili wanataka kuisajili shule haiwezekani, sasa tunafanya nini? Siyo tunawavunja nguvu kweli, tunawavunja moyo badala ya kuwatia moyo kwa kuzisajili hizi shule labda na kuwaambia tunaomba kila baada ya mwaka basi muongeze madarasa mawili mengine mzisajili shule ziweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule nyingi ambazo zimekamilika lakini madarasa mawili hajijasajiliwa. Kwa hili kwa kweli ningeshauri Serikali hebu iliangalie kwa kina shule zote ambazo zimekamilika zikiwa na madarasa hayajafika hayo sita zisajiliwe ili wanafunzi waanze kusoma. Tuambizane tu kwamba kila mwaka tujitahidi tuweze kuongeza madarasa mengine pamoja na nyumba za walimu ili tuweze kusonga mbele. Hilo ni kwa upande wa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la pili la maji na afya. Maji ni muhimu sana ili wananchi wetu wawe na afya bora. Wananchi wetu wakiwa na afya bora wataweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na katika kuisukuma nchi kuivusha kutoka hali hii ya uchumi tuliyonayo hadi uchumi wa kati lakini maji safi na salama ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishangaa ukiangalia kwa kiasi kikubwa sana vyanzo vya maji na salama ama vinatokana na mito ama vinatokana na mabwawa yaliyojengwa kama hivi tunaona kuna mabwawa ya Farkwa

yanatakiwa kujengwa huo lakini wewe ni shahidi Kanda yetu ya Kati, Dodoma maji chini ya ardhi ni mengi sana. Mji wa Dodoma kwa wasiojua unapata maji siyo ya bwawa, siyo ya mto, maji yanatoka kwenye visima kule Mzakwe kwa Mji wote wa Dodoma. Hii ni kudhihirisha kwamba chini ya ardhi Dodoma kuna maji mengi. Sasa inashangaza, nenda vijijini kwetu watu wana shida ya maji kwa nini Serikali isiweke nguvu ya makusudi kuchimba visima vya uhakika kila kijiji ili watu wapate maji safi, wawe na afya bora na washiriki katika kuleta maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie suala la maji na kilimo. Tunazungumzia kuivusha nchi hii kwenda kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda vinavyotegemea kilimo. Kama kilimo chetu tutategemea mvua nadhani hapo tumepotea njia. Kilimo chetu lazima kiwe kilimo cha uhakika. Kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji ama utatumia mabwawa lakini kwa Dodoma kama tunavyoendelea kusema Dodoma maji chini ni mengi Serikali ifanye juhudi ya makusudi maeneo fulani fulani ichimbe visima kwa ajili ya vijana kufanya shughuli za umwagiliaji na uzalishaji ambao utalisha viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee suala zima la umeme. Tunapozungumzia Tanzania ya viwanda maana yake tunazungumzia umeme lakini umeme bado ni tatizo sehemu kubwa sana vijijini yaani tunataka kusema kwamba maendeleo yaje mjini vijijini hapana. Naipongeza sana Serikali kwa mpango mzima wa *REA* ambao unakwenda kwa kasi vijijini naomba kasi yake iongezwe ili hivi viwanda ambavyo vimeshamiri mijini pia vikapatikane huko vijijini na mambo mengine ya uzalishaji yapatikane vijini badala ya kila jambo kuja mjini. Mazao yazalishwe vijijini yaje mjini kuchakatwa, kwa nini yasichakatwe huko huko, mjini zijie ama *semi-finished product* au *finished products* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, mchango wangu ni huo, maoni yangu ni hayo Mheshimiwa Waziri kama akiyachukua akiyafanyia kazi nitashukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joel Mwaka, Mbunge wa Chilonwa. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Flatei Massay atafutiwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali ambayo kimsingi imeonyesha njia. Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa hii Awamu ya Tano kwa kweli nitakuwa mchoyo sana kama sijaweza kumpongeza kwa kazi anazozifanya. Ukiangalia wako wanaombeza hasa katika suala la kununua ndege, ukiangalia sasa hivi kwa kweli mimi mwenyewe nafurahia sana kuona hali hii ambako leo Tanzania tunaweza kuona huko angani ndege zinapishana na sisi tunasafiri. Naamua kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ajili ya hili. Wako wanaobeza juhudi hizi kuonekana kwamba kipaumbele chetu sio ndege lakini ukweli ukiona baba amenunua kitu fulani nyumbani unaamua kumpongeza kwa sababu tu kwanza fedha zinatumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si vibaya nikampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi anazozifanya. Kwa kweli ni namuona mara nyingi katika shughuli za Serikali hasa kwenye maeneo yetu anapofanya ziara za kuhimiza maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi sasa naomba niende kutoa mchango wangu katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa 2019/2020. Kuna mambo ambayo Mheshimiwa Dkt. Mpango anapaswa aangalie kwenye mpango huu. Nimeangalia sana na kusoma kitabu hiki cha mpango ukiangalia miradi mingi kwa kweli imetekelezwa. Ukurasa wa 31 anaonyesha miradi 1,595 ya maji imekamilika, kwa hili nimpongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado sasa tu natakiwa kuongeza kasi zaidi kwa sababu miradi hii tunayoiita miradi ya maji, kimsingi visima vingi vimechimbwa kila mahali na maeneo mengi sana kwenye maeneo yetu miradi hii haikuisha, imeishia nusu mengine 90%, mingine 40% hasa

ukiangalia miradi hii mingi imeanza miaka mingi. Kwa hiyo, tusipoweka mipango ya kuimalizia miradi hii ni wazi thamani ya shilingi inashuka na miradi hii inakuwa ghali kwa maana hiyo Serikali inapata hasara hata ukipanga bajeti ya namna gani inaweza kuwa shida kumaliza miradi hii vizuri na wananchi wakapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri ni vizuri tunapopanga mipango yetu hii na tunapopanga fedha ziende kwa wakati ili wakandarasi walipwe wanapomaliza ili iweze kuhudumia wananchi na wakati huo basi inakuwa na kiwango kile kile kilichokusudiwa kumaliza mradi. Hii itasaidia pia katika uchumi wa nchi yetu, tutakuwa hatutumii fedha nyingi ambazo hazikukadiriwa kwa sababu unapochelewa kumaliza mradi ni wazi kabisa ule mradi unapanda gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye eneo hili la miundombinu. Kwanza kwa kweli naipongeza Serikali kwa eneo hili la miundombinu barabara nyingi zimejengwa, maeneo mengi sasa yanapitika. Kuna eneo ambalo nalipongeza, Mheshimiwa Rais amefungua Daraja la Sibiti ambalo ukiangalia kwa kanda hii ya Simiyu, Shinyanga kuja mpaka Singida na Manyara kwenda upande wa Arusha utakuwa umetengeneza njia nyingine ya kupeleka usafiri wa hakika kwa wakulima au wafanyabiashara. Kwa hiyo, nashauri fedha zitengwe ili walau lile Daraja la Sibiti linalojengwa limalizike ili barabara hiyo inayokuja Singida inayopita Manyara inayokwenda moja kwa moja mpaka Arusha ifanye kazi kwani ni njia rahisi utakuwa umeokoa kilomita 200 kuliko kupitia Singida kwenda Babati kwenda Arusha kwa njia ile. Kwa hiyo, nilitaka nimuongeze ndugu yangu ili alielewe hili, barabara ile inapopita maeneo yale itakuwa na tija kubwa sana kwa maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi za Serikali, naona wazi na natambua juhudi za Serikali hasa katika suala la elimu. Niipongeze pia Serikali kwa kutenga

shilingi bilioni 20.9 kila mwezi kwenda kwenye elimu bure, kwa kweli kwa hili mnastahili pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi elimu ya msingi imeboreka na mambo yanaenda si vibaya na elimu ya sekondari vilevile, lakini tunapoenda kwenye vyuo na kuhitaji wataalam kwenye viwanda tunayo kasoro kidogo katika mitaala. Ni vizuri kutafuta wataalam na kubadilisha *modules* zetu katika ufundishaji wa vyuo vyetu hivi, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambayo itasaidia kupatikana kwa wataalam watakaosaidia katika viwanda vyetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafundi mchundo, mafundi sanifu, hatuwezi kuwapata kama *module* na ile mitaala iliyopo katika vile vyuo vyetu itabaki vilevile. Ukiangalia China waliweza kufanya kazi nzuri wakati wa mapinduzi yao kwenda kwenye uchumi wa kati. Ukiangalia historia yao walitumia ujanja wa kufundisha wataalam wao ili wataalam hao wakaweze ku-*cover* kwenye kufanya shughuli za viwandani. Ukiangalia leo hii hata sufuria tunazopikia nchini hapa zinatengenezwa Kenya na maeneo mengine lakini tukiwa na watu wetu tukawafundisha ni rahisi basi tukawa na wataalam ambao watatengeneza vyombo hivi na viwanda vyetu vitapata wataalam na hivyo, tutakuwa tumewapatia watu wetu kazi na vijana watapata ajira na pia viwanda vyetu vitainuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote katika kilimo tunahitaji kufanya jambo moja ambalo ni rahisi kulifikiri, hatuwezi kutegemea kilimo cha mvua. Nchi nyingine ukiangalia na sisi bahati nzuri tuna mvua nyingi za kutosha, tuangalie namna ya kuzuia mvua zinazonyesha kipindi cha masika ili kuwa na mabwawa mengi tukalima kilimo ambacho kinaweza kusaidia. Kilimo cha mabwawa, tutakuwa tunazalisha kila mwaka na kwa vipindi mbalimbali bila kutegemea mvua, kwa hali hii itasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa nimeona kwenye mpango huu kwa kiasi kidogo sana umezungumzia kilimo lakini kilimo kinabeba kwa kweli eneo kubwa la Mtanzania.

Watanzania wengi wanatumia kilimo zaidi ya asilimia sitini na kitu mpaka sabaini. Kwa hiyo, ukielekeza nguvu nyingi kwenye kilimo Mheshimiwa Dkt. Mpango utakuwa umesaidia Watanzania wengi ambao kimsingi tunategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niipongeze pia Serikali kwa kutekeleza huu mpango wa *REA* Vijijini. *REA* tatizo lake ni moja tu, wakandarasi wanadai hawana fedha, sasa sina hakika kama Serikali haiwalipi au ni nini kilichopo. Hakuna kiwanda bila umeme, tukitaka tuweze kuzalisha vizuri ni vizuri tukapeleka umeme kwenye viwanda vyetu na hii miradi ya mkakati kwa kweli tusipoangalia itakuwa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi wengi sana saa hizi wanalia habari ya kutokuwa na fedha, sasa sina hakika kwenye mpango uliopita nini kilifanyika, lakini sasa hivi tunaona kabisa yako maeneo mengi wakandarasi wanasuasua. Sasa niombe fedha tunazozipanga mara nyingi ziende moja kwa moja kwenye mpango na tunapopanga tupange nini tunafanya na kipi ni kipaumbele.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri hata mkijisikiliza tu ninyi wenyewe mnapaswa kuona aibu na kupunguza sauti hizo, yaani mnaji-*regulate* tu wenyewe. Endelea Mheshimiwa Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, kizuri ukishaweza kuziba sehemu hii ya wakandarasi hawa hakika mambo yataenda vizuri na Tanzania ya viwanda itapatikana ikiwa Serikali itawekeza katika suala la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo niliwahi kushauri zamani kwenye mpango uliopita suala la gesi. Nimewahi kutembelea sana na kuangalia miradi hii ya gesi, sina hakika wapi imepotelea lakini nimeiona imendikwa kidogo kwenye ukurasa huu wa 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumepata matumaini sana gesi inaweza kusaidia nchi hii, hasa

kutupatia fedha za kigeni au kwa matumizi ya kawaida. Tungeweza kusaidia lakini tuone nini changamoto hasa za gesi ili tupate namna ya kusogea mbele ili...

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massay, malizia.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa hili, nitakuwa mchoyo sana kama sijasema suala la mifugo na wafugaji. Tuone namna ya kuisaidia mifugo na wafugaji kwani kwa kufanya hivyo mambo yataenda vizuri sana. Mifugo yenyewe, kwa mfano ng'ombe kila kitu ni thamani kuanzia ngozi, maziwa, kwato na kadhalika, tukiweza kuweka viwanda ambavyo vitachakata mazao haya ya mifugo hakika Tanzania itasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa anafuata Mheshimiwa Charles Kitwanga na baada yake Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi. Kwanza nianze kabisa kwa kuipongeza Serikali kwa mpango huu ambao kwa kweli umeendana na *Vision* yetu 2020-2025 ambayo tumeikatakata katika vipingili vya miaka mitano-mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili suala tunalosema kwamba pesa zimepungua. Kwa kweli, nilichukua muda kuzungumza na wataalam wa Benki Kuu walichoniambia *money in circulation* zinaendana na uchumi na hakuna hata siku moja tumeweza kupungua bali siku zote pesa zinaongezeka. Ikabidi nipige kichwa niweze kufikiria ni kwa nini watu wanasema pesa zimepungua? Tofauti iliyopo



sasa hivi na zamani ni kwamba kila hela unayoipata ni lazima uwe umeifanyia kazi. Siku za nyuma wakati mwingine hii magumashi zilikuwa nyingi tunapatapata hela ambazo tulikuwa hatuzifanyii kazi, tufanyeni kazi pesa tutapata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuunge mkono huu mpango kwa sababu wote tuliupitisha kama Mpango wa Miaka sasa umekuja katika mpango wa mwaka mmoja ili tuweze kufanya utekelezaji wake. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi anavyotekeleza maana tukianza kufikiria wengine kabla hatujazaliwa reli iliyokuwepo ilijengwa na Mjerumani lakini kwa sasa hivi tunajenga reli hii wenyewe na tunajenga sisi Watanzania kwa pesa zetu, hata kama tumekopa. Unaweza ukawa una hela zako kwa kukusanya kodi au unaweza ukawa na hela zako kwa kukopa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuangalia nini nikishauri Serikali ili tuweze kuweka tija zaidi katika uchumi wetu. La kwanza ni katika utekelezaji, je, ni namna gani tutaongeza *money in circulation* ndani yetu? Ni kweli tuna miradi mikubwa, kwa mfano, tuna ujenzi wa reli yetu, makampuni yanayojenga pale ni ya nje, malipo yatakayofanyika pesa zile zinaweza zikaenda nje, tulenge nini sasa? Kwa sababu Serikali ni moja, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Ardhi na watu wote, pale tunapokuwa tunamuajiri mkandarasi wa nje tuhakikishe kazi ambazo zinaweza zikafanywa na wakandarasi wa ndani, wapewe wakandarasi wa ndani ili wakilipwa hizo pesa zibaki hapa na ziende kwenye mzunguko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie katika upande wa madini. Ukiangalia akina nani hasahasa wanaweza ku-*contribute*, ukiangalia mwenye mradi wa madini, *asset* kubwa aliyonayo ni madini yaliyopo chini, kinachofuatia ni ile pesa, kinachofuatia ni ule utalam aliokuwanao. Sasa madini kama yana-*contribute* sehemu kubwa basi wenzetu wa Wizara ya Madini wawaangalie wachimbaji wadogowadogo na wachimbaji wa kati

ambao ni Watanzania tuwawezeshe waweze kuchimba na hela nyingi zibaki katika maeneo yetu. Hicho ndicho ninachoweza kuishauri Serikali katika mpango wetu huu kwa ajili ya ku-*make sure* kwamba hizi pesa tunazozipata na huu uchumi mzuri ambao tunao sisi Watanzania leo hii unawafaidisha Watanzania hata kule Koromije. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie sekta ya utalii. Niiombe Serikali iweke nguvu sana katika Shirika letu la Ndege la Tanzania. Watu wanazungumzia Shirika la Ndege la Tanzania lakini *contribution* yake huwezi ukajua itakuwaje pale litakapokuwa na nguvu. Kwa mfano, chukua jirani zetu wa Kenya, wanaruka moja kwa moja mpaka New York, wanaleta watalii moja kwa moja wao wenyewe. Nchi yetu kama itakuwa na Shirika la Ndege lenye uwezo na lenye nguvu watakaporuka mpaka pale *Julius Nyerere International Airport* kutakuwa na ndege nyingine itakayoruka kuwachukua watalii kuwapeleka Mwanza ambapo ni karibu na Serengeti. Watakapowafikisha pale Mwanza kutakuwa na mtu kutoka Koromije mwenye *Pick-up* yake, mwenye *Landrover* yake, atakayewabeba watalii na kuwapeleka Serengeti. Uchumi utakuwa umeshuka mpaka kwa mtu wa Koromije kule chini. Wasiojua ni wale wa upande huu, eleweni. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Umeanza eeh?

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Kwani nimesema upande gani?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa msikilize vizuri, shule hiyo.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Kwani nimesema upande gani? Nimesema upande huu, mbona wanajishuku? (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muwe mnavumilia mambo madogo madogo, ukiguswa tu, yaani ukitekenywa tayari ushaamka.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa, taarifa.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Charles Kitwanga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, taarifa.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye *local companies*, tuchukulie mfano mzuri tu ambao nimeuona wa ujenzi wa barabara kutoka...

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anayezungumza alikuwa Waziri, tunataka tumpe taarifa kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muache aendelee analizie mchango wake.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa.

**MWENYEKITI:** Unataka kuchafua hali ya hewa tu, haina sababu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sichafui, sichafui.

**MWENYEKITI:** Naomba ukae basi bwana, endelea Mheshimiwa Kitwanga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi...

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mzuri mmoja tu ambao watu wataweza kuona jinsi ambavyo pesa zitazidi kubaki hapa Tanzania. Kuna Kampuni ya *ESTIM* inayojenga barabara kutoka Ubungo mpaka nadhani Kibaha, ile ni kampuni ya Kitanzania na pesa zitakazopatikana pale nyingi zitabaki, lakini ukipita pale utafikiria ni kampuni ya nje, hamna tofauti. Kwa hivyo, niwaombe ndugu zangu waliokaa huku mbele, mliokaa huku mbele kidogo mlitambue hilo na mshirikiane na mimi nilikuwa nikikaa zamani, bado nyie ni wenzangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kusema Mtanzania anayependa nchi yake ataitumikia nchi yake mahali popote. *Let me say this thing once and for all, I have never been in this House drunk, I will never do that and it will never happen.* Mnaoendelea kusema hivyo, endeleeni na mtaendelea mpaka Yesu atakapokuja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kitu kingine cha muhimu zaidi ambacho...

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Hebu nawaomba tuwe na kusikilizana kiasi fulani. Unajua shida yetu hapa watu wengi hatufahamiani, Mheshimiwa Charles Kitwanga *is not a light weight, yah, kabisa, he is somebody.* Kwa hiyo, siyo kama anavyofikiri jamaa yangu ooh alikuwa Waziri, huyo yuko vizuri. Endelea Mheshimiwa Charles Kitwanga. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa *complement*. Niendeleo kuzungumzia kitu kingine ambacho ni cha muhimu sana kwa Taifa letu, ni hili tunalolizungumzia la *Stieglers' Gorge*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya ndiyo dakika zimeisha. Nilitamani uendelee kidogo lakini dakika zimeisha. Mheshimiwa Saada Mkuya nimeshakutaja.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi)*

Baada ya Mheshimiwa Saada Mkuya atafuata Mheshimiwa Mary Muro.

**MHE. SAADA SALUM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa hii ya kuchangia mpango wetu wa maendeleo. Kidhati kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake na watendaji ambao wamewezesha kutuletea kitabu hiki kwa sababu natambua kwamba, siyo kazi rahisi, lakini imewezekana na imekuja tumeanza kujadili toka juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maeneo machache ya kuzungumza. Nianze kwa kutambua *achievement* moja ambayo imepatikana katika Serikali ya Awamu iliyopita na Awamu hii, hususan katika utekelezaji wa mipango yetu kwa upande wa *establishment* na *implementation* kwa *Tanzania Agricultural Development Bank* ambayo imekuwepo kwa lengo la kusaidia ukuaji wa kilimo kupitia katika sekta mbalimbali lakini vilevile kupitia kwa *individual*. Mheshimiwa Mbene alizungumza *despite* kwamba *TADB* ipo na inaendelea na utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kifedha lakini bado tabu ipo palepale. Kwa maana kwamba *individual* ambaye amejishirikisha na kilimo akitaka kupata mkopo gharama inakuwa kubwa kwa sababu kwanza *TADB requirement* yao lazima upitie *PASS (Private Agricultural Sector Support)* ili wakuandikie *plan* ambayo mara nyingine inakuwa *very expensive* kwa mtu ambaye anataka *production* kwenye kilimo. Tumeweka hiyo *TADB* lakini masharti yake yamekuwa sawasawa na benki nyinginezo, kwa hiyo, utaona kwamba kumekuwa na ugumu uleule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ingekuwa vizuri kama tumeweka *TADB* kwa ajili ya kusaidia kilimo isiwe *TADB* inafanana na *commercial banks* nyingine. Lazima kuwe kuna utaratibu ambao umewekwa *specifically* kwa ajili ya kuwapatia mikopo. Inawezekana kabisa *rate* ni ndogo *TADB* ukilinganisha na *banks* nyingine lakini ile gharama ya *acquisition* ya mkopo yenyewe inakuwa ni kubwa kwa sababu anakumbana na vikwazo vingi. Kwa hivyo, tunaomba *TADB* utaratibu wa kuwakopesha wakulima pamoja na kampuni zinazojishughulisha na kilimo uangaliwe upya ili tuweze kuona kwamba tunafikia malengo tunayokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia ni katika ukurasa wa 42, uhibitaji wa katika matumizi ya fedha za umma, imetokana vilevile na ukurasa wa 41, mahitaji ya rasilimali fedha. Ni jambo zuri katika mambo yote yaliyotajwa kwamba kuhakikisha kuwa kampuni zote ambazo Serikali ina hisa zinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kutoa gawio stahiki kwa Serikali. Ni jambo zuri sana na mimi napata moyo sana kwenye hili kwa sababu kuna sehemu nyingine ambapo Serikali tumekuwa na hisa lakini kweli hatupati gawio kama inavyokusudiwa. Tunaweza kuwa tunapata gawio lakini sio kama inavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nimkumbushe Mheshimiwa Dkt. Mpango, kuna mashirika mengine ya Serikali ambayo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanatoa gawio, Zanzibar haijawahi kupata stahiki yake katika magawio ambayo yapo katika mashirika ya Muungano. Tunaomba katika usimamizi wa utaratibu huu kwa mpango huu Zanzibar iwe inapata gawio stahiki kutokana na mashirika ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo Zanzibar ni sehemu yake nayo inaingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hilo tu, vilevile katika usimamizi wa taasisi na mashirika ya umma, tuhakikishe mashirika ya umma yanajiendesha kibiashara, yanaandaa mwongozo wa gawio utakaotoa utaratibu wa malipo ya

gawio kwa Serikali. Hili limeanza kufanyika, nadhani tumeshuhudia sio mbali Mheshimiwa Rais akipokea gawio kutoka katika mashirika yetu ya umma. Kuna mashirika baadhi ya mashirika ni ya Muungano lakini Zanzibar kabisa haijapata senti katika gawio ambalo limetolewa na ni gawio stahiki kabisa kwa hivyo, tunaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa taasisi ya umma ambayo inatoa gawio ni Benki Kuu ya Tanzania, hakuna gawio lingine linalotoka katika taasisi nyingine. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuanzia mwaka huu wa fedha Zanzibar iwe inapata stahiki yake kama ilivyo kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huu umetambua sana umuhimu wa miundombinu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi. Katika *aspect* hiyo, imeongelea kabisa ujenzi wa bandari, ujenzi wa barabara pamoja na viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati nachangia mpango na niliuliza kwa nini mpango huu hauja-*integrate* Zanzibar, nilipata majibu ambayo kwa wakati ule pengine yalikuwa *valid* kwamba katika Katiba iliyopendekezwa tunakusudia kuweka Tume moja ambayo itashughulikia mipango. Sasa hivi hatuna matumaini ya Katiba Mpya, Mheshimiwa Dkt. Mpango tunafanya nini, *as a follow back position?* Kwa sababu huu mpango Zanzibar haimo ni sawa, lakini utekelezaji wake kwa namna yoyote uta-*integrate* masuala ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya bandari, kuna barua imeandikwa sijui toka lini kwa ajili ya *acquisition* ya mkopo kutoka Exim Bank ya China kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri Zanzibar. *Document* inakwenda inarudi, kwa Mwanasheria imerudi, kwa maoni ya Kamati imerudi, kwa *NDMC* imerudi, miaka nenda miaka rudi. Kwa taarifa nilizozidi-*dig out* hii Bandari ya Mpiga Duri imeanza kuzungumzwa miaka 25 iliyopita, hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bandari ni kichocheo kikubwa sana cha uchumi hususani uchumi wa visiwa, tunaomba vile unavyo-*feel* kwamba huu mpango *aspect* yake kubwa ni pamoja na miundombinu, *feel* kwa Zanzibar *aspect* ya ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri. *Aspect* ya ujenzi wa *Terminal III* iko katika ngazi zenu, tunaomba mliangalie hili ili sasa na uchumi wa Zanzibar ambao hauja-*integrate* humu kwenye mpango na wenyewe uweze kuendelea kutokana na mipango ile ambayo itatekelezwa. Tunaweza kule kutengeneza mpango lakini unahusika na wewe moja kwa moja, tunaomba sana hili lizingatiwe tena lizingatiwe kweli kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni nadhani na wao wanafanya *research* na wanakuja na *alternative*. Kuna taarifa hapa imenishtua kidogo hususani ukurasa wa kwanza wanasema kwamba kiwango cha umaskini Tanzania kimefikia asilimia 47, hii ni taarifa ya kutisha na haiwezekani kabisa. Wakati tunafanya *research* zetu ni lazima tuangalie vyanzo sahihi vya *information* kwa sababu *document* hii wanaweza wakaja wengine wakasema kama ni *reference document*. Unaandika taarifa ambayo tumem-*quote* William Atwell, mimi nimekuwa *very much interested* nimekwenda kumtafuta huyu William Attwell ni nani? Yeye mwenyewe katika taarifa ambayo iko kwenye *website* ya *Frontteers Strategy Group* amekuwa *quoted* huyu hiyo asilimia 47 ameipata yeye kutokana na *recent visit* yake kwa East African countries. *How could you just to have a recent visit* ukaweza kupata *estimate* ya 47% ya *population*. Nadhani *this is very wrong*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jumba lina dhamana kubwa katika nchi hii. Sina uhakika kwenye Kanuni zetu lakini *just* kutoa taarifa kwenye *blogs* halafu tunakuja tunazileta hapa ndiyo zisaidie maendeleo ya Taifa hili, *it's just very wrong*. Tunatarajia takwimu sahihi katika vyanzo vya kuaminika. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nimekwenda kwenye *website* ya *World Bank*, taarifa ambayo imetolewa mwaka 2017 inasema Tanzania *basic poverty line* ni 28% lakini *food poverty line* ni 10%. Sasa tunasema hii 47% imepatikana wapi? Tunaomba sana pamoja na mambo mengine Kanuni zetu ziwe zinazingatia takwimu sahihi kwa sababu wananchi wanaotuamini wanaweza waka-*quote* hii kama ni takwimu sahihi, hususani kwenye hizi *blogs* inakuwa ni mawazo ya mtu mwenyewe binafsi *rather than* kuwa takwimu sahihi. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saada.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Ooh, ooh! Kwani nimemaliza?

**MWENYEKITI:** Muda hauko upande wako, ahsante sana.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Ooh!

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Nilishamtaja Mheshimiwa Mary Muro dakika tano.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Najua kabisa dakika zangu ni chache, nina mambo machache sana ya kushauri kwa ajili ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natambua kabisa kwamba enzi za Mwalimu Nyerere alipotoa ile kauli mbiu ya Kilimo ni Uti wa Mgongo, alimaanisha kwamba binadamu huwezi kutembea bila uti wa mgongo na ukawa hai. Kwa maana hiyo kama tunafahamu kabisa kwamba kilimo ni uti wa mgongo, ningemshauri Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango yafuatayo na inatokana na kile ambacho nakiona kwenye kilimo kwa wakati huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mwalimu Nyerere aliposema Kilimo ni Uti wa Mgongo, alihakikisha

katika maeneo mbalimbali anawasaidia wananchi kulima kisasa. Kwa mfano, natoka Pwani, alihakikisha Bonde la Ruvu linatoa mpunga wa kulisha karibu Dar es Salaam nzima na Tanzania kwa ujumla. Leo hii ukipita Kibaha ukafika Ruvu, utakuta lile bonde limegeuzwa kuwa viwanja vya kujenga nyumba. Nataka kujua hivi tumeshabadilisha lile shamba la Ruvu kuwa la ujenzi? Wakati Waziri ana *windup* atujulishe basi kama lile bonde ambalo tulikuwa tunapata mpunga na tunanunua chakula kwa bei nafuu kama limebadilishiwa matumizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye viwanda nimeona Pwani tunaongoza kwa viwanda, lakini kinachonishangaza pale Kibaha kuna matrekta, wananchi wa Tanzania ili tuweze kuondokana na kilimo cha jembe, tulitarajia kwamba Serikali itakuja na mpango angalau wa kuanzisha hata *SACCOS* wakopeshwe yale matrekta waweze kulima kilimo cha kisasa ili tuendane na ule mpango wa Rais wa Awamu ya Kwanza wa kauli ya mbiu ya kusema kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Matrekta yale yanaoza pale Kibaha hayajulikani yatapaki kwa muda gani na wananchi wanalima kwa jembe la mkono na ni wa Kibaha pale pale. Hakuna maelezo yale matrekta yametengenezwa halafu yanaenda wapi, mwaka juzi yalikuwepo pale pale, mwaka jana yako pale pale lakini tuna Tanzania ya viwanda. Sasa ukianza kujjuliza nini maana ya Tanzania ya viwanda, kama ni Tanzania ya viwanda...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

**WABUNGE FULANI:** Ana dakika tano tu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nampa taarifa mzungumzaji..

**MWENYEKITI:** Tutatunza dakika zako Mheshimiwa Mary Muro.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nampa mzungumzaji taarifa...

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo Mheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Si ulininyima mimi.

**MWENYEKITI:** Zima kidogo *microphone*, ahsante sana. Mheshimiwa Keissy.

## T A A R I F A

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa mzungumzaji taarifa kwamba matrekta walikopeshwa na baadhi ya Wabunge wanadaiwa, Serikali ilitoa matrekta tena *JKT*. Serikali ilifanya juhudi sana kugawa matrekta bure kila kijiji lakini mpaka sasa *SUMA JKT* inadai watu na baadhi yao ni Wabunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Muro, alikuwa anawashauri tu Wabunge wanaodaiwa matrekta walipe.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sikubaliani na hiyo taarifa kwa sababu mimi nimesema hivi, sasa hivi ni Tanzania ya viwanda na kile Kiwanda cha pale Kibaha hakijaanza enzi hizo za Wabunge walipokopa, yale matrekta yametengenezwa siku za karibuni, tunahitaji yatumike ili uti wa mgongo uwe ni kilimo. Hatuwezi kuwa na vijana ambao hawana kazi, Bonde la Ruvu limechukuliwa linajengwa nyumba, matrekta ambayo tulitarajia yagawiwe kwa wananchi yamepaki pale, halafu tuseme kuna Tanzania ya viwanda na kwamba tutawakwamua wananchi kwenye umaskini? Hicho ndicho nilichokuwa nakizungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia kuhusu *PPP*. Natambua...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Jamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma nimekuona.

**WABUNGE FULANI:** Aaah, kuna ubaguzi.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa mzungumzaji kwamba kwa kuwa mara nyingi tunapokuwa tunajadili mipango, huwa wanatoka nje haelewi, namshauri aje ajifunze kwenye Halmashauri zetu kule Geita, tayari tunakopeshwa matrekta kwa sababu tumeshafuta taratibu na tumeshaunda vikundi na matrekta yale yanatoka kwa mkopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Juzi niliona pale Mwanza yakigaiwa matrekta na Waziri wa Kilimo sijui alikuwa anawagawia watu gani wale zaidi ya trekta 50 lakini wazo lako ni zuri sana tunalipokea kwa kweli.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kukubali ile taarifa, mimi naongelea mpango ambao una mambo mengi, kwake kwenyewe hata maji hamna, sasa tunataka mwananchi ajikwamue ili hizi rasilimali nyingine ziende mahali kwingine zikafanye kazi. Kwa hiyo, mtani wangu siwezi kumkubalia hilo. Mimi nilikuwa naelezea kwamba tuko vizuri katika kupanga mipango lakini katika kutekeleza lazima tuchukue hatua za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongelea kuhusu PPP. Nafahamu kabisa kama tungetumia PPP ina maana tungeweza kubakiza akiba ya pesa tukafanya mambo mengine kulikoni kila kitu kufanya sisi kama Serikali. Tunachukulia mfano kwamba mpaka sasa hivi haijajulikana kama reli na *Stiegler's Gorge* vinajengwa kwa pesa za ndani au kwa mkopo? Hata tunapoulizwa na wanachi tunashindwa kujibu kwa sababu, mara tuambiwe inajengwa kwa mkopo, mara tuambiwe inajengwa kwa pesa za ndani, kipi ni kipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda Mheshimiwa Dkt. Mpango ukija ku-*windup* utuambie kabisa hii miradi ya kimkakati inafanywa kwa pesa za ndani au kwa pesa za mkopo au kwa pesa za ndani pamoja na pesa za mkopo? Hilo tutaielewa ili tuweze kuwaelimisha wananchi kwamba jamani tunafanya hili kwa pesa za mkopo na kwa hili tunafanya kwa pesa za ndani. Hii itasaidia suala hili kueleweka kuliko kufanya propaganda kwamba tuna hela nyingi sana wakati wananchi wanaishi kwa shida, tuna hela nyingi sana wakati tungeweza kufanya kwa PPP tukaokoa hela. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwishwa kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, dakika zako zilikuwa tano tu.

**MBUNGE FULANI:** Zimeingiliwa.

**MWENYEKITI:** Zimeshaisha.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili zangu.

**MWENYEKITI:** Unga mkono basi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Kiteto Koshuma atafuatiwa na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na Mheshimiwa Papian ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuendelea kutoa michango yangu katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa utangulizi ufuatao. Sasa tunaelekea mwisho wa miaka

mitano ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2016 - 2021 na sasa tuko katika Mpango wa Nne ambao ndiyo tuko tunaujadili sasa hivi. Naomba wakati tunajadili Mpango huu wa Nne wa Maendeleo ya Taifa, naomba tuangalie baadhi ya mambo ambayo kama itapendeza Wizara kama walivyoahidi katika kitabu chao kwamba wanachukua maoni yetu kwa sababu haya ni Mapendekezo ya Mpango, kwa hiyo, kama itawapendeza kuchukua mawazo yangu basi nitashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kuangalia hali ya uchumi katika Taifa hili la Tanzania. Hali ya uchumi katika Taifa hili la Tanzania kutokana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri, anasema kwamba hali ya uchumi imeimarika. Hata hivyo, ukiangalia hali ya uchumi wa mwananchi mmoja mmoja bado ni duni, *purchasing* na *buying power* ya wananchi imepungua na iko chini sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa hali ya kawaida kwa sasa hivi, kwanza kabisa vifaa vya ujenzi vimepanda bei kiasi kwamba mwananchi tu wa kawaida hata kujenga nyumba inamuwia vigumu. Ukiangalia katika zile *basic needs*, nyumba ni kitu cha msingi sana lakini maisha ya mwananchi bado yako duni kiasi kwamba hawezi kuwa na uwezo wa kujenga nyumba kwa sababu vifaa vya ujenzi vimepanda bei. Hata katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba mfumuko wa bei kwa sasa hivi umepungua. Ni kweli katika vitu vidogo vidogo kama vile vyakula lakini masuala yale ya msingi ambayo yanaweza kusaidia mwananchi kuwa na maendeleo hali bado sio nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vilevile wakati uchumi wa Taifa wenyewe unakua lakini uchumi wa wananchi unaendelea kuwa duni, bado wapo wezi, mimi nawaita wezi. Kumezuka janga kwa hawa watu wenye hizi *betting centers*, nitazitaja, sasa hivi kuna Tatu Mzuka, Premier Bet, Moja Bet na Biko, hawa wote ni wezi ambao wanaiba fedha za wananchi katika mifuko yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hawa ni wezi kwa sababu hiki wanachokifanya ni sawasawa na upatu. Sisi wenyewe wananchi ndiyo tunatoa pesa zetu halafu baadaye wanatokea wanatangaza kwamba kuna mshindi ameshinda shilingi milioni 100. Hata hivyo, ukiangalia wananchi ndiyo wame-*contribute* zile fedha, zimefika shilingi bilioni moja huyu mtu amekusanya, kwa kuwa yeye hana mtaji, halafu mwisho wa siku sasa, wananchi kwenye mifuko yao wanabaki bila fedha, halafu anatokea mtu mmoja anatangazwa mshindi anachukua shilingi milioni 100 yeye katajirika. Huu ni wizi wa waziwazi kabisa, mimi nimeangalia nimeona hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kuishauri Serikali kwamba sasa tunapojadili Mpango huu wa Nne hebu tuangalie tunasaidiaje wananchi kutoka katika hali ya umaskini ili waweze kujikomboa na kuwa na maisha mazuri. Kwa sababu hauwezi ukajinadi ukasema kwamba uchumi wa nchi unakua wakati hali ya wananchi wako inazidi kuwa duni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali kama ikipendeza wachukue maoni haya, waweke mkakati wa kuhakikisha wanazi-*control* hizi *betting centers*.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Waangalie ni kwa namna gani hizi *betting centers*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma unapewa taarifa na Msukuma mwenzi, Mheshimiwa Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa dada yangu Mheshimiwa Kiteto kwamba hawa watu wanaohusika na michezo ya ku-*bet* wapo kwa mujibu wa sheria za Tanzania na wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria ambayo tulitunga humu humu Bungeni. Kwa hiyo, siyo kwamba wanafanya wizi. Ahsante.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mdogo wangu Mheshimiwa Salome na naamini kabisa ame-*scrutinize* kitu ambacho amekisema kabla hajanipa taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa hawa watu wa *betting centers* wapo kisheria lakini mimi naangalia ni namna gani wanaiba fedha katika mifuko ya wananchi. Ndiyo maana naendelea kuishauri Serikali iangalie ni namna gani wanaweza kuzi-*control* hizi *betting centers* ili wasiendeleo kuchukua fedha katika mifuko ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo.

**MWENYEKITI:** Jamani hebu tumsikilize Mheshimiwa, unaweza ukawepo kisheria na bado ukawa mwizi tu.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Kabisa.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeshaishauri Serikali iangalie *controlling* ya hizo *betting centers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutokana na hali ya wananchi wetu kuendelea kuwa duni, *solution* mojawapo ambayo Serikali inaweza kuifanya ni kuongeza *Government expenditure*. Serikali ijitahidi katika kuhakikisha kwamba inatumia sana ili kule chini mzunguko wa fedha uendeleo kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ambapo sasa tunaenda katika Mpango huu wa Nne, ukiangalia fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu haziendi. Waheshimiwa Wabunge wataniunga mkono kwa sababu wamekuwa wakisema mara kwa mara humu ndani kwamba fedha za maendeleo katika Halmashauri zetu haziendi, ni sifuri kabisa. Sasa unategemea ni kwa namna gani hawa wananchi wanaweza wakawa na maendeleo wakati fedha za



maendeleo kwenye Halmashauri haziendi, ina maana kule kwenye Halmashauri zetu hakuna miradi yoyote ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri katika changamoto ambazo amezisema, amesema changamoto mojawapo ni kutokuweza kuwalipa wakandarasi wa ndani pamoja na wazabuni mbalimbali. Nashauri Serikali basi iweze kuweka mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba wakandarasi na hawa wazabuni wanalipwa kwa wakati ili wananchi waweze kuwa na mzunguko wa fedha waweze kujikimu kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nionglee suala la deni la Taifa. Mara kwa mara nimekuwa nikiongelea suala la deni la Taifa na leo sitaweza kuliongelea kwa muda mrefu kwa sababu ya muda kutoniruhusu. Deni la Taifa tunaliona linaendelea kuongezeka. Kwa taarifa ambazo siyo rasmi, deni letu la Taifa sasa limeongezeka kwa asilimia 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipingani kwamba tusikope, tukope lakini lazima tuweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunaweka *control* ya ukomo wa deni. Tusiwe tunakaa tunasema kwamba deni letu ni stahimilivu na hivyo tuendeleo tu kukopa pasipokuwa na mpango mkakati wa ukomo wa kukopa, tutakopa mpaka shilingi ngapi na tunavyozikopa hizo fedha tutazikopa kwa sababu ya nini? Ningefurahi sana tunapotengeneza Mpango huu wa Nne tuangalie ni kwa namna gani tunali-*control* deni letu la Taifa ili lisiendeleo kuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi karibia asilimia 35 ya mapato ya ndani inatumika kulipa deni la Taifa. Hii inasababisha baadhi ya miradi kuzorota na kutoweza kukamilika kwa wakati. Kwa hiyo, nashauri Serikali iangalie namna gani ya kuweza kuli-*control* deni hili la Taifa ili tusije tukajikuta tunaingia katika nchi ambazo na zenyewe zimeingia katika *debt stress*, zimepata *stress* ya madeni. Ukiangalia nchi kama Mozambique wamekuwa wakikopa

na kukopa, Serikali inakuwa inasema kwamba deni ni stahimilivu hatimaye sasa hivi Mozambique imeletewa kuwa ni nchi ambayo imeingia katika *debt stress*. Sitapenda Serikali ya Tanzania au nchi ya Tanzania iingie katika kuwa na *debt stress*. Kwa hiyo, nashauri Serikali iweke *good management* ya deni letu la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama muda wangu unaruhusu, naomba Serikali iweke mkakati wa kuwakikisha kwamba wanaachana na suala la kukopa mikopo ambayo ina riba kubwa, wakope mikopo yenye riba nafuu ili tuweze kuwa na uwezo wa *services* deni letu. Kwa maana kwamba tukifanya hivyo, basi tunaweza kuchochea maendeleo ya wananchi katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine naomba kushauri Serikali ijitahidi kuwawezesha wataalam kupata mafunzo ya *negotiation skills* ili wanapoenda kujadili mikataba ya kukopa haya madeni ya Taifa waangalie zile *contract* ambazo wanaweka kwamba zina manufaa gani katika nchi yetu. Sasa hivi China amekuwa anakopesha nchi za Afrika na China ni mjanja sana anamkopesha mpaka Mmarekani lakini anapokuja kuzikopesha nchi za Afrika anajuwa sisi hatuna *negotiation skills*, kwa hiyo, yeye analeta masharti yake na sisi tunayakubali wakati yale masharti yanakuwa siyo mazuri. Unakuta Mchina anakukopesha halafu anakwambia wafanyakazi wake ndiyo wafanye kazi wakati sisi wananchi wetu wapo na wana uwezo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiteto, malizia sentensi moja.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naiomba Serikali iweze kuangalia wanapokwenda kujadili mikataba ya kimataifa kuhusu mikopo wajue wanakopa kwa ajili gani, kwa sababu gani na mikopo ya bei nafuu. Nashukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Jamani, jamani, Mheshimiwa Kiteto huwa anasema mawazo yake na ni mawazo mazuri tu, hamna kibaya alichoongea. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, mwisho atakuwa Mheshimiwa Emmanuel Papian.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu katika Mpango wa Bajeti wa 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nishukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa miradi mikubwa ambayo inaendelea nchi nzima lakini *specifically* katika Mkoa wangu wa Dar es Salaam. Kuna mambo mengi ambayo yamefanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam, tuna barabara za juu lakini pia hata hii treni ambayo inajengwa sasa hivi ya kisasa imepita kwenye Mkoa wetu wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuishukuru Wizara ya Afya kwa kuleta pesa katika Jimbo langu la Segerea kwa ajili ya vituo vya afya. Vilevile nimshukuru Waziri wa Miundombinu kuhakikisha kwamba Jimbo la Segerea linakuwa na miundombinu mingi, japokuwa tuna changamoto chache lakini naamini kabisa mtazimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, sasa naomba nitoe mchango wangu katika mpango wa 2019/2020 . Nashauri mpango utakaokuja 2019/2020 kuwepo na mpango wa kibajeti wa kuhakikisha kwamba tunamaliza mafuriko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam japokuwa sasa hivi siyo mji mkuu wa Serikali lakini bado ni mji maarufu na mji ambao unaiongezea kipato kikubwa Tanzania. Mafuriko yanapotokea kwanza yanaathiri uchumi, uchumi wa mtu mmoja mmoja lakini pia hata uchumi wa Serikali. Kama juzi hapa kulikuwa na mafuriko tuliona hata

mabasi yetu mengi yalishindwa kutembea lakini pia wafanyabiashara walifunga maduka yao lakini siyo tu kwa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Mikoa ya Dodoma, Morogoro pamoja na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri katika mpango unaokuja basi aweze kuweka mpango wa kibajeti wa kuweza kumaliza kabisa mafuriko haya ili wananchi waweze kukaa au wafanyabiashara waweze kufanya biashara zao vizuri na Taifa liweze kupata kipato. Kwa sababu tunapokuwa tunayashughulikia haya mambo wakati yanapotokea tunashindwa kuyamaliza. Kwa hiyo, nashauri sana kuwepo na mpango kwa ajili ya kumaliza mafuriko katika mikoa ambayo nimeitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nashauri kuwepo na mpango wa kurasimisha makazi holela ambayo yapo kwenye mikoa tofauti tofauti kama Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa mingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango aje na mpango wa kuweza kushirikisha wadau na sekta binafsi ambao wanaweza wakaongea na hawa watu ambao wako kwenye makazi holela waweze kushirikiana nao, aidha, kuwajengea nyumba kwa kuingia nao ubia labda anaweza kupewa *apartment* moja halafu nyingine wakachukua hao watu wanaojenga kwa ajili ya kusaidia kuondoa hao watu makazi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapoweza kuingia ubia na hawa wananchi ambao wanakaa kwenye makazi holela basi hata uchumi unaweza kukua kwa sababu kwanza tunawaongezea thamani ya maeneo yao lakini pia lile eneo ambalo tunaliita makazi holela linakuwa limetoka. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango aweze kuja na mpango ambao utaweza kuwasaidia wananchi ambao wanakaa kwenye makazi holela washirikiane nao kwa ajili ya kuwajengea nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilichokuwa nataka kuongelea ni kwa ajili ya kutengeneza miundombinu.

Mheshimiwa Waziri aje na miundombinu rafiki kwa wajasiliamali wetu ambao wako Dar es Salaam kama mama ntilie, bodaboda, waweze kuwatengenezea miundombinu rafiki. Hawa watu hii ndiyo ajira yao, mfano bodaboda wapo Tanzania nzima na ajira nyingi ya vijana sasa hivi imekuwa ni bodaboda. Sasa hivi kinachoendelea ni kwamba wanapata ajali nyingi lakini pia wamekuwa na matatizo ya hapa na pale mara wanakamatwa na mambo kama hayo. Kama Mheshimiwa Waziri akija na mpango wa kuwatengenezea miundombinu mizuri ambapo wenyewe watakuwa wanapita lakini pia kuwatambua kwamba Dar es Salaam nina bodaboda kadhaa, hiyo pia itaisaidia Serikali kuweza kupata kipato wanapolipa kodi kujulikana kwamba hawa bodaboda wapo wapi sambamba na mama ntilie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nataka niongelee kuhusiana na suala vijana wetu wanaomaliza vyuo. Vijana wetu ambao wanaomaliza vyuo wamejengwa katika mazingira kwamba unapomaliza chuo moja kwa moja unaenda kuajiriwa. Tofauti na watu ambao wamesoma ualimu, udaktari na vitu ambavyo unaweza ukaenda ukaajiriwa, mfano, kama mtu amesoma udaktari, anaweza akaajiriwa kwenye hospitali binafsi, mtu ambaye amesomea ualimu anaweza akaajiriwa shule binafsi lakini wale waliosoma sayansi, Serikali ije na mpango wa kuwajenga ili wakimaliza chuo wajue kwamba wanakuja kujiajiri na siyo kwamba wanakuja kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema sasa hivi tunajiandaa kwa ajili ya kwenda kwenye uchumi wa kati, vijana wetu wengi hawawezi kushindana na vijana ambao wanatoka *East Africa* kwenye kufanya kazi. Mfano kama sasa hivi tunasema Serikali ya Awamu ya Tano ni ya viwanda lakini hatujawaandaa wale vijana kwamba wakimaliza tu chuo waje kufanya kazi kwenye viwanda, wanaishia tu kupata kazi ambazo ni za vibarua na kazi nyingine ambazo haziwezi kuwasaidia kiuchumi ili kupata wanachokipata. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje na mpango wa kuangalia vijana wetu ambao wanamaliza vyuo

waweze kujajiri wenyewe na isiwe wanamaliza chuo kwa ajili ya kuajiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bonnah Kaluwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papian.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naipongeza Serikali kwa kazi zote inazozifanya na jinsi mpango huu ulivyotengenezwa na unavyotupa *direction* ya wapi tunapokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema jambo moja kwamba kwenye mpango huu sijaona ule mradi wa umeme wa Kakono ambao unazalisha *megawatts* 78. Benki ya Maendeleo ya Afrika ilishamaliza kazi yake na kuna vitu vilikuwa vinaendelea lakini siuoni kwenye mpango hapa. Waziri atakapokuja atuambie huu mpango umefikia wapi kwa sababu *megawatts* 78 siyo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji linaonekana kwa nchi ni tatizo kubwa sana. Nashauri tuongeze Sh.50 kwenye mambo ya simu, tulete hizi pesa kwenye maji baada ya miaka miwili tutakuwa hatuna madeni lakini miradi mingi ya maji nchini itakuwa imemalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo nataka kushauri kwamba tunaweza kuigawa nchi yetu kwa *zone*, nimeona kwenye mpango hapa ukionyesha mikoa tofauti tofauti, tuigawe nchi yetu kwenye *zone* lakini tunapofanya *zoning* tutengeneze zile *agro-processing centers* huko huko ambazo zitaweza kuwa-*managed* na Watanzania na *foreigners* watakaokuja ku-*invest* pesa zao wakae na Watanzania huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hawa *investors* watakaokuja kwenye hizo *agro-processing plant* katika maeneo hayo washirikiane na Watanzania. Kama Mtanzania

anaweza kuingiza 30% aendelee yule mwekezaji akija na 50% aendelee, 20% iwe ni ya wale *outgrowers* wadogo wadogo waweze ku-*manage* uchumi kwenye vile viwanda vitakavyokuwa kwenye maeneo hayo ili *growth* ya *economy* iende sambamba na uhalisia wa maisha ya watu wetu tunaowaona kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi ita-*protect* wale wakulima wadogo kwa sababu tulipobinafsisha hivi viwanda vya chai anazalisha ile chai yake akimaliza ana-*determine* chai *price* ya yule mkulima ambaye ni *outgrowers*. Kwa hiyo, mwisho wa siku yeye akisema anapunguza bei anapunguza kwa sababu *already* ana mashamba. Suala hili naomba Serikali ilianganalie sana kwamba anakuwa na kiwanda, hana *involvement* na *shareholders* wadogo mwisho wa siku lazima awanyonye na awaamulie anavyotaka, atawamaliza na mwisho wataning'inia bila mazao yao kununuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili litasaidia jambo lingine kwamba hata kama atakuwa na hicho kiwanda atazalisha mwisho wa siku atakachofanya chochote kile kwa sababu *outgrowers* wetu na wao wana *share* pale ni wanufaika wa ile *income* atakayopata. Kwa maana hiyo, itatusaidia hata ku-*protect price* ya wale wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine hawa *foreigners* watakapokuja nao watatusaidia ku-*oversee* masoko ya nje ya haya mazao tunayozalisha. Leo tumepata shida ya mbaazi kwa sababu hatuna watu nje. Leo tunapata shida ya korosho ni kwa sababu hatuna watu nje lakini ingekuwa tunabangua korosho hizi siasa uchwara usingezisikia Mtwara, usingesikia udalali, usingesikia kelele pale Mtwara kwenye korosho kwa sababu wale wakulima wenyewe wangukuwa ni *shareholders* kwenye zile *agro-processing plants* ambapo ni *beneficiary*, nani angezalisha siasa pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Uganda inakwenda kuwa nchi ya kwanza Afrika kwenye uzalishwaji wa maziwa

na teknolojia wameichukua Tanzania *ten years back*. Niombe Mheshimiwa Waziri hebu tafuta timu ya watu kutoka Ofisi yako ya Mipango, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TIC, Benki ya Kilimo na Benki Kuu, *team up* hawa watu waangalie ni mbinu gani tunaweza kuzitumia kuhakikisha kwamba Tanzania inaweza kuwa *the biggest producer of milk* Barani Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda leo wana-*export* zaidi maziwa na kwenye *contribution* ya uchumi wao sasa hivi maziwa yanaenda kuiondoa kahawa na chai, kahawa inaenda kuwa ya tatu, chai inakuwa ya pili na maziwa yanakuwa ya kwanza. Ukiangalia *ecological area* na *environment* yetu sisi tuna maeneo makubwa lakini yenye *weather* sawa na Uganda, kwa nini hatujafanikiwa kwenye sekta hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Dkt. Mpango asije kusema tunahitaji *big investment* kwenye hili, hakuna pesa nyingi. Shida tunayoipata ni kwamba hatuna *access* ya *grants* kwenye *agro-business* na kwa wakulima wetu. *East Africa* Tanzania ni ya mwisho ku-*access grants*, Ulaya watu wanashusha *grants* Kenya na kwenye nchi nyingine, wanaweka miundombinu na vitu vyote wakimaliza wanakwambia wewe fanya kazi, maisha ya raia wao wanakuwa vizuri wewe unakusanya kodi. Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa usije kutuambia unahitaji hela, hakuna hela, wale watu wana uwezo wa kua-*access grants*. *Team up your people* waende wakafanye kazi hizo na sisi wakulima wetu *wa-access grants* waweze kufanya kazi na sisi tupate msaada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Dkt. Mpango wala usije ukatuambia chochote nenda katafute washauri Marekani hata wapi waje wakushauri wakuambie ni mipango gani inatufaa. Wewe usitusikilize sisi wanasiasa, panga pangua, panga vitu vyako sisi tunataka kuondoka kwenye umaskini na hizi shida tulizonazo. (Makofi)



## T A A R I F A

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Papian, kuna huyu bwana nikimnyima taarifa hii, anapenda kweli taarifa, haya ngoja tukusikie Mweshimiwa.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nafahamu na Wabunge wote tunafahamu kwamba kazi ya Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali. Leo tunaona mjumbe mmoja anasema kwamba asisikilize ushauri wa Wabunge, akatafute washauri wengine nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampa taarifa tu kwamba kazi yetu itabaki pale pale kuishauri na kuisimamia Serikali na Mheshimiwa Dkt. Mpango lazima ushaurike na kupokea ushauri wa Wabunge kwa sababu ndiyo kazi yetu hiyo. Nilikuwa nampa taarifa tu huyu ndugu yangu mzungumzaji wa sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea kuchangia.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema wanasiasa siyo Wabunge, maana hata kule mtaani tuna wanasiasa kwani wanasiasa ni sisi peke yetu tuliomo humu ndani? Hatuna waandishi wa habari wanaamka asubuhi wanatangaza ya kwao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namshauri Waziri wangu, mambo mengine usiwe unatuaga, wewe nenda kachape kazi tunatafuta maendeleo, hapa tunakuja kuku-*support* mambo mengine tu. Wewe unatuaga kufanya nini?

Tafuta pesa na wataalam huko watusaidie, Tanzania hatuwezi kuifunga, hii siyo kisiwa, nchi imeshakwenda na duniani nyingine, Watanzania wanatakiwa watoke na wapate ajira. Tafuta *technical persons* watusaidie, sisi siyo kisiwa, siyo kwamba ni wajinga lakini kupata ushauri na akili ni kuhemea *brain*, unaingiza hapa tunapata maisha, watu wanahitaji kubadilika, wewe tusaide. Mtu mwingine akija kwako analeta siasa unamskiliza, nunua *ream* za karatasi mwambie nenda kaniandike ya kwako kwenye makaratasi akupe nafasi ya kufanya kazi uweze kupumua. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kushauri jambo lingine la mwisho kwamba Watanzania hawafanyi kazi. Nchi nyingine *they are working over night*, kadiri wanavyofanya kazi usiku na mchana ndivyo zile mashine zinatema kodi. Saa nne tumelala, saa mbili tayari, Dar es Salaam saa tatu wako barazani wanazungumza habari ya wanawake, mama ana tako, mama ni mnene, utafanya lini hiyo biashara, utapata kodi saa ngapi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe na Bunge hili mnikubalie nchi hii ifanye kazi usiku na mchana. Watu waondoke kwenye ufuska na kufikiria mawazo mabaya na kutukanana hovy hovy, tufanye kazi, watu wafanye kazi mchana na usiku. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Kariakoo nzima leo, ukaamua maduka yote fungueni mchana na usiku, *you are creating employment to our graduates* ambao wako mtaani wanacheza na simu. Vilevile una-*create employment* kwa watu ambao ni *jobless* wanafanya kazi mchana wengine wanafanya kazi usiku, tunaongeza ajira, *shift* zinakuwa mchana na usiku halafu kodi inaendelea kukusanywa. Kwani saa nane usiku mashine ya *EFD* haito risiti, inatoa. Je, wewe Mheshimiwa Dkt. Mpango haupati fedha? Nashauri tuanze biashara usiku na mchana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri jambo lingine kwamba huu mpango wetu sisi twende kushauri Serikali lakini tusibeze yale yanayofanyika.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa Papian.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nashauri kwamba Benki ya Kilimo *TADB*, niungane na Mheshimiwa Saada, Mheshimiwa Dkt. Mpango angalia ni namna gani unaweza kufanya isiwe kama *commecial bank* iendane na hali halisi ya mazingira ya Watanzania, waweze kukopesheka vinginevyo zile pesa zitakaa pale, utalaumu watendaji, utawafukuza, utajiri wengine na pesa hazitatoka. Mheshimiwa Waziri angalia ni namna gani ya kushusha zile pesa katika mfumo ambao ni *reasonable*. Utamwambia aandike *business plan* na yeye ana heka zake mia mbili anataka akakope trekta na *TADB* inatakiwa impe hela *PASS im-garantee* atatokea wapi? Punguzeni masharti, angalieni ni namna gani ya kui-*handle* ile benki ili iweze kwenda sambamba na *life brain* na stahili za wakulima wetu kule kwenye *grassroot*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Emmanuel Papian kwa ushauri uliokuwa unatoa. Haya mambo ya kilimo anayokushauri Mheshimiwa Papian basi ujue ni mkulima mkubwa, kwa hiyo, anazungumza kutokana na uzoefu kabisa wa kilimo hasa katika maeneo yetu haya.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa uchangiaji ambao tumeufanya toka asubuhi. Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

### MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni 68(7) kuhusu jambo ambalo limetokea leo ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Bwege anachangia hapa ndani alitoa taarifa kwamba alichukua familia ya mtu anayedai kwamba alifiwa na ndugu yake aliyeuawa na Polisi na akawapeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wakati wanajadiliana na Waziri Mkuu, Waziri Mkuu alionyesha ku-*sympathise* na kuonyesha kwamba kuna makosa yamefanyika, lugha inayofanana na hiyo kwa sababu sina *Hansard* hapa, ningependa kui-*quote* ile lugha vizuri lakini yenye mwelekeo huo na Kiti chako kinaweza kikanisaidia katika lugha ile aliyoitumia Mheshimiwa Mbunge akithibitisha kwamba alikutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu alieleza hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini nachofahamu, kwa sababu niko pale kusaidia shughuli za Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati wa kuratibu wageni waliokuwa wanamtembelea Mheshimiwa Waziri Mkuu katika jambo hilo, hao wageni walipokwenda kwake Mheshimiwa Waziri Mkuu alichogiza ni kwamba, kwa kuwa taarifa za matukio hayo ziko mikononi mwa Polisi na ingefaa kila mtu asubiri taarifa ambazo zinafanyiwa uchunguzi kwa mujibu wa sheria na Polisi zitakapotoka ndipo ukweli wa jambo hilo uweze kubainika na utaratibu rasmi wa kisheria uweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili limezungumzwa ndani ya Bunge na kwa uzito ule ambao umezungumzwa na hasa linampomgusa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni katika masuala ambayo uchunguzi unaendelea na vyombo vinavyohusika, ningependa tu kupata mwongozo kwa nini jambo hili labda

lisingeondolewa kabisa kwenye *Hansard* ya mazungumzo ya leo ili kuondoa *records* ambazo siyo sahihi na hazina uelekeo wa uhalisia wa jambo lenyewe kwa kuzingatia yale yaliyojiri siku ya ugeni huo ulipomtembelea Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mheshimiwa Bungara yupo?

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**SPIKA:** Basi Mheshimiwa Waziri wa Nchi mimi nilipokee hili, kwa wakati muafaka tutampa nafasi ili aweke vizuri jambo lake na kama anaweka msisitizo basi afanye hivyo halafu tutaona hatua gani nyingine zitakazofuata. Kwa sababu hatujapata nafasi ya kumsikia tena tuwe na uvumilivu kidogo lakini ni jambo ambalo tutaendelea kulifuatilia humu humu ndani kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli za leo zimekamili na wachangiaji karibu wote wamepata nafasi, yeyote ambaye jina lake hakulisikia kwa namna moja au nyingine ajiorodheshe tena kesho na tutaendelea na uchangiaji wetu kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 9 Novemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*